
# HUU NDIO
# UISLAMU





Picha ya angani ya Waislamu wakielekea Al Kaaba ambayo Mwenyezi Mungu alimuamuru Nabii Ibrahim kuijenga na kuamuru Waislamu kuielekea katika Swala zao popote watakapokua.

ح دار الدليل المعاصر للنشر والتوزيع ، ١٤٤٣هـ

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

باهمام ، فهد بن سالم
هذا هو الإسلام باللغة السواحلية. / فهد بن سالم باهمام - الرياض ،١٤٤٣هـ
١٥٦ ص ، ٢٢ X ١٥ سم
ردمك: ٦-٥-٩١٤٠٨-٦٠٣-٩٧٨

١- الاسلام - مبادئ عامة أ.العنوان
ديوي ٢١١ ١٤٤٣/١٦١٦

رقم الإيداع : ١٤٤٣/١٦١٦
ردمك: ٦-٥-٩١٤٠٨-٦٠٣-٩٧٨

**Chapa ya kwanza**
2021
Haki miliki zimehifadhiwa na shirika
la ***Dalili al Mu'a-swir***

# HUU NDIO
# UISLAMU

Fahad Bin Salim Bahammam



- **Hivi** huoni umuhimu wa kuiona taswira sahihi iliyo bayana ya ubora wa Dini yenye kujadiliwa zaidi kwenye vyombo vya habari duniyani?
- **Hivi** huoni haja ya kutulia na kuitambua kwa kina Dini inayoenea kwa kasi duniani na inayo kubalika kwa haraka kwa mujibu wa takwimu za kimataifa
- **Hivi** wewe hupati raha katika kuvumbua na kuzifahamu tamaduni za watu wengine na falsafa zao kuhusu maisha, Dini, na ulimwengu unaotuzunguka?
- **Je utaipa** nafsi yako nafasi kwa ajili ya kutambua maarifa yaliyothibitishwa yahusuyo Dini ya Kiislamu kutoka katika vyanzo vyake vya asili, kisha uyahukumu kwa kutumia uwezo wako wa kufikiri na akili yako?

**Ikiwa unaona hilo ni jmabo muhimu au ni lenye kuvutia basi kitabu hiki chaweza kukusaidia kwenye jambo unalo litaka**

## Ni wapi Qur’ani imetoka?

## 84

Ni suala la kimantiki kabisa lile linalopita katika fikra za watu pale wanapozungumzia Kitabu kitukufu cha Waislamu, Qur’ani na Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama,* wakati mwingine wao huhoji kwa nini sisi tukubali maelezo ya Waislamu kuhusu chanzo chake? Je sisi hatupaswi kuuliza maswali kuhusu hilo?



# Maudhui ya Kitabu


Maswali ambayo yanatufadhaisha wote — 12

- DINI YA KIISLAMU
- MAANA YA NENO LA UISLAM
- UISLAMU NI DINI YA MITUME WOTE

UISLAMU NI DINI YA ULIMWENGU — 16

- KUSHUGHULIKIA MAZINGIRA NI KATIKA SEHEMU YA IMANI
- DINI YA ELIMU
- UISLAMU UNAHUSISHA MAMBO YOTE YA MWANADAMU
- DINI YA MAWASILIANO NA USHIRIKIANO

MUUMBAJI MMOJA MWABUDIWA MMOJA — 32

- KATI YA KANUNI ZA KAWAIDA NA KANUNI ZA SHERIA
- HAKUNA UTAKATIFU KATIKA UISLAMU
- JE KUNA MIIKO MAALUMU YA KUINGIA KATIKA DINI YA UISLAMU

MITUME NI NANI KWA HAKIKA? — 40

- UTU WA MITUME
- UKATI NAKATI KATIKA UTUKUFU WA MITUME
- MSIMAMO WA UISLAMU KUHUSU MITUME

MSIMAMO WA UISLAMU KUHUSU NABII ISA - ALAYHI SALAAM — 44

Ni nani mjumbe wa Uislamu — 50

- Mzunguko wa haraka katika kumtambua Mjumbe wa Uislamu Muhammad juu yake amani

Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kwa mtazamo wa wale waadilifu — 56

Baadhi ya sifa za Mtume Muhammad- *Swallallaahu alayhi wasallama* na maadili yake — 62

- Unyenyekevu
- Huruma
- Uadilifu wake
- Wema na ukarimu wake
- Subira na uvumilivu wake
- Kujizuwia na mambo ya dunia
- Utekelezaji wake wa ahadi

Baadhi ya maneno ya Mtume Muhammad - Swalla Llaahu alayhi wasallama — 72

Qur'ani tukufu iliyo muujiza wa milele — 78

- Muujiza wa kuihifadhi
- Miujiza ya kilugha na maudhui zake

Ni wapi Qur'ani imetoka? — 84


- Tuhuma mbali mbali
- Kwa nini Tusione Hilo kuwa ni Uwezo Mkubwa wa kiakili
- Je inawezekana Qurani ikawa ni kutokana na vitabu vilivyoitangulia?
- Ukweli wa kihistoria
- Kila mmoja na neno lake
- Suratul Faatiha

Nini maana ya ibada mbali mbali katika Uislamu? — 94

- Nguzo za Uislamu
- Kwa nini majukumu hayo?
- Swala ya Kiislamu
- Zaka
- Swaumu
- Hijja

Familia katika Uislamu — 110

- Ndoa na malezi ya familia katika Uislamu
- Uislamu umempa kila mtu katika familia heshima yake awe ni mwanaume au mwanamke
- Uislamu umeweka mkazo katika kuwaheshimu na kuwajali wazazi wote wawili wa kiume na kike katika uhai wao wote
- Amri ya kulinda haki za watoto wa kiume na wa kike na kufanya uadilifu katika kuwahudumia
- Uislamu umeamrisha kutembeleana na kuunga udugu



# Familia katika Uislamu

110

Familia nyingi siku hizi zimegeuka kuwa makundi tu ya watu wenye kuishi katika nyumba moja wenye funguo tofauti.



## UWILI WA AKILI NA DINI

136

Baadhi ya watu, wale wenye fikra finyu, hudhani kwamba Dini ni yenye kupingana na Akili. Kwa sababu dini kwa mtazamo wao ni chimbuko na taswira za hovyo, simulizi za watu wa kale na fikra potofu.

Nafasi ya mwanamke katika Uislamu —— 116

- Mfano wa Sheria mbali mbali zinazohusiana na kumuheshimu mwanamke ni hizi zifuatayo
- Namna Uislamu ulivyomtukuza mwanamke
- Hakuna mgogoro wa kijinsia katika Uislamu
- Uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke katika Uislmu
- Tabia ya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamme katika Uislamu
- Kinachotakiwa katika uhusiano huo
- Kwa nini sheria ya Hijabu kwa ajili ya Kujihifadhi dhidi ya Wanaume?

Kanuni kuhusu vyakula na vinywaji —— 126

- Nguruwe
- Pombe na madawa ya kulevya
- Qur'ani imeharamisha pombe

MAKOSA NA TOBA —— 132

UWILI WA AKILI NA DINI —— 136

- Baadhi ya vikwazo vya tafakuri vinavyowekwa wazi na Qur'ani ni kama ifuatavyo

UISLAMU NI DINI YA AMANI —— 142


- Uislamu ndiyo dini inayoenea kwa kasi hivi leo
- HIVI WATU WALILAZIMISHWA KUINGIA KATIKA UISLAMU

Uislamu na Hali ya baadhi ya Waislamu leo —— 148

- Mtazamo Mpya

# Maswali ambayo yanatufadhaisha wote





Ni nani miongoni mwetu ambaye hajapata kutumia muda mchache katika umri wake kujiuliza,ni kinaendelea ? mimi ni nani, nimetokea wapi, ninakwenda wapi, mwisho wangu ni upi na nini lengo la kupatikana kwa ulimwengu? Taabu yote hii ni ya nini katika dunia ikiwa mwisho ni umauti, mchanga na kutokuwepo?

Waislamu pamoja na watu wenye dini zilizotoka mbinguni wanaamini kuwa maisha ya mwanadamu bila ya kuamini uwepo wa Muumba Aliye Muadilifu, na uwepo wa maisha baada ya haya, ambayo ni ya milele na ndani yake mtu mwema atapata malipo yake ambayo ni Pepo; na muovu atapata adhabu yake, ambayo ni Moto ni upuuzi mtupu bila ya maana , na kujitoa mhanga bila ya malipo wala mapato

Na kwamba haiwezekani kufahamu maisha haya ya migongano na hikma katika maisha ya tabu, na kosa na la sawa na kutaabika, iwe ndiyo kusudio la uwepo wetu! Tunatakiwa kumuamini Allah-Mtukufu Aliye Mola, Muumba, Mfanyaji wa kila jambo, Mwenye Hekima na Mwadilifu, Yeye Amefanya uhai kuwa na mwisho ambao kila mtu atapata fungu lake kwa mujibu wa kile kilichotangulizwa na mikono yake, iwe ni cha heri au shari.

Na wakati huo inakuwa Imani madhubuti nan a ufahamu wake ambao tunalingania watu kama vile uadilifu, upendo, upole, ukweli, uvumilivu na huruma, hapo utakuwa ni uhakika ambao unakubalian na maumbile yetu. na wakati huo changamoto inakuwa na maana yake, na kufaulu kupata tamu yake, na uvumilivu wetu uwe na utamu wake.

Na tunapata yakwamba Qurani, Kitabu kitukufu cha Waislamu kina ashiria hilo Allah-Mtukufu Anatusimulia sisi kuhusu watu wenye akili, wanaotafakari kwa kusema; "*... na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto." Q3:191*

> Huwezi kufahamu tofauti ya Maisha na hekima ya maisha kuwa magumu na kujua la sawa na lamakosa na kuteseka ila pale unapo muamini Mungu kuwa yeye ndie Muumba na mwenye kuyasurufu mambo mwenye Hekima muadilifu

## DINI YA KIISLAMU

Dini nyingi katika ardhi zimepewa majina kwa kunasibishwa na watu, kundi au miji ambayo dini hizo zilidhihiri ndani yake. Dini ya kikristo imechukua jina lake kutoka kwa Masihi (Isa mwana wa Mariyamu) juu yake rehma na amani, dini ya uyahudi inanasibishwa na kabila la Yahudha,na dini ya kibudha inanasibishwa na muanzilishi wake Budha,na wahindu inanasibishwa na nchi ya India, na kadhalika.

Ama kuhusu Uislamu, haunasibishwi na mtu maalumu, au asili fulani, au kundi. Na hilo ni kwasababu si Dini maalumu kwa kundi fulani la watu ili anasibishwe nao, wala haukuzushwa na mtu ili unasibishwe nae. Si vingine isipokuwa umeitwa tu Uislamu.

## MAANA YA NENO LA UISLAM

Tunaporejea katika asili ya neno Uislamu katika lugha ya kiarabu, kwa hakika limekusanya maana inayozunguka kati ya kujisalimisha, kunyenyekea, kutii, kutakasa kwa nia, amani ama utulivu.

Uislamu ni kujisalimisha kwa Allah Mtukufu kikamilifu na utiifu kwa Mola Aliye Muumba, Mmiliki na kujikomboa kutoka kila aina ya utumwa kwa mwingine asiyekuwa Yeye.

Na hii ndiyo maana iliyotiliwa mkazo katika Aya kadhaa ndani ya Qur'ani,

Qur'ani inavyotufahamisha;

Kwamba yeyote atakayemwelekea Allah Mtukufu kwa moyo wake na viungo vyake, akanyenyekea na kujisalimisha Kwake, akatekeleza maamrisho na makatazo Yake, hakika atakuwa ameshika kamba madhubuti isiyo katika na atafuzu kwa kila kitu.

*"Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu." Q31:22*

Hivyo basi Uislamu ni utumwa kamili kwa ajili ya ALLAH . na ni uhuru kutokana na kumnyenyekea na kua mtumwa kwa asiyekua yeye, na Muislamu ni mwanaadamu anaefanya ibada yake kwa kuitakasa nia yake, na ambae anaishi amani katika nafsi yake, na anaeneza amani kwa walio kando yake.

**Lakini je hayo ndiyo waliyokuja nayo Mitume wote?**

## UISLAMU NI DINI YA MITUME WOTE

Qur'ani inathibitisha kwamba nyumati zote katika zama mbali mbali walipelekewa Mitume waliowafundisha wao Dini ya Allah Mtukufu, na Mtume Muhammad amani iwe juu yake ameelezwa ndani ya Qur'ani ;

*"Hakika Sisi Tumekutuma wewe kwa Haki, kuwa ni mbashiri na mwonyaji. Na hapana umma wowote ila ulipata mwonyaji kati yao." (Q35:24)*

Mitume wote walikuja na Dini ya haki na wao hawatofautiani katika ujumbe wa Imani na misingi ya hukumu na tabia.

Na Uislamu aliokuja nao Mtume wa mwisho, Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama kabla ya miaka zaidi ya elfu moja na mia nne ni mwendelezo wa Dini waliyokuja nayo wale Mitume waliyomtangulia; na Qur'ani inawaamrisha waislamu waamini yale waliyotumwa nayo wale Mitume waliopita kama vile Nabii Ibrahim-Alayhi salaam, Nabii Ishaqa-Alayhi salaam, Nabii Yakobo-Alayhi salaam, na Nabii Isa-Alayhi salaam;

*"Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu Kwake." (Q2:136)*

Na katika yenye kutia mkazo ni kuwa Qur'ani imetusimulia sisi usia wa Nabii Ibrahimu-Alayhi salaam, baba wa manabii, kwa wanawe, na mfano wake ni Nabii Ya'aquub kwa wanawe wakati alipokaribia kufariki duniya kwa kuwaambia - hakika Allah Mtukufu Amekuchagulieni nyinyi Dini ya haki kuweni imara katika Uislamu mpaka mtakapofikiwa na kifo; *"Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu." (Q2:132)*

Kwa ushahidi huu Dini hii ni mwendelezo wa Dini ya Manabii wote. Itikadi ni moja haibadiliki katika asili yake, bali mabadiliko ni katika sharia na upambanuzi wa hukumu kwa kwenda sawa na hali za zama mbali mbali, mpaka alipotumilizwa duniyani Mjumbe wa mwisho aliye Mtukufu wa daraja Mtume Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama, ili aweke sharia ya mwisho kwa watu wote.

Na hapa Qur'ani inathibitisha kwa uwazi kuwa dini ni moja nayo ni Uislamu, na kuwa hizi tofauti tunazozishuhudia kati ya watu wenye kufuata dini zilizotoka mbinguni katika upande wa itikadi, hapana ila ni upotoshaji ndio uliowaweka wao mbali na yale waliyokuja nayo Mitume wao.

*"Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Na walio pewa Kitabu hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia ujuzi, kwa sababu ya uhasidi ulio kuwa baina yao. Na anaye zikataa Ishara za Mwenyezi Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu." (Q3:19)*



# UISLAMU NI DINI YA ULIMWENGU



Jambo

Jambo la kushangaza ni kuwa Qur'ani haikutaja neno Waarabu pamoja na kuwa imeteremka kwa lugha yao, na Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* alitumwa akiwa kwao; na tunakuta leo hii Waarabu ni sehemu ndogo tu kati ya waislamu waliyo ulimwenguni, bali wapo chini ya asilimia 20 kwa mujibu wa sensa ya waislamu; na nchi iliyo na waislamu wengi duniyani ni Indonesia, nchi iliyo mwisho wa kusini mashariki mwa bara la Asia; bali jimbo moja la wa waislamu katika nchi ya India peke yake unakaribia kuzishinda nchi nyingi za Kiarabu kwa pamoja.

Dini ya Kiislamu imekuja kuwa ni rehema na muongozo kwa mataifa yote yaliyo tofauti katika tamaduni zao, asili zao, desturi zao na miji yao kama ilivyokuja katika Qur'ani: *"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote."* (Q21:107)


Uislamu unatanguliza mtazamo wa uwepo wa tofauti za watu kwa namna ambayo haijawahi kujulikana na mfumo mwingine, wala hawajapata kuuzoea mataifa ya watu.

Tutazame kwa makini maelekezo ya Qur'ani ambayo kimsingi hayawasemeshi waarabu tu wala waislamu peke yao bali ni maelezo kwa watu wote kwa kuzingatia asili zao zote bila ya kujali madhehebu zao;

*"Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na Tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye khabari."* (Q49:13)

Na kwa mafundisho hayo Qur'ani inathibitisha kuwa watu wote vyovyote watakavyokuwa rangi zao na asili zao wao wote ni watoto wa Nabii Adamu na Bibi Hawa - Juu yao wote wawili amani, na kwamba tofauti na aina ambazo zilizo kati yao si kwa ajili ya ubora, na si vingine ila ni kwa ajili ya kujuana, kushirikiana na kusaidiana, lakini ubora na kukirimiwa kuliko adhimu kutakuwa kwa yule aliyemwabudu Allah Mtukufu kwa unyenyekevu unaostahili.

> Uislamu hotoa maono ya tofauti ya watu kwa njia ambayo hakuna utawala mwingine unaojua, na ambayo watu wa dunia hawajaahidi.



**Muhammad ni Mtume wa Uislamu**

«Enyi watu ,jueni ya kuwa Mola wenu ni mmoja,na baba yenu ni mmoja,jueni ya kuwa hakuna ubora wa Mwarabu kwa asiekuwa Mwarabu,wala kwa asie kuwa Mwarabu kwa Mwarabu,wala (ubora) wa mtu mwekundu kwa mtu mweusi,wala Mtu mweusi kwa mtu mwekundu ila kwa Ucha Mungu»



**Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu**

Ambayo inatambua usawa wa watu katika uhuru, haki na heshima

630m — 1948

Bali Qur'ani inatuzindua kuwa kutofautiana rangi za watu, maumbile, lugha zao na tamaduni zao ni miongoni mwa neema za Allah Mtukufu na ishara Zake na maajabu ya viumbe Wake katika ulimwengu huu. Na Akalifanya jambo hili kuwa ni kipimo cha utukufu Wake na umuhimu Wake katika Kuumba mbingi na ardhi, na kuwa hazinduki kwa hilo na kuzingatia ila yule mwenye elimu, anayetafakari. *"Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi." (Q30:22)*

Wakati kifungu cha kwanza Katika Azimio la Umoja wa Haki za Binadamu ni suala la usawa katika uhuru wa watu, haki na heshima, ilijulikana rasmi mwaka 1948, na kuanza kutekelezwa baada ya hapo jambo hilo si jipya kwa kuwa tayari Mjumbe wa Allah Mtukufu Muhammad –*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa amekwishatangaza haki hizo kutoka zaidi ya miaka 1400 huko nyuma, na kuwapa watu mtazamo mpya pale aliposema akiwahutubia watu; *"Enyi watu hakika Mola wenu nyinyi ni Mmoja na hakika baba yenu nyinyi pia ni mmoja, tambueni kwamba hakuna ubora kwa mwarabu juu ya asiyekuwa mwarabu, wala asiyekuwa mwarabu juu ya mwarabu, wala mwekundu juu ya mweusi, wala mweusi juu ya mwekundu ila kwa uchaji Mungu wake."* (Imepokewa na Imamu Ahmad 23489)



## KUSHUGHULIKIA MAZINGIRA NI KATIKA SEHEMU YA IMANI

Baadhi ya falsafa zinazotawala zinamchukulia mwanadamu kuwa ndiye bwana katika ulimwengu huu, anaweza kufanya atakavyo kwa faida ya maslahi yake, bila ya kuwepo wa kumuuliza au kumchunga. Hata kama kufanya kwake hivyo kutapelekea kuharibika kwa sehemu ya ulimwengu au kuangamia kwa aina fulani ya viumbe. Na kinyume cha hilo baadhi ya falsafa zinamchukulia mwanadamu kuwa kama kitu kingine, hakuwa ila ni aina tu kama zilivyo aina nyingine za mamilioni ya viumbe hai. Hivi Uislamu unatazama vipi mafungamano ya mwanadamu na ulimwengu?

Uislamu unayatazama mafungamano ya mwanadamu na ulimwengu katika taswira ya kiimani kwamba vitu vyote ni vyenye uhusiano unaotegemeana na kumalizia kwa hukumu za upambanuzi kwa ajili ya kudhibiti na kuweka sawa huo uhusiano kati ya mwanadamu, wanyama, ardhi na viumbe vingine vilivyopo.


Na Kitu cha kwanza kinachogusa jicho la mtafiti katika falsafa ya Kiislamu juu ya mafungamano hayo ni ule ulinganifu ambao Qur'ani imeuthibitisha. Allah Mtukufu Amemtukuza mwanadamu na Akampambanua na viumbe wengine waliobaki:

*"Na hakika Tumewatukuza wanaadamu, na Tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na Tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa Tulio waumba."* (Q17:70)

Na kisha Yeye Akamdhalilishia ulimwengu na viumbe vyote vilivyomo ili Apate kunufaika kwavyo na kuwatunza:

*"Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwa hayo Akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na Akafanya yakutumikieni majahazi yanayopita baharini kwa amri Yake, na Akaifanya mito ikutumikieni. Na Akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na Akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu."* (Q14:32-33)

Mwanadamu sio kama aina tu ya kiumbe kati ya mamilioni ya viumbe wengine, asiye na faida kuliko wengine, bali ni kiumbe mtukufu, mwenye heshima, aliyedhalilishiwa mazingira asili ili yamtumikie na kufaidika nao:



"Yeye Ndiye Aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi. Tena Akazielekea mbingu, na Akazifanya mbingu saba. Naye Ndiye Mjuzi wa kila kitu." (Q2:29)

Lakini kwa upande wa pili Qur'ani inatusisitizia kuwa yeye si bwana moja kwa moja katika ulimwengu huu, ambaye anaweza kufanya atakavyo na kwamba hadhi aliyopewa na utofauti huo juu ya viumbe wengine haumpi yeye haki ya kufanya uharibifu katika ulimwengu, na kufuja mali asili zilizopo, kwa kuwa Mmiliki hasa ni Allah Mtukufu Aliye Muumba wa vyote. Kazi ya mwanadamu na hadhi yake inaishia kwenye ukweli kwamba Allah Mtukufu Amempa mamlaka katika ulimwengu, kwa maana ya kufanywa muangalizi, mwenye haki ya kunufaika na kufaidika, akamwamrisha ajishughulishe, yaani afanye kazi kwa ajili ya kuviendeleza na kuvikuza, bila ya kuleta madhara au uharibifu kwa watu, mazingira au viumbe hai wengine:

*"Na kina Thamud Tuliwapelekea ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Yeye Ndiye Aliye kuumbeni katika ardhi, na Akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu Kwake. Hakika Mola Wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi."* (Q11:61)

*"Na pale Mola Wako Mlezi Alipo waambia Malaika: Mimi Nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa Sifa Zako na tunakutaja kwa utakatifu Wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua."* (Q2:30)

Na Sharia ya Kiislamu imelithibitisha na kuliwekea mkazo jambo hilo. Zipo kanuni na maelekezo kadhaa yenye upambanuzi uliyo bayana, kwa ajili ya kuweka sawa huo uhusiano madhubuti uliyopo, kati ya mwanaadamu na viumbe wanao mzunguka, na mfano katika hayo ni kama ifuatavyo:




## 1.Kuwahurumia wa wanyama

Yamekuja maelekezo mengi kutoka kwa Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* ambayo yanahimiza kuzingatia haki za wanyama, na ahadi ya kupata malipo makubwa akhera kwa kuwafanyia wema, na kukataza kuwatesa na kuwafanyia vibaya, na ametoa onyo la adhabu kali ya Allah Mtukufu kwa kwenda kinyume na maagizo hayo.

Wakati ambapo jumuia ya kwanza ya kujishughulisha na haki za wanyama ilianzishwa Uingereza mnamo mwaka 1824 kwa jina la Jumuia ya Mfalme ya Haki za Wanyama, Sheria ya kwanza kujulikana katika Zama za kisasa inampa uhalifu kwa wenye kuwatesa na kuwafanyia vibaya wanyama, ilithibitishwa mwaka 1949, hali ya kuwa tayari Uislamu kabla ya karne ya kumi na nne ulikwishaharamisha kuwatesa na kuwafanyia vibaya wanyama na kulichukua kama kosa kubwa, na imekuja mifano mingi katika maandiko mengi kutoka kwa Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* kama vile kuharamisha kuwaweka na njaa au kwa kuwadhibu wanyama, kwa kuwaweka alama za moto, au, kuwabebesha mizigo zaidi ya uwezo wao, kuwachezea kwa namna inayohatarisha uhai wao, kumpiga usoni, na mengine yasiyokuwa hayo katika hukumu mashuhuri katika Vitabu vya fiqhi ya Kiislamu.

Huenda msomaji akafahamu ni kwa kiwango gani Uislamu umezingatia suala la kuwahurumia na kuwafanyia wema wanyama pale atakapoitazama kauli ya Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* alipokuwa akiwasimulia watu kisa cha yule mwanamke aliyekuwa akifanya kazi ya ukahaba, kazi ambayo ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa; yeye alimuona mbwa anaekaribia kufa kwa kiu, akamuhurumia kwa hali yake, akavua kiatu chake, akakijaza maji kutoka katika kisima, kisha akamnywesha mbwa yule. Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* anasema; *"Allah Mtukufu Akamsamehe yeye dhambi zake kwa sababu ya tendo hilo."* (Imepokewa na Imamu Bukhari)



## 2. Kutunza mimea

**Uislamu umehimiza kutunza mimea na kilimo , sawa jambo hilo liwe ni kwa maslahi yake mwenyewe , au maslahi ya w engine katika wanaadamu na viumbe wengine katika huu ulimwengu.**

Na katika hayo ni pamoja na lile analotufahamisha Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* kwamba, *"Hapana yoyote anayepanda au anayeshiriki kuotesha kinachowafaa viumbe, ndege akala kutokana na mmea huo ndege au mtu au mnyama, isipokuwa huwa kwake ni sadaka."* (Imamu Bukhari /2320).

Bali Mtume Mkarimu anamhimiza Muislamu aliye katika mazingira magumu kwamba asiache kufanya juhudi ya kulinda mazingira na kuiendeleza ardhi na kuistawisha kwa kilimo hata kama ana hakika kwamba yeye hatofaidika nayo, pale aliposema, *"Wakati wa kutukia Kiyama (tukio lililo kubwa kuliko yote katika ulimwengu) kama mkononi mwa mmoja wenu patakuwa na mche, anatakiwa aharakishe kuupanda kama ataweza ili iwe ni sadaka kwake."* (Imamu Ahmad/12981)

Akalifanya jambo la kuistawisha ardhi na kuiendeleza kuwa la kuazimiwa na ni ibada katika mazingira magumu yasiyompa mtu nafasi ya kuachana nayo kwa vyovyote.

## 3. Kutunza Rasilimali za asili


**Uislamu umetilia mkazo suala la uhifadhi mazingira na kutoharibu vyanzo vya Asili, au kuyachafua na kuyaharibu, ukaweka jedwali lililo kamilika kwa watu ambalo limesimama katika msingi wa (kinga ni bora kuliko tiba) na katika hilo ni kuhakikisha usafi wa mtu na kushughulikia upambanuzi wake, na kuhifadhi vyanzo halisi na uchumi katika kuyatumia (mazingira) na kulifanya kuwa ni kosa kuyaharibu au kuyachafua, na mfano wa hayo ni kama ifuatavyo:**

- **Uislamu** umeharamisha ufujaji katika kutumia vyanzo asilia na cha kwanza katika hivyo ni maji hata kama ni kwa lengo la maandalizi ya kufanya ibada kwa kupata udhu (nako ni kuosha viungo maalumu kabla ya Swala).
- **Kuwazuia** watu wenye nguvu na maamuzi kuhodhi vyanzo asilia kwa namna inayopelekea madhara kwa wengine, ukaharamisha kuzuia maji, (uwe kama mfano kwa vyanzo asilia) na moto (kama mfano wa nguvu (za uzalishaji) na majani (kama mfano wa chakula) (Imamu Abuu Daud 3477)

> Kutunza mazingira na kuchangia utakaso wake kutokana na uchafuzi ni sehemu ya imani kama Mtume wa Uislam.

- **Uislamu** umekataza kila chenye kuharibu mazingira yanayotuzunguka na mfano wa hilo ni makatazo ya kukojoa kwenye maji yaliyotuwama, kujisaidia kwenye maeneo ya kivuli na njia, kwa kuzingatia kuwa ni maeneo wanayopita watu na kuyaelekea wapita njia kwa ajili ya kupumzika kutokana na uchovu wa safari.

Na hayakuwa mifano hii michache ni yenye kushangaza kwa sababu imetokamana na Dini ambayo Mtume wake mtukufu anazingatia kwamba kusafisha mazingira na kuondosha uchafu njiani ni katika matendo mema tu, bali ni sehemu muhimu katika ukweli wa Imani ya mtu - (Imamu Muslimu 35).



## DINI YA ELIMU

Halikuwa ni  jambo la bahati mbaya kwamba neno la kwanza kuteremshwa kwa Mtume wetu Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama,* katika Qur'ani lilikuwa "Soma" msisitizo huo umekuja ndani ya Qur'ani na kupitia maneno ya Mtume - Swallallaahu alayhi wasallama, ili kulipa kipaumbele suala la elimu katika fani zake zote zenye manufaa kwa watu, hata njia anayopita mtu Muislamu katika kuitafuta elimu na maarifa kuwa ni njia yake ya kwenda Peponi. Kama alivyosema Mtume - Swallallaahu alayhi wasallama; *"Yeyote atakayepita njia akitafuta elimu ndani yake, Allah Mtukufu Atamfanyia wepesi njia ya kwenda Peponi."* (Imamu Muslim/2699)

Katika kulinganisha ubora wa elimu na vitu vingine Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* kwa kauli yake anasema; *"Hakika ubora wa mwenye elimu kwa yule mwenye kufanya ibada tu ni kama vile ubora wa Mtume kwa kumlinganisha na mtu wa chini kabisa."* (Imamu Tirmidhy/2685)

Kwa hiyo Uislamu Uislamu haujakuwa  vita  dhidi ya elimu kama ilivyo katika dini zingine, wala haujapata kuwahukumu wanataaluma kwa kutangaza matokeo halisi ya tafiti zao kama ilivyokuwa katika zama za kiza. Lakini ni kinyume kabisa na hivyo, bali Dini ya Uislamu ilikuwa ndiyo nuru ya elimu na ndio yenye kuipa nguvu na kuhimiza watu kusoma na kufundisha, na ilikuwa misikiti enzi za Makhalifa waliyo waongofu ndiyo minara ya kuendeleza elimu mbali mbali na maarifa, muda wa kuwa kuna kheri kwa watu.

Wala hatushangai kuona kwamba kundi kubwa la wanasayansi wa Kiislamu katika fani mbali mbali walianza masomo yao kwa kujifunza Qur'ani na kuihifadhi na kujifunza Dini, kisha ndiyo wakafanya vizuri katika maeneo yao mahususi ya kitaaluma.

Allah Mtukufu Ametukuza cheo cha mjuzi mwenye kuwafundisha watu kheri, na Akamtunuku daraja la juu. Hata Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* akasema kwamba, *"Viumbe wote wanamuombea rehema mtu mwenye kuwafundisha watu kheri."* (Imamu Tirmidhiy/2685)



"Wanachuoni wengi wa Kiislamu katika fani mbali walianza Maisha yao kwa kujifunza Qur'ani ambao ile wapeleka katika kubobea katika Elim nyinginezo

## BAADHI YA WANAZUONI WANASAYANSI WA KIISLAMU



1. **Khawaarizmiy** (790-850 Baghdad), Mwanasayansi huyu alikuwa mtaalamu wa hesabu, uhandisi na elimu ya anga, na ndiye muasisi wa hesabu za Aljebra, jina linalotokana na jina lake al-Jabir, ambaye vitabu vyake vilitafsiriwa katika karne za mwanzo kwa ajili ya watu wa mataifa mengine, yaani wazungu wa Ulaya; na kwa njia hiyo maneno ya Kiarabu kama, Algebra, sifuri, yakaingia katika lugha za kilatini kwa sababu yake.





2. **Ibnul Haytham** (965-1040 al-Qahira), Mwanasayansi huyu alikuwa mtaalamu wa fizikia na uhandisi, aliyekuwa na mafungamano na chuo cha al-Azhar, huko Misri, ametoa mchango mkubwa katika elimu ya viona mbali, yaani darubini; na yeye hunasibishwa na misingi ya uvumbuzi wa kamera, na watafiti wengi wanathibitisha kuwa neno kamera ambalo limeenea katika lugha nyingi ni neno la Kiarabu linalotokana na neno Qamar (yaani mwezi). Nalo ni jina la chumba cha mwanga alichogundua Ibnul Haytham.



3. **Al-biiruuniy** (973-1048 Khawarizm), Mwanasayansi huyu alikuwa mtaalamu mkubwa wa mambo ya anga za juu, yeye ndiye wa kwanza kutangaza kuwa ardhi inazunguka katika mzingo wake na akaashiria katika nadharia tete ya nguvu za mvutano.

4. **Azzahraawiyyu** (936-1013 Andalus), Mwanasayansi huyu alikuwa tabibu mpasuaji. Alikuwa Mwanasayansi Muislamu ambaye upasuaji umeendelea hivi leo kupitia mikono yake. Yeye ndiye aliyegundua na kuvipa majina vifaa vingi vya upasuaji kwenye vitabu vyake, na vitabu vyake ndiyo vikawa vyanzo vikubwa vya rejea katika fani ya utabibu na upasuaji kwa karne nyingi na vilitafsiriwa katika lugha mbalimbali.



5. **Ibnu Sina** (980-1037 Bukhaara - Uzbekistan), Mwanasayansi huyu alijulikana na wazungu wanasayansi wa Ulaya kwa jina la Avicenna. Yeye alikuwa tabibu aliyebobea na mwanafalsafa mashuhuri ambaye hapakuwa na mfano wake katika zama zake. Ameacha athari na vielelezo vingi vya kitabibu. Aliandika majedwali ya magonjwa na tiba zake na jambo hilo limenyanyua hadhi ya majaribio ya kielimu katika tafiti alizofanya na kudurusu kwake mambo ya tiba ambako kulimfikisha katika matokeo mazuri yaliyoshinda katika zama zake, na kubakisha kumbukumbu hadi hivi leo. Hilo linadhihiri wazi katika Kitabu chake alichokiita (Al-Qaanun) ambacho hadi leo ndiyo rejea kubwa katika mafunzo ya utabibu. Kwa karne saba baada ya kukiandika kiliendelea kufundishwa katika Vyuo Vikuu vya Ulaya mpaka katikati ya karne ya kumi na saba.



Na baada ya kuwa mtu mashuhuri kwa sababu ya taaluma yake alikuwa akiwatibu watu bure katika kutukuza utu wa binadamu na kutoa shukurani kwa Allah Mtukufu kwa neema ya elimu na maarifa Aliyompa.

6. **Ibnu Annafiis** (1212-1288 Damaskas), Mwanasayansi huyu ni katika wanazuoni wa Sharia na fiqhi, na wakati huo huo ni mmoja miongoni mwa wanataaluma wakubwa wa tiba na elimu ya kazi za viungo. Katika historia yeye ndiye mwanasayansi wa kwanza kugundua mzunguko mdogo wa damu na kuuelezea vizuri, na kuweka idadi kubwa ya nadharia tete za kitabibu ambazo nyingi bado zinafanyiwa kazi hadi hivi leo.



## UISLAMU UNAHUSISHA MAMBO YOTE YA MWANADAMU

Watu wengi hustaajabu pale wanapotambua kwamba Uislamu si Dini ya Ibada tu, matendo na maelekezo ya kitabia kwa ujumla Kama ilivyo katika dini nyingi walizoahidi, lakini ni zaidi ya hayo, tofauti kabisa na namna zilivyo dini nyingi zilizoenea duniyani.

Kwa hakika Uislamu si Dini iliyolenga kukidhi mahitaji ya kiroho pekee, kwa waislamu kujazana misikitini kwa dua na Swala, bali ni mfumo kamili wa maisha ya kijamii katika nyanja zake zote.

Na wala si rai, itikadi na falsafa tu wanazoamini wafuasi wake tu.

Kama ilivyo  Siyo tu mfumo wa kiuchumi au wa kimazingira uliokamilika.

Na si kanuni na nadharia za kujenga mfumo (nidhamu) na jamii tu.

Na haikuwa vilevile ni rundo la tabia na nyenendo katika kamiliana na wengine.



Bali ni njia iliyotimia katika kuendeleza nyanja zote za maisha kwa mapana na undani wake, inakusanya yote hayo na mengine.Pamoja na hayo haufungi uhuru wa watu bali inajaribu kuwafanyia  wepesi maisha yao ili juhudi zithibiti katika kuboresha, kujenga na kuleta maendeleo ya kijamii, nayo ni moja kati ya neema kubwa ambazo Allah Mtukufu Amewaneemesha waja Wake kama Qur'ani inavyotilia mkazo jambo hilo:

*"Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliye chinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliye kufa kwa kunyongeka koo, na aliye kufa kwa kupigwa, na aliye kufa kwa kuanguka, na aliye kufa kwa kupigwa pembe, aliye liwa na mnyama, ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama aliye chinjiwa masanamu. Na ni haramu kupiga ramli. Hayo yote ni upotovu. Leo walio kufuru wamekata tamaa na Dini yenu; basi msiwaogope, bali Niogopeni Mimi. Leo Nimekukamiliishieni Dini yenu, na Nimekutimizieni Neema yangu, na Nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo Dini. Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu."* (Q5:3)

Na pale kwa kejeli mtu asiyekuwa muislamu alipomwambia mmoja wa maswahaba wa Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama aliyekuwa* anaitwa Salmanu Alfaarisiyyu; *'Hakika huyu swahibu yenu (Mtume) anakufundisheni nyinyi kila kitu hata adabu za kukojoa na kujisaidia haja kubwa?' Yule swahaba mtukufu akamjibu; 'Ndiyo!' Ametufundisha na kisha akamtajia hukumu za Kiislamu na adabu zake katika jambo hilo."* (Imamu Muslimu 262).

Uislamu ni mfumo kamili katika Nyanja zote za Maisha kwa mapana na undani wake.

## DUNIA NA AKHERA

Wamisri wa kale walikuwa wakikausha maiti (mumiani) kisha wanamuwekea mali zake zote za thamani na kumzika navyo wakidhania kwamba atazihitaji katika maisha yake mengine huko anakokwenda baada ya kufa.

Na kwa upande mwengine kulikuwa pia watu wa tabt waliokuwa wakikatakata viwiliwili vya maiti zao na kuviweka katika maeneo ya miinuko ili kuwa chakula cha ndege na wanyama. Na wahindu nao wao mpaka leo huchoma miili ya maiti wao kwa kuwa kwa mujibu wa itikadi zao, ndiyo njia pekee ya kutakasa roho zao.

Hii ni mifano michache ya aina mbalimbali ya mila za kumsafia maiti na kumuaga zilizo tofauti, na ni taratibu katika zama na sehemu mbali mbali kwa kutegemea dini na itikadi za watu husika baada ya kifo, na ni kielelezo cha idadi ya maswali ya kina yanayohitaji majibu, je kuna maisha mengine baada ya kifo na je maisha hayo yakoje na huko tunahitaji nini?

Na hilo ni kwa sababu kifo ndio jambo la hakika ambalo sisi sote tunakubaliana kwamba kinatusubiri. Sote bila ya kumvua yoyote, iwe tunaamini kuwa kuna Maisha ya Akhera au hatuamini kuwa kuna hesabu za matendo yetu, kwamba baada ya kufa maisha yanakuwa yamekwisha katika yale tuliyokuwa tunaona na kugusa kwa viungo vyetu vya hisia, na ni sawa tu iwe tulijiandaa na muda huo wa kufikiwa au tulijaribu kujisahaulisha na kughafilika nao kwa sababu ya vyenye kupumbaza na kushughulisha na Maisha.

Hapo hubaki swali linalopingana na kila aina ya kughafilika na kujisahaulisha, linalolazimisha majibu, mara kwa mara, kutoka kwa kila mtu anapotafakari mwenyewe. Je kufa ndiyo mwisho wa uhai na kwamba hakuna tena kitu baada yake?. Je uwepo wetu duniyani ni aina tu ya mchezo?

Ni swali ambalo hukariri kwa kwenye akili zetu kila mara na Qur'ani vile vile inakariri kwa njia tofauti, na wakati huo huo kufahamisha juu ya majuto na hasara kubwa ambayo baadhi ya watu wataipata siku hiyo ya Kiyama. Kwa sababu hawakuziandaa nafsi zao kwa ajili ya kulijibu hilo swali na wala hawakujitayarisha kwa ajili ya siku hiyo, wakati huo baadhi yao watasema:

*"Atasema: Laiti ningeli jitangulizia kwa uhai wangu!" (Q89:24) na mwingine atasema; "Laiti ningeli kuwa udongo!"* (Q78:40)



Inajulikana kwamba watu wote wenye dini zilizoteremshwa kutoka mbinguni wanaamini maisha ya akhera na malipo mema na adhabu ndani yake! Kwa sababu hayo ndiyo dhumuni la yale waliyokuja nayo Mitume wote. Na kwa kuwa akili inashuhudia kwamba uhai hauna maana, wala dini, wala tabia, bila ya maisha mengine ambayo yatawahisabu watu, na kila mtu atapata ndani yake malipo yanayotokana na kheri zake au shari zake.

Pamoja na hayo watu wengi wanadhania kuwa dini na maisha haviwezi kukusanyika pamoja au starehe na kujiendeleza , ima ufanye kwa ajili ya Dunia au ufanye kwa ajili ya Akhera na waona haiwezekani kukusanyika wakati mmoja kama vile haezekani kukutana usiku na mchana wakati mmoja ima iwe ni usiku au mchana ..

Na hakuishi kustajabu kwao, bali inakuwa vigumu kwa baadhi yao kusadiki jambo hilo la kukusanya baina ya Ibada a na kustarehe au baina ya ibada na kuchuma Mali na wadhani kuwa hilo hakuna katika itikadi ya Muislamu na Mtume Mtukufu Muhammad (Rehma na amani zifikie yeye) anatujulisha ya kuwa Mwanadamu anapotenda amali yoyote ile na akakusudia kufanya kheri basi atalipwa kwa kitendo kile siku ya Akhera hata kama ni kuondosha mwiba katika barabara wanaopita watu, au hata kama ni tonge unamlisha mkeo (Bukhari 56)

Na alipo tuelezea Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* kuwa milango ya kheri ni mingi isiyokwisha na akapiga mfano ambao uliwashangaza maswahaba zake, pale aliposema; "Pale mmoja wenu anapokidhi matamanio yake kwa mkewe, yeye huandikiwa thawabu," maswahaba zake wakauliza; "Kuna uhusiano gani kati ya malipo na mtu kukidhi matamanio yake?" Mtume akasema; *"Mnaonaje kama angekidhi matamanio yake kwa njia ya haramu je asingechuma dhambi?" Wao wakajibu; 'Atachuma!' Yeye akasema, "Kwa sababu hiyo yeye huandikiwa thawabu kwa sababu ya kufuata njia iliyo sahihi."* (Imamu Muslimu 1006)

Kwa hivyo ataona yule mwenye kutaka kuutambua Uislamu katika uhalisi wake ukweli wa uwiano kati ya maisha ya dunia na akhera kama inavyo tupa taswira Qur'ani. Wakati Uislamu unawahimiza watu kufanya ibada maalumu kwa ajili ya kuitafuta akhera na unatilia mkazo kujitahidi katika Dunia kwa ajili ya kutafuta radhi ya Allah Mtukufu. *"Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua. Na itakapo kwisha Swala, tawanyikeni katika nchi mtafute Fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa."* (Q62:9-10)

Katika kutafuta riziki halali kwa ajili ya familia yake mtu hupata thawabu muda wa kuwa amekusudia kupata radhi ya Allah Mtukufu kwa kitendo hicho. Na Muislamu ameamrishwa kumuabudu Allah Mtukufu kwa kujitahidi katika wadhifa wake na kazi yake kwa ajili ya kutafuta riziki na kuwalea watoto wake na kushughulikia na afya yake na mazingira yake na kuiendeleza jamii yake kama anavyomuabudu Allah Mtukufu kwa Swala zake na Sadaka zake na Funga zake.

Na hiyo ndio moja ya siri za utulivu wa nafsi na amani ya ndani ambayo Muislamu huipata pale anapoona mafungamano baina ya Maisha yake ya Dunia na Maisha akhera, na kupata ladha ya ibada yake na kustarehe kwake hakuna mgongano, bali ni jingo kamili lenye kutiliana nguvu baina yake

Na hapa Qur'ani inatuwekea wazi nembo ya Muislamu ambayo imekusanya falsafa ya Kiislamu na ikimwamrisha aitanaze wazi: kuwa Maisha yangu yote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wala sio Swala na ibada peke bali vitendo vyangu vyote na tarajia malipo kwa Mwenyezi

Mungu na yeye atanihukumia amali zangu na atanilipa baada ya kufa kwangu na kufanya hivyo huwa nimejilazimisha na amri zake Mwenyezi Mungu na kushikamana na Dini yake ya Uislamu

*"Sema: Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote."* (Q6:162)

## DINI YA MAWASILIANO NA USHIRIKIANO

Hadi hivi leo inazingatiwa kwamba wasifu wa safari ya mwanahistoria Muislamu Ahmad Ibnu Fadhlaan, aliyetembelea Russia, Denmark na mataifa ya Scandnavia, ni wasifu wa kwanza madhubuti na wa kiuchambuzi juu ya maisha ya watu na tabia za kijamii ambao ulimwengu uliutambua kuhusu tamaduni za watu wa miji hiyo.

Na hilo ni kwa sababu mwaka 921 Ahmad Ibnu Fadhlaan alifanya safari ndefu ya Ajabu ambayo inazingatiwa kuwa ni miongoni mwa safari muhimu za mawasiliano ya kimaendeleo iliyopata kufanyika katika karne za kati. Aliondokea Baghdad uliokuwa mji mkuu wa elimu na ustaarabu wakati huo, na akapitia idadi kubwa ya miji na mataifa na akathibitisha ushuhuda wake na matukio aliyoishi nayo katika zama zake kwenye kitabu kilichojaa taarifa nyingi muhimu kuhusu maisha ya kijamii ya watu wa mataifa mbali mbali alimopita na kilisambazwa kwa mara ya kwanza mwaka 1923 kutokana na chapa iliyoandikwa kwa mkono iliyopatikana huko Russia.

Na sababu ya umuhimu wa kitabu cha Ibnu Fadhlaan imeelezwa vizuri na mtaalamu wa Kimarekani Michael crichton ni kwamba pamoja na waislamu katika mji wa Baghdad kushikamana sana na Dini yao, bado walikuwa wazi kwa mataifa yaliyotofautiana nao katika mitazamo, maarifa na tamaduni na hata itikadi. Na kwa maana hiyo walikuwa wanaopenda kujifunza tamaduni mpya na maarifa kutoka popote pale vilipopatikana. Na wakati huo kulikuwa na mataifa machache tu katika maeneo mbali mbali, na hilo liliwawezesha wao kukusanya ushahidi wa maendeleo na taaluma katika nchi za mbali na tamaduni za watu wengine.

Uislamu ulikwishatoa wito wa kushirikiana na watu katika kuendeleza ustaarabu, kutengeneza na kuchanganyika nao na kuwasiliana nao kwa kiwango cha juu kwa tabia na maadili mazuri pamoja na kuwepo kwa tofauti za tamaduni na dini; na unatuzindua kwamba kujitenga na kuwa mbali na watu si njia ya Uislamu uliyo sahihi. Na kwa sababu hiyo Mjumbe wa Allah Mtukufu - *Swallallaahu alayhi wasallama* amesema, *"Mtu anayechanganyika na watu na akawavumilia yale yanayomsibu kutoka kwao, maudhi na makosa yao, ni m-bora kuliko yule anayetengana nao na kuwa mbali nao."* (Ibnu Maja 4032)

# MUUMBAJI MMOJA
# MWABUDIWA MMOJA



## Uislamu

Uislamu unathipitisha kuwa Imani imani ya kinadharia haitoshi kuingia katika Imani ikiwa Mola muumba ni mmoja,basi ni lazima awe Mola anaefaa kuabudiwa kwa haki awe ni mmoja.

## Katika lugha ya Kiarabu Jina Allah lina maana tatu kwa pamoja

- Inamanisha Muabudiwa kwa haki Ambaye watu humtakasia yeye ibada zao zote, Swala na Funga zao, na mwelekeo wa nyoyo zao.
- Mtukufu katika Dhati Yake na Sifa Zake na Cheo Chake kwa hali ambayo akili hazina uwezo wa kudhibiti.
- Ni Yule Ambaye nyoyo zimefungamana Naye, na zinapata utulivu kwa Kumtaja na kupata ladha kwa ukaribu Wake na kwa kumuabudu.

Qur'ani imeweka mkazo kwamba ni lazima kwa kila mmoja kuweka sawa mtazamo wake kuhusu Allah Mtukufu kwa kumtakasia ibada na kumuweka mbali na upotoshaji na uzushi unaoshusha Hadhi na Utukufu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Allah Mtukufu, kama inavyoweka wazi Qur'ani, Ndiye Muumba na Mwanzilishi wa ulimwengu huu na mfumo wake, na yote yanayotokea ndani yake yanatokea kwa Kutaka Kwake, Makadirio Yake na Elimu Yake, hakibebi mimba chenye kubeba katika aina zote za viumbe, wala havizai isipokuwa kwa Elimu Yake na Kutaka Kwake, wala halidondoki tone la mvua wala hayatokei mabadiliko yoyote ya usiku au mchana, yaliyo wazi na yale ya siri, ulimwenguni, isipokuwa Allah Mtukufu Amekizunguuka kwa Elimu, Uwezo na Rehma Zake.

Na ni Mwenye Sifa zilizo nzuri, zilizo kamilifu, Yeye Ndiye Mwenye Nguvu Ambaye Hashindwi, Aliye Mpole Ambaye Huruma Zake zimekienea kila kitu, na Mtukufu Asiyemithilika, Asiye na upungufu kwa namna yoyote ile.

Na wakati makafiri walipodai kwamba Allah Mtukufu Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akapumzika siku ya saba, Qur'ani ikaja kukanusha madai hayo na kuweka wazi:

*"Na bila ya shaka Sisi Tumeziumba mbingu na ardhi na vilio baina yao mnamo siku sita; na wala hayakutugusa machofu."* (Q50:38)



Quran inasisitiza kwamba kila kitu kinachotokea hutokea kwa ujuzi na uwezo wa Mungu, hata matone ya mvua na majani ya mti yanapo annguka huwa ni kwa ujuzi wake.

Na kwamba madai hayo na mfano wake hayawezi kuzuka katika akili isipokuwa kwa kumfananisha Allah Mtukufu na viumbe ambavyo akili inavijua. Lakini Yeye Ndiye Muumba na vilivyobaki ni viumbe tu, ni vipi viumbe watafanana na Muumba wao. *"Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona."* (Q42:11)

Na Yeye kwa Utakasifu Wake Ndiye Hakimu Muadilifu Asiyedhulumu hata chenye uzito wa mdudu chungu. Na tunayoyaona katika maisha kutoka Kwake yanatudhihirishia sisi hekima Yake na upole Wake. Kama ilivyo kwa mtoto mdogo asiyeweza kufahamu baadhi ya matendo ya mzazi wake, kwa kule kutoweza kwake kufahamu au kutafsiri maana zake kwa sababu ya ufinyu wa fikra zake uliyopo kati yao, na vivyo hivyo akili ya binadamu haina uwezo wa kutambua kitu katika hekima ya Allah Mtukufu kwa baadhi ya viumbe Wake na matakwa Yake.

Wala Uislamu hautosheki kwa itikadi za kinadharia zisizotosha kumuingiza mtu katika Imani, kama Mola Muumbaji ni mmoja inatakikana pia Mola Mwenye kuabudiwa Awe mmoja na wala haifai kufanya chochote katika ibada au Dua kumfanyia asie kuwa Allah Mtukufu, bali ibada zote ni kumtakasia yeye bila ya kumpachika mshirika au mwenye kushufaia. Allah Mtukufu ni Mkubwa kuliko na ametakasika na ushirika.

Ikiwa watawala wa kiduniya ambao hawawezi kutambua shida za watu wao wenye mahitaji na wanyonge halafu kuwasaidia ila kwa kupitia wasaidizi na watu wa karibu zao, wanaowajulisha wao kuhusu hali za raia zao. Basi Allah Mtukufu Anajua yaliyowazi na yaliyofichika na Yeye ni Mwenye Nguvu, Mfalme Mwenye uwezo na ulimwengu wote uko katika milki Yake, na chini ya maamuzi Yake na Anapotaka jambo Lake Huliambia tu kuwa na huwa papo hapo! Kwa nini basi kumwelekea mwingine?

Na Qur'ani inathibitisha kwamba utulivu wa moyo na ukunjufu wa kifua haukamiliki kama Muislamu hajamuelekea Mola wake, na kuziweka shida zake mbele Yake. Na Yeye Ndiye Muweza Mkubwa Asiyemithilika Mwenye Kuwapenda waja Wake, mpole kwao Aliye karibu nao Ambaye Hufurahia maombi ya waja Wake Kwake; Anawakirimu na Kuwalipa kwa kiasi cha kuelekea kwao na unyenyekevu wao Kwake:

*"Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu Akakufufueni! Kisha Atakufisheni, tena Atakufufueni, kisha Kwake mtarejeshwa?"* (Q2:28)

*"Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na Akaiondoa dhiki, na Akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia. Au nani yule anaye kuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya wanao washirikisha naye."* (Q27:62-63)

Na kwa sababu hiyo hoja iliyo bayana katika Uislamu ni wajibu wa kuzitakasa ibada kwa ajili ya Allah Mtukufu Peke Yake bila ya kumshirikisha na mwingine:

*"Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha."* (Q16:36)

Na huo ndiyo wito wa Mitume wote kama inavyotuarifu Qur'ani, hapana Mtume wala mfalme wala walii,

vyovyote utakavyofikia wema wake, asielekezewe chochote katika aina ya dua kwa hoja kuwa wao wanakaa kati ya Allah Mtukufu na waja Wake. Kwa sababu mwisho wa yote wote ni viumbe wa Allah Mtukufu na watumishi Kwake. Na Allah Mtukufu yupo karibu na waja Wake Anasikia maneno yao na Anajibu maombi yao pale watakapozitakasa ibada zao kwake.

Na kwa nini asipate ladha ya furaha na kuliwazika yule mwenye kutakasa mwelekeo wake kwa Allah Mtukufu. Hapana haja ya kuyumba wala kutikisika, vipi ayumbe yumbe ikiwa mfalme wa kweli ni Mmoja tu, na Muumba ni Mmoja tu na Mwabudiwa ni Mmoja tu na kwa kuelekea ni kumoja tu, na si kwingineko ila ni kwa Allah Mtukufu pasi na mwingine.

Na hii ndiyo maana ya Sura fupi miongoni mwa Sura kubwa kabisa na tukufu za Qur'ani, *Suuratul-Ikhlas*.

### Suratul Ikhlas

Katika sura hii Allah Mtukufu Anamuamrisha Mtume wake Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama atangaze kwa uwazi kabisa kana kwamba anayejibu swali lililouliza Yeye ni nani?

"*Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana Naye hata mmoja.* " (Q112:1-4)

- Hakika Allah ni Mmoja tu hana mshirika katika ibada.
- Yeye Ndiye ambaye wanamtegemea na wanamwelekea viumbe wote katika haja zao.
- Na Yeye Ametakasika kuwa na mtoto au kuzaliwa. Yeye Ndiye wa Mwanzo hakuna kitu kabla Yake.
- Na wala Hana mwenza anayefanana Naye katika Dhati Yake na Sifa Zake kwani yeye Ndiye Muumba na wasiokuwa Yeye ni viumbe.




## KATI YA KANUNI ZA KAWAIDA NA KANUNI ZA SHERIA

Allah Mtukufu Ameumba huu ulimwengu ambao tunaishi ndani yake akianza na seli ndogo tu katika miili yetu, na kilicho kidogo kuliko hicho na Kumalizia kwa maumbo ya mbali ambayo huonekana tu kwa vifaa vya kukuza vitu vikaweza kuonekana, kwa umakini mkubwa na ukamilifu na mpangilio wa kustaajabisha. Uhai hautawezekana wala mazingira asilia kuwa kama yalivyo, isipokuwa kwa amri Yake. Na wataalamu wa mazingira asilia wanakiri kwamba hitilafu kidogo tu katika mfumo huo inaweza kuleta maangamizi na uharibifu mkubwa.

Na Muislamu anaamini kuwa Yule Muumba Aliyeweka mfumo huo wa kustaajabisha katika umadhubuti wote na umakini Ndiye Anayejuwa lenye maslahi kwa viumbe Wake katika Sharia, hukumu na mfumo wa maisha. Na Dini Aliyoiweka ndio mfumo pekee wenye uwezo wa kustawisha maisha ya watu, na kuyaokoa ndani yake na ubaya wa upande mwingine. Na Allah Mtukufu Amekwisha sema ndani ya Qur'ani Akibainisha kuwa Aliyeumba ulimwengu na watu Ndiye Mwenye Kujua yale yanayowafaa. *"Asijue Aliye umba, Naye Ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?"* (Q67:14)





## HAKUNA UTAKATIFU KATIKA UISLAMU

Katika dini nyingi tunashuhudia baadhi ya watu kupewa kipaumbele kuliko wengine, na zikifungamanisha ibada za watu na imani zao kwa ridhaa na muafaka wao. Kwa mujibu wa mafunzo ya dini hizo wao ndio wakala kati yao na mungu wao! Na wao hutoa misamaha, na kudai kujuwa mambo yaliyofichika na kama ilivyo katika itikadi zao, wao wanadai kule kutofautiana nao ni hasara kubwa.

Ama katika Uislamu hakuna wadhifa ambao jina lake ni mtu wa dini. Uislamu umemtukuza mwanadamu na ukainua hadhi yake, na ukamkomboa kutokana na kutawalia katika masuala ya ibada na ya kiroho kwa ujumla wake, ambayo ndio kiunganishi kati yake mtu na Mola wake Allah Mtukufu. Uislamu umebatilisha kuwa kufanikiwa kwa watu, toba yao au ibada yao kufungamanishwa na matakwa ya watu maalumu namna watakavyo kuwa katika ubora na wema.


Kama vile ulivyowakomboa watu kuachana na fikra potofu ya kutawala watu kielimu kwa kudai kwamba kuijua dini ni jambo maalumu na kwa watu maalumu na si mwingine yeyote. Bali tunapata kwenye Qur'ani jambo la kuijuwa dini na kuifahamu ni jambo la watu wote na si hivyo tu bali limefanywa kuwa ni jambo la wajibu juu yao. Na inawaamrisha Waislamu wote kuisoma Qur'ani , na kuifahamu na kuzingatia maana yake na kuyafanyia kazi mafundisho yake. *"Na hiki Kitabu, Tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili."* (Q38:29)

Katika Uislamu ibada zote na imani ni kati ya mja na Mola wake, na hakuna mtu yoyote aliye bora katika hilo wala kuwa ndio njia ya kumuelekea Yeye. Allah Mtukufu Yu karibu na waja Wake na Anasikia maombi yao na kuwaitikia. Na Anaona pia ibada zao na swala zao na swaumu zao na sadaka zao na Yeye Atawalipa wao kwazo. Na hakuna kiumbe yoyote ana haki ya kutoa msamaha na kukubali toba. Wakati wowote mja anapotubia kwa usafi wa nia, ni Allah Mtukufu tu Ndiye Mtakabali toba, Mwenye Kusamehe dhambi. Allah Mtukufu Yu karibu na wote pale wanapomuelekea.

> Uislamu umemtukuza mwanaadamu na ukanyanyua cheo chake , basi ukamuweka huru kutokana na mamlaka yeyote ya kiroho ambao unakua kiunganishi baina yake na ALLAH basi ukabatilisha yakwamba furaha ya wanaadamu au kutubia kwao au ibada yao iwe inafungamana na watu maalum namna watakavyofikia katika ubora na kuwa wema.

*"Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka."* (Q2:186)

> Qur'ani tukufu inakariri kuwa Mwenyezi Mungu yuko karibu na waja wake pale watakapo muelekea yeye na kumuomba



**JE KUNA MIIKO MAALUMU YA KUINGIA KATIKA DINI YA UISLAMU**

Hakuna miiko tata katika kuingia ndani ya Uislamu kwa yule aliekinaika na akataka kusilimu. Wala si lazima jambo hilo liwe katika sehemu maalumu, au kwa kuhudhuria idadi ya watu maalumu, bali mtu anapolitaka hilo inatosha tu kwake kutamka shahada mbili kwa kujua maana yake na kuiyakinisha moyoni mwake. Na shahada mbili ni tamko;

*Ash-haadu An-lailaha illa Allah* (Ninashuhudia na kuitakidi kuwa hapana muabudiwa anayepasa kuabudiwa kwa haki ila Allah Mtukufu, name namuabudu Yeye Peke Yake, Naye hana mshirika.

*Wa-ash-haadu Anna Muhammadan Rasuulullah!* (Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mjumbe Wake kwa watu wote na ninaahidi kutii amri zake na kujiepusha na makatazo yake, na nitamuabudu Allah Mtukufu kwa mujibu wa Sharia Yake na mafundisho Yake.



# MITUME NI NANI KWA HAKIKA?



Allah

Allah Mtukufu Aliwaumba watu kwa ajili ya kumwabudu, halafu Akawapelekea Mitume ili wawafundishe wao Sharia Zake, na kuwakumbusha wao kuhusu Dini yao. Walifanya kazi ya kustawisha dini ya watu na maisha yao ya kijamii, ili wapate kuwa kigezo chema kwa watu wao, wakati wakipambana na upotofu na kuwaongoza watu kufuata njia sahihi iliyo ya haki, ili watu wakose hoja ya kutomuabudu Allah Mtukufu.

## UTU WA MITUME

Qur'ani kupitia Aya zake nyingi imeweka wazi kwamba Mitume na Manabii walikuwa watu ambao Allah Mtukufu Amewahusisha kwa Kuwapelekea ujumbe Wake kwa binadamu kupitia Malaika Jibrilu - *Alayhi salaam*, pamoja na kufanana nao wao wamepewa daraja la juu kwa utakasifu na unyoofu waliopewa, kwa hali ambayo Allah Mtukufu Aliwawezesha kubeba ujumbe Wake na Dini Yake kwenda kwa watu, kama ilivyoteremshwa katika Qur'ani;

*"Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola Wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola Wake Mlezi."* (Q18:110)

Mitume wote ni watu, wanazaliwa kama wanavyozaliwa watu wengine, na wanakufa kama wanavyokufa, na wanaugua kama wao, wala hawatofautiani nao katika umbo au mahitaji yao.

Hakuna chochote kwao cha kiungu, kwa sababu uungu ni wa Allah Mtukufu tu Peke Yake, lakini wao ni binadamu wanaofikishiwa amri ya Allah Mtukufu kupitia Malaika au kwa njia nyingine.

Na kwa hakika umati za mwanzo walistaajabia ufunuo. Na Allah Akapinga kustaajabia kwao huko na Akabainisha kuwa hakuna sababu za msingi kwa kustaajabu huko. Kwa sababu hiyo ndiyo njia ya kufikisha muongozo wa Allah na mafundisho ya Dini yake kwa viumbe wake. *"Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu, na wabashirie wale walio amini ya kuwa watakuwa na cheo cha juu kwa Mola wao Mlezi? Wakasema makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhaahiri!"* (10:2)

## UKATI NAKATI KATIKA UTUKUFU WA MITUME

Allah Mtukufu Aliwachagua waliyo bora katika viumbe ili kubeba ujumbe Wake. Wao ni watu waliyo katika daraja la juu la unyoofu na wema, na Qur'ani imewasifu Mitume wote kuwa ni waongofu, wafanya mema, watengenezaji na wateule waliyoimarishwa juu ya walimwengu;

*"Na Tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. Kila mmoja wao Tulimwongoa. Na Nuhu Tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake Tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo Tunavyo walipa wafanyao wema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema. Na Ismail, na Al Yasaa, na Yunus, na Lut'. Na wote Tuliwafadhilisha juu ya walimwengu wote."* (Q6:84-87)

> Qur'an inathibitisha kuwa mitume wote ni wanadamu ambao Mwenyezi Mungu kawatukuza kwa kuwapa ufunuo na utume.

Na pale Mtume yoyote anapoelekea kuingia kwenye makosa, Allah Mtukufu Humzindua katika hilo, ili apate kurejea na kujirekebisha kutokana na kusudio hilo. Na hilo linakuwa kosa kwa sababu ya kukosea katika jitihada na si kwa kuvuka mipaka kwa makusudi kwa yale anayoyataka Allah Mtukufu kutoka kwao.

Na hivi Qur'ani ndivyo inawataja Mitume kwa sifa zilizo madhubuti, hakuna kwao kuchupa mipaka wala kudhuru, wao wamehifadhiwa na

madhambi makubwa. Lakini pamoja na hayo wao ni binadamu na si miungu wala watoto wa miungu, wala hawana sifa za kiungu ili waabudiwe.


Na katika yanayoweka wazi jambo hilo ni yale Anayosimulia Allah Mtukufu katika mazungumzo yatakayofanyika siku ya Kiyama ili Allah Mtukufu Apate kudhihirisha kwa mazungumzo hayo kumtakasa Kwake Nabii Isa - Alayhi salaam na uzushi wa kuabudiwa na watu; *"Na pale Mwenyezi Mungu Atakapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Isa) atasema: Subhanaka, Wewe Umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka umekwisha yajua. Wewe Unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika Wewe Ndiye Mjuzi mkubwa wa yaliyo fichikana. Sikuwaambia lolote ila Uliyo niamrisha, nayo ni: Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola Wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipo kuwa nao. Na uliponifisha ukawa Wewe Ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu."* (Q5:116-117)

## MSIMAMO WA UISLAMU KUHUSU MITUME

Baadhi ya watu, wale wenye akili finyu, wanadhani kwamba hii Qur'ani ni simulizi za Mjumbe wa Allah Mtukufu Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* ambavyo ameibuni mwenyewe. Na wengine wanadai kwamba ni visa tu vya watu wa kale, hushangaa pale wanapofahamu kwamba Qur'ani imemtaja Nabii Isa - *Alayhi salaam* kwa kulitukuza jambo lake na kumtakasa yeye kutokana na tuhuma potofu mara 25. Na imelitaja jina la Nabii Musa - Alayhi salaam mara 136, na haikutaja jina la aliye Mtukufu wa daraja Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* aliyeteremshiwa Qur'ani ila mara 5 tu.

> Kila mwenye kuisoma Qur'ani anatambua kwamba baadhi ya Sura zake zimepewa majina ya Mitume, kama vile Nabii Ibrahim, Nabii Yusufu na Nabii Yunus, na Allah Mtukufu Ameiita moja ya Sura kwa jina la mama wa Nabii Isa - *Alayhi salaam*, Bibi Mariyamu.

Na wakati ambao watu wa dini zingine hawamkubali Mtume Muhammad - Swallallaahu alayhi wasallama isipokuwa baadhi ya mitume wengine na baadhi yao kuwafanyia kabisa uadui mitume wengine, ni jambo la changamoto kubwa kwa kila anayeisoma Qur'ani na kukuta msititizo mkubwa katika baadhi ya Aya zake kwamba mtu hawezi kuwa Muislamu mzuri mpaka kwanza awaamini pia Mitume walioletwa kabla ya Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama*. Na kama atamkanusha hata mmoja wao tu au kuwa na mashaka juu ya ukweli wa utume wake, au kumtuhumu kwa mambo yasiyofaaa, atakuwa ametoka katika Uislamu. Kwa kuwa Qur'ani inatia mkazo kuwa Mtume - Swallallaahu alayhi wasallama na waumini wanaamini yaliyokuja kutoka kwa Allah Mtukufu na kwa ajili hiyo wanamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Malaika Wake na Mitume Wake na hawabagui yeyote miongoni mwao; *"Mtume ameamini yaliyo teremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake na Mitume Wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume Wake, na (Waumini) husema: Tumesikia na tumet'ii. Tunakutaka maghfira Mola Mlezi wetu! Na marejeo ni Kwako."* (Q2:285



# MSIMAMO WA UISLAMU KUHUSU NABII ISA - *ALAYHI SALAAM*



# Inazingatiwa

Inazingatiwa kwamba Nabii Isa, mwana wa Mariyamu, ni miongoni mwa watu muhimu katika historia ya wanadamu, na ni miongoni mwa manabii walioufanyia watu kheri nyingi. Watu ni wenye mitazamo tofauti kumhusu yeye na mama yake! Wapo wale wanaoamini kuwa ni Mungu au mtoto wa mungu, na wapo wale waliomfanyia uadui na kumtuhumu tuhuma nyingi zilizo batili, sasa ni upi msimamo wa Uislamu kuhusu Nabii isa - *Alayhi salaam*?


Holy
Bible

## 1 Nabii Isa - *Alayhi salaam* ni miongoni mwa mitume waliyo watukufu

Qur'ani imekwishaeleza kuhusu Nabii Isa - *Alayhi salaam* kwamba ni miongoni mwa Mitume wakubwa na wenye hadhi kubwa mbele ya Allah Mtukufu, na kwamba mama yake bibi Mariyamu ni mwanamke mkweli, aliyemuabudu Mola wake kwa uyenyekevu mkubwa, mtakasifu aliyejizuwiya na machafu yote, bikira aliyemzaa Nabii Isa - *Alayhi salaam* bila baba kwa uwezo wa Allah Mtukufu. Akamuumba kimuujiza usio na Mwisho kama Alivyomuumba Nabii Adamu - *Alayhi salaama* bila ya baba wala mama, na kama Alivyomuumba bibi Hawa bila ya mama, na vile vile amemumba Nabii Issa bila baba kwa uwezo wake pindi anapolitaka jambo huliambia kuwa na likawa kama Anavyosema ndani ya Qur'ani; *"Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; Alimuumba kwa udongo kisha Akamwambia: Kuwa! Basi akawa."* (Q3:59)

## 2 MUISLAMU ANAAMINI MIUJIZA YAKE *(ISSA ALAYHI SALAM)*

Kama ambavyo Muislamu anaamini miujiza ambayo Allah Mtukufu Aliipitisha katika mikono yake kama vile kuponya wenye mbalanga, vipofu, kufufua wafu na kuwajulisha watu kile watakachokula na kile watakachoweka akiba kwenye majumba yao. Yote haya yalipatikana kwa idhini ya Allah Mtukufu ili iwe ni dalili na ishara bayana za unabii na utume wake kupitia kwayo.

## 3 Allah Mtukufu Alimteremshia yeye Injili Kitabu kilicho kitukufu.

Qur'ani imeweka wazi kwamba Allah Mtukufu Alimteremshia yeye Injili moja kati ya Vitabu Vyake vikubwa, kilichokuwa nuru na rehema kwa ajili ya kuwaongoza watu, lakini kwa bahati mbaya baada ya kuondoka kwake mikono ya waandishi ilikipotosha kwa kuingiza uzushi na hadithi za wapagani wa Antiokia.

## 4 Nabii Isa-*Alayhi salaam* ni mtu si Mungu wala mtoto wa mungu.

Qur'ani imeweka wazi kwamba Nabii Isa - *Alayhi salaam* ni mtu katika wana wa Adamu - *Alayhi salaam* ambaye Allah Mtukufu Alimfadhilisha yeye na Kumtuma kwa wana wa Israelli na Akapitisha miujiza mbali mbali juu ya mikono yake, ambayo haimpi chochote katika sifa za ki-ungu wala haki ya kuabudiwa, kama Allah Mtukufu Anavyosema; *"hakuwa yeye isipokuwa ni mja ambaye Tumemneemesha na kumfannya kuwa ni mfano kwa wana wa Israeli."*(Azzukhruf: 59)

## 5 HAKUSULUBIWA LAKINI ALINYANYULIWA MBINGUNI

Qur'ani inatufahamisha sisi kwamba Nabii Isa - Alayhi salaam katu hakusulubiwa, bali Allah Mtukufu Alimwinua yeye mbinguni pale madui zake walipotaka kumuuwa. Allah Mtukufu Akafanya mtu mwingine kufanana naye na wakamuuwa na kumsulubu wakidhani kuwa ndiye. Ama kuhusu Nabii Isa - Alayhi salaam Qur'ani inathibitisha; *"Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini. Bali Mwenyezi Mungu Mtukufu Alimnyanyua Kwake. Na daima Yu Allah Mtukufu Mshinda yote, Mwenye Hekima."* (Q4:157-158)

## UKOO WA MITUME

Mitume wa Allah Mtukufu ni wengi na hawa ambao tunawataja hapa ni baadhi ya wale mashuhuri - Juu yao wao wote rehma na amani:

### Nabii Adamu - *Alayhi salaam*

Baba wa watu wote. Allah Mtukufu Alimuumba kwa udongo na Akawaamrisha malaika wote kumsujudia, sijida ya taadhima ya maamkizi, na akateremshwa kutoka Peponi hadi duniyani.

### Nabii Nuh - *Alayhi salaam*

Aliwalingania watu wake kwa zaidi ya miaka mia nane na hawakumuani. Wakaadhibiwa kwa mafuriko. Yeye na wale waliomwamini wakaokoka ile gharika kwa jahazi alilokuwa ameunda kwa amri ya Allah Mtukufu.

### Nabii Ibrahim - *Alayhi salaam*

Baba wa manabii na mmoja kati ya Mitume wakubwa. Yeye alilingania Tauhidi, yaani kumpwekesha Allah Mtukufu, na ndiye aliyeijenga Al-Kaaba, ambayo ni kibla cha Waislamu kwa amri ya Allah Mtukufu.

### Nabii Ismail - *Alayhi salaam*

Mtoto wa Nabii Ibrahim - *Alayhi salaam*, alimsaidia baba yake kujenga Al-Kaaba.

### Nabii Ishaqa - *Alayhi salaam*

Mtoto wa Nabii Ibrahim - *Alayhi salaam*, ambaye alizaliwa baada ya Malaika kumbashiria baba yake Nabii Ibrahim - *Alayhi salaam*.

### Nabii Ya'aqub - *Alayhi salaam*

Mtoto wa Nabii Is-haqa - *Alayhi salaam*, ambaye huitwa pia Israeli na ndiye chimbuko la wana wa Israeli, yaani mayahudi.

## Nabii Yusufu - *Alayhi salaam*

Mtoto wa Nabii Ya'aqub - *Alayhi salaam*, yeye alikutana na mitihani mbali mbali, lakini mwishowe akaja kuwa mtawala wa Misri.

## Nabii Musa - *Alayhi salaam*

Mmoja kati ya Mitume wakubwa, Allah Mtukufu Alimpeleka kwa wana wa Israeli na Akamteremshia Taurati kama muongozo wao. Akampa nguvu kwa muujiza mbali mbali. Firauni wa Misri akampinga na Allah Mtukufu Akamzamisha yeye baharini na Akamuokoa Nabii Musa - *Alayhi salaam* na wale waliokuwa pamoja nae.

## Nabii Daudi - *Alayhi salaam*

Nabii ambaye Allah Mtukufu Alimpa ufalme juu ya watu wake.

## Nabii Sulaiman - *Alayhi salaam*

Mtoto wa Nabii Daudi - *Alayhi salaam* ni Nabii ambaye Allah Mtukufu Alimpa ufalme mkubwa na akamdhalilishia yeye viumbe wengi.

## Nabii Zakaria - *Alayhi salaam*

Mmoja kati ya manabii wa Allah Mtukufu kwa wana wa Israeli, na ndiye aliyekuwa msimamizi wa bibi Mariamu mama wa Nabii Isa - *Alayhi salaam*, na alikuwa msimamizi mlezi na mwalimu wake. Allah Mtukufu Alimpa mtoto ambaye ni Nabii Yahya - Alayhi salaam juu ya uzee wake na ugumba wa mke wake.

## Nabii Isa - *Alayhi salaam:*

Mmoja kati ya Mitume wakubwa, Allah Mtukufu Alimuumba kutokana na mama bila baba, na Akampeleka kwa wana wa Israeli, Akamteremshia Injili na Akampa nguvu kwa miujiza mbali mbali.

## Nabii Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama*

Mtume wa mwisho wa Allah Mtukufu Aliyepelekwa kwa watu wote, na kusadikisha Mitume waliomtangulia. Na Allah Mtukufu Akamteremshia yeye Qur'ani, Kitabu kisicho na shaka yoyote na ambacho hakitaingizwa batili mbele yake wala nyuma yake.




# Ni nani mjumbe wa Uislamu



# Muhammad

Muhammad ndilo jina la Nabii wa Uislamu

Ni mojawapo ya majina yaliyoenea duniani kote leo, na Maana yake ni yule amba watu wanamtukuza na kumsifu kutokamana na Tabia zake na vitendo vyake..

Ni nani Muhammad??

## Jina la Mjumbe wa Allah Mtukufu aliyehubiri Uislamu ni:

Muhammad, mtoto wa Abdillahi, mtoto wa Abdilmutwalib, mtoto wa Hashim, al-Qurashiyyi.

Alizaliwa mwaka 570 na kutawafu mwaka 632 na ni sharti kwa Waislamu wote kuamini kuwa yeye ni:

## Mjumbe wa Allah Mtukufu kwa watu wote.

Allah Mtukufu Alimpeleka aliye mtukufu wa daraja Mtume Muhammmad - *Swallallaahu alayhi wasallama* kwa watu wote na mataifa yote na asili zao zote, na Akawajibisha watu wote kumtii. Qur-ani inaarifu kuhusu hilo; *"Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote..."* (Q7:158)

## Aliteremshiwa Qur'ani.

Allah Mtukufu Aliteremsha Qur'ani kwa Mtume Muhammad - *Swallallaahu alayhi wasallama* Kitabu kilicho muongozo na cha mwisho kwa wanaadamu wote kutoka kwa Allah Mtukufu kisicho na shaka yoyote, na hakiwezi kuingiwa na batwili ya ainan yoyote ile.

## Yeye ndiye mwisho wa wale Manabii na Mitume

Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyemtuma Muhammad Swalla llahu Alayhi Wassalam kuwa mwisho wa wale Manabii na Mitume na wala hapana Nabii wala Mtume baada yake. Kama Qur'ani inavyoarifu; *"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."* (Q33:40)



## Mzunguko wa haraka katika kumtambua Mjumbe wa Uislamu Muhammad juu yake amani

### 1. Kuzaliwa kwa Mjumbe wa Allah Mtukufu – *Swalla Llaahu alayhi wasallama*:

Yeye alizaliwa katika mji wa Makka, Magharibi yake, mwaka (570) akiwa yatima kwa baba, na mama yake akafariki bado akiwa katika umri mdogo, akalelewa chini ya uangalizi wa babu yake Abdul Mutwallib, kisha baada yake akawa chini ya malezi ya Ami yake Abii Twalib.

### 2. Maisha yake na makuzi yake:

Aliishi miongoni mwa watu wa kabila lake la Kikuraishi miaka arobaini, kabla ya kupewa Utume (570-609) akiwa mfano wa tabia njema. Na akipigiwa mfano kwa haki na ufahamu na hata akapewa lakabu mashuhuri ya 'Mkweli mwaminifu,' alipata kuchunga mbuzi katika uhai wake na baadaye akafanya biashara ya kusafiri hadi Shamu.

Kabla ya Uislamu Mjumbe wa Allah Mtukufu – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa na sifa ya wema, uaminifu na uadilifu na alikuwa akimuabudu Allah Mtukufu kupitia mila ya Nabii Ibrahim - Alayhi salaam na hakupata kuabudu sanamu wala kufuata tamaduni za kishirikina, kabla ya kuteremshiwa Qur'ani yeye hakuwa anajua kusoma wala kuandika.



### 3. Kupewa kwake utume:

Baada ya Mtume kutimiza umri wa miaka arobaini, wakati akitafakari na kufanya ibada zake katika pango la Hiraa kwenye Jabali Annuur, yeye alijiwa na Malaika Jibrilu - *Alayhi salaam* kwa mara ya kwanza na ujumbe kutoka kwa Allah Mtukufu. Na cha kwanza kilichoteremshwa kwake ni Kauli Yake Allah Mtukufu *"Soma kwa Jina la Mola wako Aliyeumba"*

Hizi ni Aya adhimu zilizo ashiria tangu mwanzo kuteremshwa kwa nuru na rehema na elimu na muongozo kwa wanaadamu wote. Halafu baada ya hapo, Qur'ani ambayo ni maneno ya Allah Mtukufu ikaendelea kuteremshwa kwa muda wa miaka ishirini na tatu.



**4. Mwanzo wa kulingania kwake**

Mtume – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* alianza kulingania watu Dini ya Allah Mtukufu kwa siri muda wa miaka mitatu. Halafu akadhihirisha da'awa na kuitangaza katika mji wa Makka, kwa muda wa miaka kumi. Na wengi wa wafuasi wake walikuwa kundi la watu wanyonge na maskini, kama ilivyokuwa kwa Mitume wengine waliomtangulia. Mtume – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* na waumini wengine walipambana na aina mbali mbali za adhabu, taabu na dhulma na upinzani mkali kutoka kwa makafiri wa Kikuraishi, baadaye akaanza kuulingania Uislamu kwa watu wa makabila waliokuwa wanakuja Makka kuhiji, na watu wa Madina wakawa ndiyo wa kwanza kuukubali, hapo Waislamu wakaanza kuhamia huko kidogo kidogo.

**5. Kuhama kwake:**

Alihamia Madina iliyokuwa ikiitwa Yathriba mwaka 622 akiwa na miaka hamsini na tatu, baada ya wakubwa wa Kikuraishi kuendelea kumfanyia vibaya wakipinga da'awa yake. Aliishi Madina miaka kumi akilingania Uislamu, na akaamrisha kuswali na kutoa zaka, na tabia njema zote pamoja na Sharia nyingine za Uislamu tunazozijua leo hii.




**6. Kueneza kwake Uislamu:**

Mjumbe wa Allah Mtukufu ndiye muasisi wa utamaduni wa Kiislamu katika mji wa Madina baada ya yeye kuhamia hapo mwaka 622H na kuasisi misingi ya jamii ya Kiislamu. Akaondoa ubaguzi, ukabila na akaeneza elimu, akaweka misingi ya uadilifu, istiqama, udugu, kusaidiana na nidhamu. Hata hivyo baadhi ya makabila wakati huo, wakiwemo mayahudi walijaribu kuumaliza Uislamu kabla ya kustawi kwake na vikatokea vita na matukio. Allah Mtukufu Akainusuru Dini Yake na Mtume Wake, kisha watu wakafululiza kuingia katika Uislamu. Uislamu ukaingia Makka na sehemu kubwa ya miji na makabila katika bara Arabu wakaingia kwenye Uislamu kwa hiyari na kuiridhia hii Dini iliyo tukufu.

**7. Kutawafu kwake:**

Alitawafu katika mwezi Safar (mfungo tano) mwaka wa 11 tangu kuhamia kwake Madina, baada ya yeye kufikisha ujumbe na Allah Mtukufu kwa ukamilifu wake na kutimiza ile neema juu ya watu wote kwa kuwafikishia wao Dini. Mtume – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* alipatwa na homa na ugonjwa ukamzidia, akatawafu mchana wa mwezi wa mfungo sita, mwaka wa 11 ambao ni sawa na 6/8/632 akiwa na miaka 63. Akazikwa ndani ya nyumba ya mkewe mama Aisha - *Radhiyallaahu anha* kando ya msikiti wake Mtukufu.






# Mtume Muhammad - *Swalla Llaahu alayhi wasallama* kwa mtazamo wa wale waadilifu



Kwa

Kwa mtu yeyote aliye muadilifu (vyovyote itakavyokuwa elimu yake) pale atakaposoma historia iliyotukuka ya Mtume Muhammad *Swalla Llaahu alayhi wasallama* kuanzia kuzaliwa kwake, maisha yake kabla ya Utume na baada ya Utume wake, hatakuwa na jinsi isipokuwa kustaajabishwa kwa mafanikio makubwa aliyopata katika nyanja zote za maisha yake. Hivyo tunaona wanazuoni wa magharibi, wanafalsafa, wanafikra na wanafasihi wa mashariki na magharibi wanalishuhudia hilo na kuandika kwa urefu mafanikio yake katika vitabu na maandishi yao mbali mbali, miongoni mwa hayo ni haya yafuatayo:



## Gandhi alisema katika gazeti 'Young India,' 1924

"Nilitaka kujua sifa za mtu aliyeweza kumiliki nyoyo za mamilioni ya watu bila ya kutumia nguvu, kwa hakika nimekinaishwa kwamba upanga haikuwa njia ambayo Uislamu ulipata nafasi yake, lakini ni kupitia huruma na upole wa aliye Mtukufu wa daraja Swalla Llaahu alayhi wasallama pamoja na umakini na ukweli wake katika ahadi na urafiki wake kwa wafuasi wake, ujasiri pamoja na kumtegemea kwake Allah Mtukufu katika ujumbe wake. Sifa zote hizo ndizo zilizotengeneza njia ya Uislamu kustawi katika makontineti yote duniyani na kupambana na masaibu wala si upanga. Baada ya kusoma sehemu ya pili ya maisha ya Mtume *Swalla Llaahu alayhi wasallama* nilisikitika kuwa sikupata kingine cha kumjua zaidi."


Mahatma Gandhi, taarifa iliyochapishwa i 'Young India,' 11/9/1924

«Nilitaka kujua sifa za mtu ambae amemiliki mioyo ya mamilioni ya watu bila ya kuwa na mpizani Nimeamini kwa yakini kwamba upanga haukuwa ndio njia ambayo Uislam ilipata nafasi yake» Mahatma Gandhi



Katika kitabu chake mashuhuri, 'Mtu aliyepata mafanikio makubwa ulimwenguni katika historia' **Michael Hart** katika watu maarufu mia moja amemuanza Mtume Muhammad –*Swalla Llaahu alayhi wasallama* na akatoa sababu kwa kusema; "Kwa hakika kumchagua kwangu Muhammad kuwa wa kwanza katika watu watukufu katika historia ya mwanadamu, kunaweza kuwashangaza wasomaji. Hata hivyo lazima nikiri kwamba yeye ni mtu pekee katika historia duniyani ambaye amefanikiwa kwa kiwango kikubwa kabisa kidini na kidunia."


Rejea kitabu, The 100: A Ranking of the Most Influential Persons in History Ukurasa wa 3.



Katika kitabu chake 'Historia ya Uturuki' mshairi mmoja wa Kifaransa **Alphonse de Lamartine** amesema; 'Kwa hakika utakasifu wa makusudio, udhaifu wa nyenzo na ukubwa wa matokeo, ni sifa tatu za weledi wa mtu. Ni nani basi anaweza kumlinganisha Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* na watukufu wengine katika historia nzima?" Histoire de la Turquie, Juzuu ya 1 Ukurasa wa 111.



Na mwanafalsafa mashuhuri wa Kihindi, **Ramakrishna** anasema; "Mazingira yamebadilika lakini Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* hajabadilika, iwe ni katika ushindi au katika kushindwa, katika utawala au katika majanga, katika raha au katika shida. Yeye ni mtu yule yule na kwa sifa zile zile, kama zilivyo Alivyotaka Allah - Mtukufu kwa manabii wote ambazo kamwe haziwezi kubadilika." Angalia kitabu, 'Muhammad the Prophet of Islam' Ukurasa wa 24.



Mshairi mkubwa wa Kijerumani bwana **Goethe** alipata kujieleza katika barua yake kwa mpenzi wake kuhusu kuvutiwa kwake na Uislamu na kwa Mtume Muhammad –*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kwa kusema; 'Kwa hakika yeye (Goethe) hata baada ya kufikisha miaka sabini hakuacha kabisa kuendelea kuvutiwa na Dini ya Kiislamu, bali alikuwa anatamani iendelee kupata mafanikio." Hayo yalitajwa na Katharina Mommsen katika kitabu chake kuhusu Goethe 'Goethe und die arabische Welt, Ukurasa wa 177.

**Profesa Stobart anasema;** "Hakuna mfano mmoja katika historia ya duniya unaokaribia ule wa haiba ya Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama*. Hakupata kumiliki mali nyingi, lakini ni makubwa mangapi aliyokuja nayo na ushindi katika medani za vita. Na lau sisi tungesoma historia kwa mtazamo huu, tusingepata jina lenye nuru iliyo wazi kama ilivyokuwa ile ya nabii Mwarabu wa Makka." Rejea kitabu, "Islam and Its Founder," Ukurasa wa 227-228.



Katika kitabu chake 'Historia ya Utawala wa Kiislamu,' Simon Ockley, anasema; "Si kuenea kwa mafunzo ya Uislamu pekee kunakostahili kusherehekewa lakini na ile hali ya kuendelea na kudumu kwake tunakokushuhudia. Uzuri wa mji ule wa Makka na Madina na nakshi nzuri aliyoiacha Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* katika nafsi za wahindi, waafrika, wazungu na waturuki ambao ni wageni na lugha ya Qur'ani." Angalia kitabu "History of the Saracen Empire, Ukurasa wa 174."

> Hisia zilezile mzuri ambazo Muhammad amefumba huko Makka na Medina bado ina uzuri na nguvu sawa katika mioyo ya Wahindi, Waafrika na Waturuki ambao ni mpya kwa Qur'an. Simon Oakley



**Will Durant** katika Encyclopedia yake mashuhuri kuhusu historia ya ustaarabu anasema:

"Kama tutaangalia vigezo vya mtu kuwa mtukufu kutokana na kuwa mtukufu kwa watu wake na athari yake kwao, basi tungesema, 'Hakika Muhammad alikuwa ni mtukufu miongoni mwa watukufu katika historia. Alinyanyua kiwango cha mitazamo ya kiroho na kimaadili ya watu waliokuwa na sifa za ujinga na kiza cha kinyama iliyoambatana na hali ya joto na ukavu wa jangwa. Alifanikiwa katika malengo yake kwa kiwango ambacho hajapata kufanikiwa yeyote katika kutafuta ustawi wa jamii yake katika historia nzima.

Pale alipoanza kuhubiri Dini, Arabuni kote watu walikuwa makabila yanayoabudu masanamu, lakini wakati alipotawafu aliacha wakiwa taifa kubwa lililoshikamana vyema kwa umoja. Aliweza kuondoa uadui uliokuwa miongoni mwao na ushirikina na akaweza kuwatumia katika kutangaza Dini. Aliacha maingiliano mazuri na utengamano mzuri kati ya wakristo na wayahudi waliokuwa wakiishi katika dola ya Kiislamu wakati huo. Pamoja na watu wake alisimamisha Dini iliyo nyepesi, iliyo wazi na yenye nguvu, yenye maadili mazuri pamoja na ujasiri na uzalendo. Aliweza kushinda vita mia moja na kwa zaidi ya karne moja kuwa na dola yenye nguvu na kubakisha hadi leo hii nguvu yenye athari kubwa katika nusu ya sehemu ya ulimwengu.

Rejea kitabu, The Story of Civilization: The age of faith, Juzuu ya 4, Ukurasa wa 174.

> Tukiuhukumia utukufu kwa athari anayoacha kwa watu, basi tutasema: kwamba Muhammad alikuwa ni Mtukufu wa Watukufu katika Historia» Je, Durant

Imepokewa kwetu (baada ya kusilimu kwake) mmoja katika maadui wakubwa wa Mtume Muhammad – Swalla Llaahu alayhi wasallama kisa chenye kushangaza. Nayo inahusu barua ya Mtume – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* kwa Hercules mtawala wa Roma mwaka 628 C.E, akimualika kunako Uislamu, Hercules alishangazwa na hilo na akataka mtu anayetoka Arabuni, mwenye ujamaa na aliyetuma barua ile, aliye nchini aitwe mbele yake. Mtu aliyekuwepo nchini kwake wakati ule alikuwa ni Abu Sufyan aliyekuwa kule akielekea Syria kwa ajili ya biashara. Abu Sufyan alikuwa mmoja miongoni mwa wakuu wa kabila la Makuraishi na aliyekuwa adui mkubwa wa Nabii Muhammad – Swalla Llaahu alayhi wasallama wakati ule. Aliitwa kwenye kasri la mfalme na Hercules akaanza kumuuliza maswali kuhusu Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* kupitia mkalimani wake. Maswali ya Hercules kwa Abu Sufyan yalijaa hekima na utulivu wa akili wa hali ya juu. Yeye alitaka kujua ukweli na uaminifu wa Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama*, baada ya Maswali yake kujibiwa Hercules alisema kumwambia Abu Sufyan;

"Nimekuuliza kuhusu nasaba yake, na umesema kuwa yeye ni mtu mwenye nasaba nzuri kwenu, vivyo hivyo manabii hutumwa kutoka watu wenye nasaba nzuri miongoni mwa watu wa kaumu yake. Nimekuuliza kama amewahi kutokea mtu miongoni mwenu aliyepata kudai kama anavyodai yeye? Umesema; 'La, hapana,' Nami nimekuambia kuwa kama angekuwepo aliyepata kusema hivyo kabla, ningesema; 'Bila shaka bwana huyu anamuiga mtangulizi wake.'

Kisha nimekuuliza, 'Hivi nyinyi mlipata kumtuhumu yeye kwa uongo kabla hajasema alichokisema?' Umesema; 'La, hapana!' Hapo nimejuwa kwamba asingeweza kuwa mkweli kwa watu kisha awe muongo kwa Allah - Mtukufu.'

Nimekuuliza pia, 'Hivi yeye hufuatwa na watu watukufu au watu dhaifu?' Umesema kuwa yeye anafuatwa na watu dhaifu, nao hao ndio wafuasi wa Mitume. Nimekuuliza, 'Hivi wao huwa wanazidi au wanapungua?' Umesema kwamba wanazidi, na huo ndiyo mwendo wa imani hadi inapotimia.'

Nimekuuliza, 'Hivi kuna ambae anatoka katika dini yake kwa chuki baada ya kuingia?' umesema; 'La!' Na hivyo ndivyo ilivyo imani pale inapochanganyika na furaha katika nyoyo.

Nimekuuliza, 'Hivi yeye huwa hatekelezi ahadi?' Umesema; 'Hapana', Ni vivyo hivyo Mitume hawavunji ahadi.

Nimekuuliza; 'Yeye anawaamrisha nini?' Umesema; 'Anawaamrisha kumuabudu Allah-Mtukufu wala msimshirikishe na chochote, na anawakataza ibada ya masanamu na anawaamrisheni kuswali, kutoa sadaka na kujihifadhi.'

'Kama hayo unayosema ni kweli, basi yeye atamiliki sehemu moja ya mguu wangu, na nilikuwa nafahamu kwamba atakuja hivi karibuni na kuwa ameshakuja, ila sikufikiria kabisa kwamba atatoka kwenu, na kama ningeweza kumfikia basi ningefanya juhudi kubwa ili nikutana nae." (Bukhari 7)




# Baadhi ya sifa za Mtume Muhammad- *Swallallaahu alayhi wasallama* na maadili yake



# Mjumbe

Mjumbe wa Allah-Mtukufu-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* ni mfano bora wa kuigwa katika maadili mazuri kabisa ya binadamu. Hayo yameshuhudiwa na watu waliyo waadilifu mashariki na magharibi ya duniya hata na wale ambao hawakumkubali kama Mtume, kiasi cha Qur'ani kuisifu tabia yake tukufu.

Hata mama Aisha - *Radhiyallaahu anha* alipoulizwa kuhusu tabia ya Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* hakusita, yeye alitoa wasifu kwa kauli yake kwamba; 'Tabia yake ilikuwa ni Qur'ani,' yaani, alitekeleza kwa vitendo mafunzo yote ya Qur'ani kwa ukamilifu wake na maadili yake.



**Kama muhtasari wa maadili na tabia yake unavyoonyesha:**

## Unyenyekevu:

Mjumbe wa Allah-Mtukufu-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* hakukubali mtu yeyote asimame kwa kumtukuza yeye, lakini alikuwa akiwakataza wafuasi wake kulifanya jambo hilo. Kiasi kwamba wafuasi wake (pamoja na mapenzi makubwa waliyokuwa nayo kwake) hawakuwa wakisimama pale alipokuwa akielekea kwao, na walilifanya hilo kwa kufahamu kwamba alikuwa akichukizwa na jambo hilo. (Imamu Ahmad 12345)

Wakati mmoja Adiy mtoto wa Hatim kabla ya kusilimu kwake na wakati huo alikuwa mmoja kati ya watukufu wa watu wake, alikwenda kwa Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akitaka kujua lengo la yeye kutaka watu wamfuate. Adiy anasema; "*Nikaenda kwake na nikamkuta akiwa na mwanamke na mtoto ambao ilionekana wazi kwamba wako karibu na aliye Mtukufu wa daraja-Swalla Llaahu alayhi wasallama na nikajua kwamba hakuwa mfalme mfano wa Kaisari wala Kisra.*" (Imamu Ahmad 19381) Na hilo ni kwamba unyenyekevu ni tabia za manabii wote.

Alikuwa akikaa na maswahaba zake kama mmoja wao. Hakuwa akijitenga nao kiasi cha kujipambanua. Kiasi cha kwamba mgeni asiyemjuwa asingeweza kumtambua akiwa miongoni mwa wafuasi wake, hivyo mgeni hulazimika kuuliza; "*Miongoni mwenu nyinyi ni nani Muhammad?*" (Imamu Bukhari 63).

Inaelezwa kwamba baadhi ya wafuasi wake pamoja na kuwa na shughuli nyingi hakuacha kusikiliza haja zao hata zingekuwa ndogo kiasi gani. Wakati mwingine alijiwa na mwanamke aliye mfanyakazi miongoni mwa wakazi wa Madina na kumshika mkono wake na kwenda nae hata alipotekeleza mahitaji yake. (Imamu Bukhari 5724)

> Mtume wa Uislamu alikuwa akiandaa vitu vyake mwenyewe, na akihudumia familia yake na kushirikiana na wao katika kazi za Nyumbani.

Inaelezwa kwamba mmoja kati ya maswahaba wakubwa Sayyidina Umar bin al-Khattwab-*Radhiyallaahu anhu* siku moja alipata kuingia kwa Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* na akaona athari ya mkeka wa mtende katika mwili wake kwa kule kuulalia kwake. Sayyidina Umar-*Radhiyallaahu anhu* alilia sana na Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akamuuliza yeye; *"Ni nini kinachokuliza?"* Sayyidina Umar-Radhiyallaahu anhu akajibu; *"Ewe Mjumbe wa Allah-Mtukufu kwa hakika Kaisari na Kisra wanaishi maisha ya kifahari na wewe ni Mjumbe wa Allah-Mtukufu unaishi katika maisha haya!"* Mtume akamjibu: *"Hivi wewe huridhii wao kuwa na dunia na sisi tukawa na akhera?"* (Imamu Bukhari 3503)

Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa akishona nguo zake mwenyewe, na alikuwa akiwahudumia pia watu wake wa nyumbani, na akishirikiana nao katika kazi za nyumbani, na pale mama Aisha-*Radhiyallaahu anha* alipoulizwa kuhusu hali yake nyumbani alijibu: *"Alikuwa akifanya kazi za nyumbani."* (Imamu Bukhari 644) na akasema pia; *"Kama vile mmoja wenu anavyoshona viatu vyake na nguo zake."* (Imamu Ahmad 24749)

Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Hatoingia peponi yule mwenye chembe cha kiburi."* (Imamu Muslim 91)

## Huruma:

Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Wenye huruma hufanyiwa huruma na Yule Aliye Mwingi mno wa huruma (yaani Allah-Mtukufu), hivyo basi wahurumieni walio katika ardhi na Aliye mbinguni Atakuhurumieni nyinyi."* (Imamu Abu Daud 4941)

**Huruma ya aliye mtukufu wa daraja-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* ilionekana katika maeneo mengi miongoni mwayo ni:**

### Huruma yake kwa watoto:

- Pamoja na kuwa Swala ndio uti wa mgongo wa Dini ya Kiislamu ambamo ndani yake watu hawatakiwi kuzungumza, kula au kujishughulisha na chochote. Wakati mmoja Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa amembeba mjukuu wake Umama mtoto wa bibi Zainabu, na ikawa pale anapotaka kusujudu anamuweka chini na anaponyanyuka humbeba tena. (Imamu Bukhari 494).
- Ilikuwa pale Mtume - *Swalla Llaahu alayhi wasallama* anaposwalisha halafu yeye akasikia kilio cha mtoto miongoni mwa waumini alikuwa akifanya haraka kuimaliza Swala ile. Kama alivyopata kusema; *"Mimi husimama kuswali nikikusudia kuirefusha, lakini pale ninaposikia kilio cha mtoto, mimi huifupisha Swala yangu kwa kutopenda kuweka uzito kwa umma."* (Imamu Bukhari 675)

### Huruma yake kwa Wanawake

- Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alihimiza malezi mazuri kwa watoto wa kike na kuwafanyia wema, alikuwa akisema; *"Atakayeruzukiwa mtoto mmoja wa kike au zaidi ya mmoja, na akamlea vizuri na kumfanyia wema, basi mtoto yule atakuwa pazia yake (yenye kumkinga) na moto."* (Imamu Bukhari 5649)
- Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* ameacha wosia na kuhimiza haki za mke nyumbani na kushughulikia mahitaji na mazingira yake, na kwa hivyo akawaamrisha Waislamu wenyewe wausiane kuhusu hilo na akasema: "*Wausieni wanawake kheri."* (Imamu Bukhari 4890).
- Na akatoa mfano wa wema na huruma kwa mmoja wa wake zake, wakati akiwa ameketi kwenye ngamia wake, hivyo akaweka goti lake na mama Sofia, mkewe akaweka mguu kwenye goti lake ili apate kupanda juu ya ngamia. (Imamu Bukhari 2120).
- Kila pale binti yake Fatuma alipomjia yeye Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa akiuchukua mkono wa binti yake na kuubusu na kuketi nae sehemu anayokaa. (Imamu Abu Daud 5217).

### Huruma yake kwa wanyonge

- Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amehimiza sana watu kuwahudumia yatima, alikuwa akisema: "Mimi na mtu anayehudumia yatima tutakuwa hivi peponi" akiashiria kwa vidole vyake vya kati na kinachofuatia (Imamu Bukhari 4998).
- Kadhalika yule anayewasaidia wajane na fukara ni kama vile aliyepigana jihadi na aliyefunga mchana na akasimama usiku kuswali (kwa malipo). (Imamu Bukhari 5661).
- Aliwafanyia wema watu wanyonge na kuhakikisha kuwa wanapata haki zao kama sababu za riziki kwao na ushindi kwa adui, na kuhusu hili alikuwa akisema; "Nitafuteni kwa watu wenu wanyonge (mtanipata), kwa hakika nyinyi mtanusuriwa na kuruzukiwa kwa wale wanyonge wenu." (Imamu Abu Daud 2594).



Mtume Muhammad alijalia kule kuwasaidia wanyonge na kuwafanyia hisani ni sababu ya kuruzukiwa na kupata ushindi.

## Uadilifu wake:

- Mtume alikuwa mwadilifu, akisimamia sheria za Allah-Mtukufu bila ya ubaguzi wowote hata kwa watu wake wa karibu, wakati wote alifuata maelekezo ya Qur'ani: *"Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wawili na jamaa zenu."* (Q4:135)
- Wakati fulani baadhi ya maswahaba zake walikwenda kwa Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama ili kumuombea mwanamke mmoja aliyekuwa na hadhi katika jamii yake asiadhibiwe kwa kosa la wizi. Na yeye akasema; *"Kwa Yule Ambaye nafsi yangu I katika Mamlaka Yake, lau kama Fatuma, mtoto wa Muhammad angekuwa ameiba mimi ningemuadhibu yeye."* (Imamu Bukhari 4053)
- Pale alipowakataza watu riba, yeye alianza na watu wake wa karibu ambao ni baba yake mdogo Sayyidina Abbas –*Radhiya Llaahu anhu*, *"Na riba ya kwanza ambayo mimi ninaiondoa ni riba yetu, ile ya Abbas bin Abdul Mutwalib, kwani yote imeachwa."* (Imamu Muslim 1218)
- Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alifanya kipimo cha ustaarabu wa umma na maendeleo yake ni mtu mnyonge kuweza kuchukua haki yake kwa mtu mwenye nguvu bila ya woga wowote wala kubabaika. Mtume - *Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Umma bado haujaongoka kama mnyonge hawezi kuchukua haki yake kwa mwingine."* (Imamu Ibn Majah 2426)

## Wema na ukarimu wake:

- Mtu mmoja alipata kwenda kwa Mtume –*Swalla Llaahu alayhi wasallama* na akamuuliza kuhusu mali, akamwambia: *'Nunua unachotaka na kile kinachobaki nitakilipa,'* Swahaba wake aitwae Umar akasema; *"Ewe Mjumbe wa Allah-Mtukufu yeye anakubebesha lile usiloliweza."* Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akakasirika kuhusu hilo na yule bwana akasema; "Toa wala usihofu kupungua kwa Yule Mwenye kiti cha enzi (Allah-Mtukufu)." Aliye Mtukufu wa daraja-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akatabasamu na akajuwa furaha iliyo kwenye uso wake (Al-Ahadiith Al-Mukhtaarah 88).
- Wakati fulani Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alipata kupelekewa Dirhamu elfu themanini za fedha, yeye akaziweka juu ya busati kisha akaanza kuzigawa. Hakumnyima muombaji yeyote mpaka zilipomalizika. (Imamu Hakimu 5423).

## Subira na uvumilivu wake:

- Historia inaonyesha kwamba Mtume *-Swalla Llaahu alayhi wasallama* alitoka Twaif (mji ulio mbali na Makka yapata kilomita 90) akiwa amejaa mawazo baada ya wakazi wake kumgeuka wakati alipokwenda kuwalingania kunako Uislamu. Watu wale walimkejeli na kumjibu vibaya, wakati wa kurejea kwake Makka Allah-Mtukufu Aliwatuma malaika ambao walimuuliza kama anataka watu wa Twaif waangamizwe kwa makosa yao na yeye akasema; *"Bali mimi nataraji Allah-Mtukufu Atoe ndani ya viuno vyao watakaomuabudu Yeye Peke Yake bila ya kumshirikisha na chochote"* (Bukhari 3059)
- Na kubwa zaidi ni msimamo wake kwa watu wa Makka, wale ambao walimtoa katika mji wake na kumfanyia vibaya kwa maneno na panga zao, ambao hawakumpa nafasi ila kumfanyia kila aina ya vitimbi kwa miaka mingi. Pale ilipokuja nusura ya Allah-Mtukufu na yeye kuuteka mji wa Makka na watu wote wakawa chini yake! Yeye alisimama na kuwauliza; *"Mnafikiri mimi nitawafanya nini leo hii?"* Wao wakasema; *"Heri tupu, ewe ndugu mkarimu na mtoto wa ndugu aliye mkarimu,"* Yeye akawaambia; *"Mimi ninawaambia kama alivyosema ndugu yangu Yusufu (akimkusudia Nabii Yusuf - Alayhi salaam, mtoto wa Nabii Ya'aqubu ambaye aliwasamehe ndugu zake wale waliomtumbukiza kisimani) yeye alisema; "Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu Atakusameheni, Naye ni Mwingi wa Kurehemu kuliko wote wanaorehemu."* (12:92) *"Nendeni nyinyi nyote leo mko huru."* (Imamu Baihaqi 18275)

> Vyanzo mbali mbali vimeelezea kuwa Mjumbe wa Uislamu hakuwa na pupa lakukusanya mali katika Maisha



## Kujizuwia na mambo ya dunia:

- Mara kwa mara Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa akifuata Kauli ya Allah-Mtukufu kwa kusema: "*Wala usivikodolee macho Tulivyo wastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao, kwa ajili ya mapambo ya duniani, ili Tuwajaribu. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora na inadumu zaidi.*" (20:131)
- Siku moja Sayyidina Umar-*Radhiyallaahu anhu* mmoja miongoni mwa maswahaba wa Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikwenda kwake na kumkuta amelala kwenye mkeka usio na godoro na upande mmoja wa mwili wake ukiwa na alama za mkeka ule. Sayyidina Umar-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* anasimulia; Niliitazama nyumba yake, Wallahi sijapata kuona kitu kinachostahiki kutazamwa kwa kina, nikageuka na kumwambia Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama*; Muombe Allah-Mtukufu awape wasaa wa uchumi umati wako, kwani Wafursi na Warumi wamepewa wasaa wa mali, dunia imekuwa yao na huku katu wao hawamuabudu Allah-Mtukufu!" Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akasema, "*Hivi, Ibn Khattwab bado wewe una shaka, wao ni watu waliotanguliziwa mema yao hapa duniani.*" (Imamu Bukhari 2336)
- Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa akisema: "*Nina nini mimi na dunia, mimi na dunia ni kama msafiri aliyefika kwenye kivuli cha mti kupumzika na kisha kuendelea na safari yake na kukiacha kivuli kile.*" (Imamu Tirmidhi 2377)
- Ilikuwa ikipita mwezi na wakati mwingine miwili au mitatu nyumbani kwake hakujawashwa moto kwa kupika bali wakila tende na maji tu (Imamu Bukhari 2428); na wakati mwingine akipitisha siku mbili bila ya kula walau tende kidogo tu na kujaza tumbo lake (Imamu Muslim 2977). Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama hakupata kushiba siku tatu mfululizo kwa mkate hadi alipotawafu, na mkate aliopenda kula ni wa shairi. (Imamu Muslim 2976).

> Mjumbe wa uislamu anajifananisha hali yake na Dunia ni kama vile hali ya msafiri aliekaa kwenye kivuli cha mti kisha akaondoka na kukiwacha.



## Utekelezaji wake wa ahadi:

- Utekelezaji wa ahadi ni miongoni mwa sifa tukufu na katika maadili yale mazuri. Na humpa mtu nafasi nzuri kama hilo litakuwa ni kwa lengo la kurudisha zuri la mtu huku hapana ulazima wa hilo kati ya pande mbili za watu. Jambo hilo lilikuwa moja katika ada za Mjumbe wa Allah-Mtukufu - *Swalla Llaahu alayhi wasallama* ambaye alikuwa akirejesha jema kwa tukufu zaidi kuliko lile. Pamoja na kuwa hakuna mkataba wala ahadi katika yao, sasa ingekuwa vipi kama kungekuwepo na ahadi au mkataba.


- Wakati Hercules, mfalme mkristo alipowauliza makafiri wa Kikuraishi kuhusu sifa za aliye Mtukufu wa daraja –*Swalla Llaahu alayhi wasallama*; "Je, yeye huvunja ahadi?" Wao walijibu; "Hapana!" Yeye akawaambia; "Vivyo hivyo Mitume hawavunji ahadi." (Imamu Bukhari 7)

- Na katika ubora huo yeye alionyesha kiwango cha juu cha utekelezaji wa ahadi kwa mke wake wa kwanza mama Khadija-*Radhiya Llaahu anha*, alihifadhi nafasi na hadhi yake. Alikiri nafasi yake kwake na aliendelea kuwakirimu rafiki na jamaa zake wa karibu.



- Mama Aisha-*Radhiyallaahu anha* aliyekuwa mke wa Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* anasimulia kuhusu utekelezaji wake wa ahadi kwa mkewe wa kwanza mama Khadija-*Radhiyallaahu anha* aliyefariki muda mfupi baada ya kupewa Utume. Mama Aisha-*Radhiyallaahu anha* hakupata kumfahamu na alikuwa anasema; "Mtume alikuwa akimtaja sana Khadija na wakati mwingine alikuwa akichinja mbuzi na kukata kata nyama yake na kisha kuwagawia marafiki wa Khadija. Wakati mwingine nilikuwa namwambia; "Unafanya kana kwamba hakuna mwanamke mwingine duniani isipokuwa Khadija?' Na hapo yeye alikuwa anasema; "Kwa hakika Khadija alikuwa hivi na hivi… na kuanza kutaja mazuri yake." (Imamu Bukhari 3607
- Wakati fulani Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alipokea ujumbe kutoka kwa An-Najashi (mfalme wa Ethiopia aliyewapokea na kuwalinda waislamu walipohamia huko katika ile Hijra ya kwanza). Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama alisimama* na kuwahudumia mwenyewe, maswahaba zake wakasema; *"Sisi tutafanya hayo!"* Yeye akasema; *"Hawa waliwakirimu maswahaba zangu na nami ninapenda kuwalipa."* (Shiib Al-Iman 8704)

Kwa hakika Mtume Muhamad - *Swalla Llaahu alayhi wasallama* alionyesha mifano mikubwa ya kimaadili katika nyanja zote za maisha yake akitekeleza amri ya Allah-Mtukufu na kufuata tabia za manabii waliomtangulia.



Msikiti wa Mtume Muhammad, ambao alijenga huko Madina au Madinatul Munawara kama unavoitwa na Waislamu ni mji mtakatifu wa pili baada ya Makka, Mtume Muhammad alihamia na akajenga msikiti wake na kuzikwa huko, na Msikti huu unatembelewa na mamilioni ya Waislamu kila mwaka.



# Baadhi ya maneno ya Mtume Muhammad -

*Swalla Llaahu alayhi wasallama*



Waislamu


Waislamu walizingatia sana maneno ya Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* na kuyanukuu kama walivyosikia kutoka kwake kwa kuyaandika. Wenye kuhifadhi pamoja na wanazuoni walishindana katika kuhifadhi maneno yake, na kwa hivyo kutuachia sisi mfumo madhubuti wa kuthibitisha habari na maarifa yanayonasibishwa kwa Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama*, kilichothibiti na kile kilicho kinyume chake. Hali hiyo imezingatiwa hadi kwenye sentensi na maneno, na kwa hivyo kuwa rahisi kubainisha kile kilichooongezwa kutoka asili yake.

**Baadhi ya hadithi maarufu zilizonukuliwa kutoka kwake-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* ni hizi zifuatayo;**

- *"Kwa hakika matendo ni kwa nia, na kila mmoja atalipwa kwa nia aliyoiweka."* (Imamu Bukhari 1)
- *"Wema ni tabia njema, na ovu ni lile ambalo linawasha ndani ya nafsi yako, usilopenda watu walione."* (Imamu Muslim 2553)
- *"Muogope Allah-Mtukufu popote ulipo, na fuatisha jema baada ya uovu, na tangamana na watu kwa maadili mema."* (Imamu Tirmidhi 1987)
- *"Ipe nyongo dunia Allah-Mtukufu Atakupenda, na yape nyongo yaliyo kwa watu, watu watakupenda."* (Ibn majah 4102)
- *"Mfano wangu na manabii waliotangulia ni kama lile jengo lililojengwa, lakini likawa na kasoro ya tofali moja kwenye kona yake, watu wakawa wanalizunguka kwa kushangazwa na uzuri wake na huku wakisema; Kwa nini tofali lile lisiwekwe? Mimi ndio lile tofali na hitimisho la wale manabii."* (Imamu Bukhari 3342)
- *"Yeyote atakayemuondolea muumini tatizo katika matatizo ya duniani, Allah - Mtukufu Atamuondolea yeye tatizo miongoni mwa matatizo ya siku ya Kiyama, na atakayemuondolea uzito mwenye uzito wa jambo basi Allah-Mtukufu Atamuondolea yeye uzito duniani na akhera, na Allah-Mtukufu Humsaidia mja wake madamu mja wake humsaidia ndugu yake, na atakayepita njiani akitafuta elimu ndani yake Allah-Mtukufu Atamrahisishia njia ya kwenda Peponi...na atakayechelewa katika amali yake, basi nasaba yake haitoharakishwa."* (Imamu Muslim 2699)
- *"Hatoamini mmoja wenu nyinyi hadi yeye ampendee ndugu yake kile anachopendea nafsi yake."* (Imamu Bukhari 13)



*"Si miongoni mwetu yule ambaye hawahurumii wadogo wetu na wala hajuwi haki za wakubwa wetu."* (Imamu Tirmidhi 1920)



*"Hamtoingia peponi hadi nyinyi muamini, na hamtoamini hadi nyinyi mpendane, je nikuambieni nyinyi kitu ambacho mkifanya nyinyi mtapendani? Toleaneni salamu baina yenu."* (Imamu Muslim 54)

- *"Muislamu ni yule aliyewasalimisha ndugu zake waislamu na ulimi wake na mkono wake, na mhamaji ni yule aliyehama kile alichokataza Allah-Mtukufu."* (Imamu Bukhari 10)
- *"Yeyote atakayemdhulumu asiyekuwa muislamu au kumtaka afanye jambo asiloliweza, au akachukua kitu bila ridhaa yake, basi mimi nitakuwa mtoa hoja dhidi yake siku ya Kiyama."* (Imamu Abu Daud 3052)
- *"Wenye kuhurumia hufanyiwa huruma na Aliye Mwingi mno wa huruma (Allah-Mtukufu), hivyo wahurumieni walio katika ardhi na nyie mtahurumiwa na Aliye mbinguni"* (Imamu Abu Daud 4941)
- *"Atakayeiba si miongoni mwetu."* (Imamu Tirmidhi 1315)
- *"Mfano wa waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao ni mfano wa kiwiliwili, kiungo kimoja kikilalamika, basi kiwiliwili kizima kitakesha kwa homa."* (Imamu Muslim 2586)
- *"Kila mmoja ni mchunga na kila mmoja ataulizwa kuhusu kile alichokichunga, Imamu ni mchunga na ataulizwa kwa alichokichunga, mwanamme ni mchunga wa familia yake na ataulizwa kwa alichokichunga na mwanamke ni mlinzi wa nyumba ya mume wake nae ataulizwa kwa alichokichunga, ehe jueni ya kwamba nyote ni wachunga na mtaulizwa kwa mlichokichunga."* (Imamu Bukhari 4892)
- *"Mkamilifu wa imani ni yule aliye mkamilifu wao kwa tabia, na mbora wenu ni yule aliye mbora wenu kwa wanawake."* (Imamu Tirmidhi 1162)
- *"Mbora wenu nyinyi ni yule aliye mbora wenu kwa mke wake na mimi ni mbora kwa wake zangu."* (Imamu Tirmidhi 3895)

- *"Hakika Allah-Mtukufu Hupenda upole katika mambo yote." (Imamu Bukhari 5678) na amesema pia; "Atakayenyimwa upole ameharamishiwa kheri zote." (Imamu Muslim 2592)*
- *"Alama za mnafiki ni tatu: Anapozungumza husema uongo, na anapoahidi huenda kinyume na ahadi yake, na anapoaminiwa hufanya hiana."* (Imamu Bukhari 33)
- *"Miongoni mwa mema ya Uislamu ni mtu kuacha yasiyomuhusu."* (Imamu Tirmidhi 2317)
- *"Mtu mmoja alikuwa safarini halafu akapatwa na kiu, akaona kisima akateremka ndani yake na kunywa maji kisha akatoka. Halafu akamuona mbwa akitweta na kula mchanga uliolowa kwa sababu ya kiu, yule mtu akajisemeza; 'Huyu mbwa amepatwa na kile kilichonipata mimi', basi, akashuka chini ya kisima akajaza kiatu chake maji na kumnywesha yule mbwa, akamshukuru Allah-Mtukufu na Akamsamehe. Maswahaba zake wakamuuliza; "Ewe Mjumbe wa Allah-Mtukufu hivi sisi tutapata hata kwa wanyama ujira?" Mtume - Swalla Llaahu alayhi wasallama akasema; "Katika kila ini (mnyama au kiwiliwili) kuna ujira."* (Imamu Bukhari 2466).



## Wasifu wa Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* ndani ya Qur'ani

Qur'ani tukufu inaakisi kwetu sisi haiba ya kustaajabisha ya aliye Mtukufu wa daraja-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* na namna alivyotangamana na watu waliomzunguka, yote hayo yanaonekana katika maadili na sifa zake kwa wakati mmoja;

- Yeye ni rehema kwa walimwengu wote. Rejea (Q21:107) na sio kwa Waislamu peke yao, "Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote." (Q21:107) Na sio kwa waislamu peke yao.
- Yeye ni mwenye tabia nzuri kabisa, *"Na hakika wewe una tabia tukufu."* (Q68:4)
- Alikuwa anajali sana uongofu kwa watu wake na alikuwa mwenye huzuni kubwa kwa kupotea kwao, na hili linathibitisha shauku yake katika kulingania na kwamba Allah-Mtukufu Atamtimizia kwa Anayemtaka uongofu. Rejea (11:12) na (6: 107) na (18:110)
- Yeye alikuwa anawatafutia udhuru na kuwaombea msamaha wengine, *"Mwenyezi Mungu amekusamehe! Kwa nini ukawapa ruhusa kabla ya kubainikia kwako wanao sema kweli, na ukawajua waongo?"* (9:43)
- Alikuwa ni mwenye kuwaombea hata wale waliyo adui zake wasaamehewe makosa yao, kiasi cha Allah-Mtukufu kumkataza kufanya hivyo; "*Waombee msamaha au usiwaombee. Hata ukiwaombea msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotofu."* (Q9:80)
- Kinamuwia yeye ugumu kile kinachowawia ugumu waumini, nae kwao ni raufu na mwenye huruma

*"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma."* (9:128)

- Wakati mwingine alikuwa akiona haya kuwaambia baadhi ya maswahaba zake kwamba hapendezwi na wao kukaa muda mrefu nyumbani kwake wakizungumza. Hivyo kupitia Qur'ani Allah-Mtukufu Akawahadharisha wao kuhusu jambo hilo.

*"Enyi mlio amini! Msiingie nyumba za Nabii ila mtakapopewa ruhusa kwenda kula, sio kungojea kiwive. Lakini mtakapo itwa basi ingieni, na mkisha kula tawanyikeni, wala msiweke mazungumzo. Hakika hayo yanamuudhi Nabii naye anakustahini, lakini Mwenyezi Mungu Hastahi kwa jambo la haki. Na mnapo wauliza wakeze haja waulizeni nyuma ya mapazia. Hivyo ndio usafi zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haikufalieni kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala kuwaoa wake zake baada yake kabisa. Hakika jambo hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu."* (Q33:53)

- Alikuwa mwepesi na rahisi kuzoeleka, mwenye moyo laini, alitangamana na maswahaba zake kwa upole na alishauriana nao na kuchukua rai zao katika hali ngumu:

*"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanao mtegemea."* (Q3:159)



# Qur’ani tukufu iliyo muujiza wa milele



# Qur'ani

Qur'ani ni Kitabu kilichoenea na kupatikana duniyani kote. Hiki ndiyo Kitabu pekee kinachoaminiwa na idadi kubwa zaidi ya watu ulimwenguni, waislamu na wasio waislamu, hata kama baadhi yao hawataki kukiri kwa kuwa waislamu.

**Qur'ani ni Kitabu kutoka kwa Allah-Mtukufu kama muongozo kwa watu wote na kinachoaminika kwamba:**

- Ni maneno ya Allah-Mtukufu yaliyoteremshwa na malaika Jibrilu-*Alayhi Salaam* kwa Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kama nuru na muongozo kwa watu wote.
- Kitabu cha mwisho miongoni mwa Vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni.
- Ni Kitabu kisicho na shaka yoyote katika maudhui yake, kilichosheheni kweli tupu, kinachohifadhiwa na Allah-Mtukufu na ambacho katu hakitabadilishwa kwa mikono ya waandishi wala kupotoshwa.
- Ni Kitabu kinachotumiwa katika ibada na kukisoma na kukihifadhi ni ibada, na hutumika pia katika kuongoza maisha ya kijamii ya waislamu kwa hukumu na sheria zake.

Qur'ani ilianza kuteremshwa kupitia malaika Jibril - *Alayhi salaam* baada ya Mtume –*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kutimiza miaka arubaini na Aya tano za mwanzo kuteremshwa kwake ni: *"Soma kwa Jina la Mola wako Yule Ambaye Ameumba."* (Q96:1)

Baada ya hapo ikaendelea kuteremshwa kidogo kidogo kwa muda wa miaka ishirini na tatu kufuatana na haja na matukio mbali mbali.

Qur'ani imegawanyika katika Sura 114 zilizo na maudhui mbali mbali. Hata hivyo kwa makubaliano ya wanazuoni kinachostaajabisha zaidi ni ule umbuji wa lugha ya kiarabu na mtungo wa sentensi zake katika kuwaongoa watu na kuwalingania wao katika kumuabudu Allah-Mtukufu, Mmoja tu Aliye wa Pekee.

> Aya ya kwanza kuteremka katika Qur'ani ni (Soma kwa jina la Mola wako alieumba) na kuteremka kidogo kidogo kwa mda wa miaka 23 kulengana na hali na matukio.

## Na Qur'ani inazungumzia hayo kama ifuatavyo:

1. Kuthibitisha kuwa Allah-Mtukufu ni Mmoja na wa Pekee na kupinga utata wa wenye kumshirikisha.
2. Inaelezea visa vya Mitume na Manabii na nyumati zilizotangulia.
3. Lingano la kuchunguza ulimwengu mpana na kuangalia viumbe vyake vinavyotuzunguka, na kwamba neema za Allah-Mtukufu kwetu sisi ni nyingi.
4. Kubainisha sheria za Dini na maamrisho na makatazo yake.
5. Kubainisha sifa za muumini na maadili yao na kuhadharisha kuhusu sifa mbaya.
6. Mazungumzo kuhusu siku ya mwisho na malipo ya waja wema na malipo ya waovu.
7. Kuwalea waumini kupitia maelezo ya matukio yaliyokuwa yakimtokea Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama*.

**Zifuatazo ni baadhi ya sifa za Qur'ani**

## Muujiza wa kuihifadhi:

Allah-Mtukufu Amekifanya kuwa Kitabu cha mwisho na kwa sababu hiyo Qur'ani ndiyo Kitabu pekee kilichohifadhiwa katika nyoyo za watu, na katika Aya nyingi Amekiita 'Kitabu' kama ishara ya maandiko Yake na kuhifadhiwa kwake kimaandishi. Na kwa hivyo Qur'ani imehifadhiwa katika hali mbili kwa wakati mmoja, ikawa kila ilipoteremshwa Aya ya Qur'ani iliandikwa papo hapo, na papo hapo kuhifadhiwa katika nyoyo. Ushahidi wa waliyoihifadhi hautokubaliwa kama kutakuwa na tofauti na kilichoandikwa au kupokewa kutoka kwa Mjumbe wa Allah-Mtukufu-*Swalla Llaahu alayhi wasallama.*

Wakati ambapo wanazuoni wa kikristo wanakiri kwamba mgongano wa maneno ulio katika hayo maadishi yanayodaiwa kuwa ni Injili ni kutokana na waandishi na vyanzo vyao mbali mbali, na kule kuwa kwamba ile Injili ambayo Nabii Isa-*Alayhi salaam* alipewa si katika vyanzo vya hayo maandishi yanayoitwa Injili leo hii. Hata hivyo ni maoni yanayokubalika kwamba wanachotumia ni kitabu kilicho na mafunzo na visa vya wanadamu ndani yake.

Ni ukweli uliyo wazi kwamba kwa hakika Qur'ani ni Kitabu kisicho na mgongano wowote ule. Kwa kuwa maneno na maudhui yote yanatoka kwa Allah-Mtukufu, na kisha kuhifadhiwa katika moyo wa Mtume – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* na baadhi ya maswahaba zake na pia katika maandishi kutoka kwa Mtume mwenyewe - *Swallallaahu alayhi wasallama* aliyepokea Wahyi huo. Katika upokezi huo hakuna kuzidisha wala kupunguza. Pamoja na kuwepo kwa madhehebu tofauti za waislamu, lakini hapana kutofautiana katika



ukweli na usahihi wa Qur'ani kama ilivyopokewa na aliye mtukufu wa daraja Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama.*

Kuhifadhi Qur'ani moyoni kulirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kuzingatia yale maandishi ya asili na matamko yake. Uandishi wake ulifanyika kwa umakini mno kwa usimamizi wa Mtume mwenyewe – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* kiasi kwamba hapakuzidishwa wala kupunguzwa hata herufi moja. Leo hii mtu anaweza kununua nakala ya Qur'ani nchini China, Afrika ya kati au mahali popote pale duniyani na kulinganisha nakala hizo na Qur'ani iliyoandikwa zaidi ya miaka elfu moja iliyopita, zilizo katika majumba ya makumbusho leo hii na asikute badiliko lolote katika maandishi hayo. Pamoja na kupita muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa lahaja mbali mbali za lugha ya Kiarabu. Kama mtu angelinganisha kisomo cha Qur'ani cha mtoto wa Kiindonesia leo hii na kile cha mwanazuoni aliyekuwa akiendesha masomo yake katika mji wa Makka miaka zaidi ya elfu moja iliyopita asingepata tofauti yeyote ile.

Na mna ndani ya Qur'ani changamoto, *"Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi."* (4:82)

Wala hapana la kushangaza kwani Yeye Allah-Mtukufu tayari Amekwishaahidi kuilinda, na katika Suurat Hijri Anasema; *"Hakika Sisi Ndio Tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi Ndio Tutaoulinda."* (15:9)

## Miujiza ya kilugha na maudhui zake

Kama mtu ataisoma Qur'ani kwa umakini bila shaka ataona kana kwamba Qur'ani inamsemesha yeye, tena si katika mtindo wa mjadala ila kwa namna ya kushangaza ya kutanguliza maelekezo yake kama vile inamsoma msomaji kabla ya yeye kujieleza na kumpa changamoto za kupanua elimu na maarifa yake.

Wachoraji wa picha kwa njia ya kushangaza wanaweza kuchora jicho na likaonekana kukufuata popote unapokwenda, lakini jambo kama hilo kutokea kwenye kitabu kuweza kufuata fikra za msomaji ni jambo la kustaajabisha zaidi. Qur'ani inajibu maswali ambayo bado hayajaulizwa pamoja na kuwepo kwa tofauti kati ya wasomaji, tamaduni zao na hali zao za kimaisha.

Qur'ani inamiliki njia katika uchambuzi wa tabia za wanadamu na uibuaji wa siri zao na ubainishaji wa udhaifu wao, na hilo huchagiza watu na kuzipa akili na nyoyo zao maswali ambayo mara nyingi huahirishwa au kukimbiwa majibu yake.

Mfano katika nukta hii ni pale mtu anaposoma Qur'ani na kukutana na visa vya watu katika nyumati zilizopita, wasifu wao, na adhabu zilizowapata wale waovu wao, na uokovu wa wale wema wao! Kupitia Qur'ani kwa mara ya kwanza mtu hujipima kwa kutazama matendo yake ni ya muelekeo upi na kulazimika kujihesabu na kujirekebisha mwenyewe. Na kwa hivyo kuifanya Qur'ani kuwa kioo cha nafsi, kwayo mtu hubaini ukweli wake, aibu na udhaifu wake na fursa zake katika kujenga maisha ya akhera na hapo nafsi ya msomaji huzama na kukiri kuwa yenyewe ni kutoka kwa Allah-Mtukufu, Mmoja tu Asiye na mshirika.

Hivyo utakuta inamkumbusha mtu wajibu wake na kurudia rudia ili asikate tamaa;

*"Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."* (39:53)

Wakati mtu anapokuwa katika hali ya wasiwasi na kubabaika kwa mgongano mkubwa ndani ya nafsi yake. Yeye hutafuta mahali pa kuegemea na kuelekea kwa shida zinazomkabili, hivyo hupata faraja. Katika Kauli Yake Allah-Mtukufu Anasema;

*"Na waja Wangu watakapo kuuliza khabari Zangu, waambie kuwa Mimi Nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka."* (2:186)

Na pale watu wanapofikiri kuwa maisha yao yamepoteza muelekeo hupata ponyo na usaidizi katika Kauli ya Allah-Mtukufu iliyo ndani ya Qur'ani;

*"Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo. Faida ya iliyo yachuma ni yake, na khasara ya iliyo yachuma ni juu yake pia. (Ombeni kwa kusema:) Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea. Mola wetu Mlezi! Usitubebeshe mzigo kama ulio wabebesha wale walio kuwa kabla yetu. Mola wetu Mlezi Usitutwike tusiyo yaweza, na Utusamehe, na Utughufirie, na Uturehemu. Wewe Ndiye Mlinzi wetu. Basi tupe ushindi tuwashinde kaumu ya makafiri."* (2:286)

Mwanahistoria maarufu Will Durant akiandika kuhusu ustaarabu katika kitabu chake 'The Story of Civilization' amethibitisha athari ya Qur'ani na hadhi yake miongoni mwa watu waadilifu kwa kusema;

"Wasomi wengi na wanafikra mahiri waliiamini Qur'ani katika karne zilizotangulia, na katika karne hii tunayoishi pia. Kama vile walivyoamini watu wenye hali na hadhi tofauti; na hilo ni kwa sababu imekuja na itikadi ya haki iliyo bayana yenye kukubalika kimantiki na wote. Qur'an ni nyepesi, isiyo na utata katika kuelewa mafunzo yake na iko mbali na kumfunga mtu kifikra, kimatendo na iliyo mbali kabisa na ushirikina na ibada za kikuhani. Uislamu unafundisha watu mbinu za kukabiliana na hali ngumu za kimaisha, na kuvumilia shida zake, bila ya malalamiko na kukatishwa tamaa."

> *Je, Durant anasema:*
>
> «Wasomi mbali mbali wenye Elimu na mawazo wameami Qur'ani pamoja na kutofautina kwa kiwango cha elimu zao mawazo yao,sijengine isipokuwa hii Qur'ani imekuja na itikadi ya ukweli iliyo wazi ambao watu wengi wameikubali itikadi nyepesi,isiyokuwa na siri nyingi.

Allah-Mtukufu Ameieleza Dini na Kuainisha ilivyo, hapana mkristo wala myahudi mwenye itikadi iliyo sahihi ambaye atazuwiwa nayo kuikubali Dini hii, "*Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Swala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao."* (2:177)



# Ni wapi Qur'ani imetoka?



Ni suala la kimantiki kabisa lile linalopita katika fikra za watu pale wanapozungumzia Kitabu kitukufu cha Waislamu, Qur'ani na Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama*, wakati mwingine wao huhoji kwa nini sisi tukubali maelezo ya Waislamu kuhusu chanzo chake? Je sisi hatupaswi kuuliza maswali kuhusu hilo?

Wanahistoria hawatofautiani kuwa Qur'ani imekuja katika ulimi wa Mwarabu, ambaye kabla ya hapo hakuwa anasoma maandishi wala kuandika. Alizaliwa Makka katika karne ya sita AD na jina lake ni Muhammad, mtoto wa Abdullah. Baadhi ya uthibitisho wa kihistoria tunaoupata katika vitabu mbali mbali vilivyopata kuandika historia yake haufanani na ushahidi mwingine uliyopo, kama vile sisi tunavyoona katika Kitabu hiki bayana kwamba Qur'ani si kazi ya mtu, bali ni maneno matukufu yaliyoletwa kwake kutoka kwa Allah-Mtukufu. Na kazi yake ilikuwa ni kufikisha ujumbe kama ulivyoletwa kwake na kuwabainishia watu yale ambayo Allah-Mtukufu Ametaka bila kuzidisha wala kupunguza.

Hivi inawezekana kwamba Mtume Muhammad – *Swalla Llaahu alayhi wasallama* alijitangaza mwenyewe tu kwamba yu Mjumbe wa Allah-Mtukufu, au amejifunza hayo aliyoyasema na kuyasogeza kwa watu baada ya hapo?

> Lau Mjumbe wa Uislamu angetaka kuwadanganya watu kwa ajili ya kutaka cheo kwa kudai kupata ufunuo kutoka kwa Mungu, basi ni kwanini hakudai kuwa maneo yake yote ni ufunuo kutoka Mungu?

Kwa hakika haya ni maswali yanayoruhusiwa, na huingia kwenye akili moja kwa moja kama mtu mwenyewe hajapata kuisoma Qur'ani au kuwa mwanazuoni mwenye kuifahamu historia ya Mtume Muhammad-Swalla Llaahu alayhi wasallama.

Ni kitu kinachofahamika na kuthibitishwa na tafiti nyingi za kihistoria kwamba baadhi ya wanafasihi na wanazuoni walikuwa wakichukua maarifa kutoka kwa wengine bila ya kukiri chanzo halisi, na kisha kunasibisha kazi hizo kuwa zao. Kwa nini mtu anasibishe kwa mwingine athari ya akili yake ni suala linalohitaji tafakuri ya kina!

Kinacholeta maswali yote haya ni kwamba kama yeye angekuwa na nia ya kulaghai na kujipatia utukufu kwa hila, basi bila shaka yeye angeinasibisha Qur'ani kwake, vinginevyo ni kwa nini basi adai kwamba maneno yake yote ni kutoka kwa Allah-Mtukufu?

Hivi inakubalika kimantiki kwamba yeye aandike kitabu na kisha akinasibishe kwa Allah-Mtukufu ili kupata nguvu na kunyanyua hadhi na nafasi yake katika jamii. Na ndani yake tukute maarifa yaliyoenea nyanja zote za maisha ya mwanaadamu na elimu nyingine ambazo wakati huo wala hazikuwa zikifikiriwa, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya kustawisha maisha ya kijamii yaliyotukuka?

Na katika Aya zake nyingine Qur'ani imetoa maelekezo ya moja kwa moja kwa Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kuhusu uhusiano wake wa kijamii na wa familia yake. Iikiwa ni pamoja na namna ya kuwalingania watu kunako Dini! Haijapata kutokea kwa mtu kuandika kitabu na kisha ndani yake ajipe maelekezo ya namna ya kushughulikia masuala ya kijamii yanayomkabili.

Katika maelekezo aliyopewa moja ni kuhusu lile tukio la yule kipofu miongoni mwa maswahaba zake ambaye alikwenda kwake akitaka kufundishwa Dini wakati Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akiwa

katika harakati za kumtosha lodi wa Kikuraishi kuhusu Uislamu. Wakati huo Mtume-*Swallallaahu alayhi wasallama* alikuwa na mmoja wa viongozi wakubwa wa Kikuraishi na yule swahaba kipofu hakujuwa kuwa Mtume alikuwa na jambo analofanya wakati huo na akamuita; "Ewe Mjumbe wa Allah-Mtukufu nifundishe na mimi kile ulichofundishwa na Allah-Mtukufu,' na kulisisitiza hilo mara nyingi. Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* akakunja uso, na akataka yule kipofu asubiri hadi atakapomaliza alichokuwa nacho, halafu alipomaliza akaondoka bila ya kujibu ombi la yule swahaba. Kama ilivyo kawaida ya Qur'an ililizungumzia tukio lile na kulitolea maelekezo, katika moja ya Sura zake kwa jina la tukio lile*; "Alikunja kipaji na akageuka. Kwa sababu alimjia kipofu! Na nini kitakujuulisha pengine yeye atatakasika? Au atawaidhika, na mawaidha yamfae? Ama ajionaye hana haja, Wewe ndio unamshughulikia? Na si juu yako kama hakutakasika. Ama anaye kujia kwa juhudi. Naye anaogopa. Ndio wewe unampuuza?"* (Q80:1-9)

Baada ya hapo kila pale Mjumbe wa Allah-Mtukufu-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alipomuona yule swahaba alikuwa akisema; "Karibu ee yule ambaye kwa sababu yake Mola wangu alinikosoa." Kisha yeye humtandikia nguo yake.

Huo ni ushahidi tosha kwamba yeye si mtunzi wa Qur'ani, ukiachilia mbali namna alivyoliwazwa pale alipotamani umteremkie yeye Wahyi ili apate kuthibitisha ukweli wake na nafasi yake na hivyo kujikosha kwa watu wake.

Tunapata uthibitisho wa historia katika sehemu nyingi namna gani ambavyo Mtume Muhammad alivyoishi katika hali ngumu akitamani Wahyi umshukie ili uthibitishe ukweli na nafasi yake; au umuokoe yeye, na uwasafishe watu watu wake; lakini haukuja...

Miongoni mwa hayo ni watu wake kumfanyia uadui na kumuudhi wakipata msaada kutoka kwa baadhi ya waliopewa elimu na umma zilizotangulia. Msaada wao wa kumpiga vita Muhammad.



Hivyo wakawaashiria wamuulize maswali matatu, akijibu maswali hayo basi yeye ni Nabii, na kama hakujibu basi yeye sie Nabii.. Hivyo wakafanya hivyo na kumuuliza na Mtume Muhammad akasema kama kuwapa changamoto kwao: Nitawajibu kesho...

Lakini hakuteremshiwa Wahyi kwa siku kadhaa na hivyo adui zake wakawa wanamjia mara kwa mara na kumfanyia stihzai kwa kukosekana yale majibu. Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama alipatwa na huzuni kwa sababu ya jambo lile. Na Wahyi haukuteremshwa kwake ila baada ya siku kumi na tano, ulikuja na majibu ya maswali waliyomuuliza na maelekezo mengine kwake; *Wala usisema kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho. Isipo kuwa kwa kusema 'Mwenyezi Mungu Akipenda'. Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unapo sahau, na sema: Asaa Mola wangu Mlezi Ataniongoa kwenye uwongozi ulio karibu zaidi kuliko huu*. (Q18:23-24)

Kana kwamba akiambiwa katu usiseme kwa hakika mimi nitafanya jambo fulani kesho, isipokuwa baada ya kuliunganisha hilo na uwezo wa Allah-Mtukufu, na hivyo useme; InshaAllah! Na hilo ndiyo ilikuwa sababu ya kuchelewa kwa yale majibu kama funzo kutoka kwa Allah-Mtukufu kwake.

## Tuhuma mbali mbali.

Kwa hakika tunaweza kusema kwamba maisha ya Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kabla na baada ya kupewa Utume yalikuwa ishara tosha ya ukweli wake kwamba ni Mjumbe wa Allah-Mtukufu.

Ni vipi basi, mtu ambayo hakuwa anajua kusoma kabla ya kuteremshiwa Qur'ani wala hakuwa anaandika, katika jamii ya watu ambao hawakupata kuteremshiwa kitabu kutoka mbinguni. Aliokuwa akishirikiana nao katika maisha ya kila siku na kuhudhuria vikao vya kijamii katika mambo yasiyohusisha maovu. Aliyekuwa akijishughulika katika kutafuta riziki yake na ya familia yake. Aliyepata kuchunga wanyama kwa ujira, ambaye hakupata kuwa na uhusiano wowote na wanazuoni. Ambaye ameishi miongoni mwao kwa zaidi ya miaka arobaini ya uhai wake. Ghafla tu aliweza kuzungumza nao bila ya ahadi na kuwafahamisha wao yale ambayo hawakuwa wanayajuwa kutoka kwa baba zao. Na akawasimulia pia visa vya watu waliyopita, historia ya uumbaji, maisha ya manabii waliotangulia na sheria mbali mbali za hukumu katika nyanja zote za maisha?

Ukweli huo uliwakaa vibaya wale waliomfanyia uadui Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* miongoni mwa ndugu na jamaa zake, ambao walipata mshtuko mkubwa kwa lile alilokuja nalo, na wakaanza kutafuta tuhuma ambayo ingeweza kuwafanyia watu kuwa mbali naye?

Kwanza waliwaza kwamba haitaleta maana kudai kwamba Qur'ani ni simulizi kutoka kwake mwenyewe, kwa kuwa haitakubalika akilini hasa pale mtu atakapoisoma Qur'ani na kuizingatia. Hasa maudhui zake katika taaluma mbali mbali, maarifa na dua ambazo ni katika elimu aliyoipata kutoka nje ya mazingira aliyokuwa akiishi, na mazingira hayo yanajulikana. Hivyo baadhi yao wakadai kwamba Muhammad, kama walivyokuwa wakimwita, anasimulia ndoto anazoota, wengine wakadai kuwa ni mchawi, wengine mshairi na wengine wakaleta madai ambayo hayaafikiani kabisa na maudhui ya mafunzo yake, kwamba ni mwenda wazimu!

Kihistoria hayo yote ni katika muendelezo wa aina ya tuhuma ambazo alituhumiwa kwazo Nabii Musa-*Alayhi salaam*, za uchawi, Nabii Isa-*Alayhi salaam* kwa uwazimu?

Na hivi ndivyo ilivyokuwa kwa manabii wengine waliyomtangulia! Pale adui zao walipoona mafanikio wanayopata katika jamii zao, na kimsingi hayo huwa madai ya watu wasio na hoja katika kile wanachong'ang'ania kuamini isipokuwa matakwa yao ya ovyo!

## Kwa nini Tusione Hilo kuwa ni Uwezo Mkubwa wa kiakili:




Watu wote wanakubaliana kwamba Allah-Mtukufu Amewapa baadhi ya watu akili na maarifa ya kuweza kugundua yale ambayo ni vigumu kufikiriwa na watu wa kawaida, kwa kuwa ni jambo linalojulikana kwamba hata akili nayo ina mipaka katika kuwaza na kutoka na kitu? Pamoja na kuwa akili inakiri kuwepo kwa Muumba Mwenye Uwezo usiomithilika na kwamba uadilifu Wake unahitaji kuwepo na maisha mengine baada ya haya ili kila mmoja wetu akapate malipo yake stahiki kwa mujibu wa matendo yake, iwe ni yale ya heri ama yale ya shari. Swali linabaki kuwa! Hivi ni lazima akili ithibitishe kila kitu hata yale mambo yanayotakiwa kuthibitishwa na roho kama vile uwepo wa Mungu, yaani Allah-Mtukufu, Pepo kwa ajili ya watendao mema, na Moto kwa ajili ya watendao mabaya?

Kama mtu ataisoma Qur'ani kwa kuzingatia maudhui zake ataona kwamba inatupa sisi maelezo ya kina juu ya imani, na pia maelezo ya kina namna Allah-Mtukufu Alivyoanzisha uumbaji na vipi uhai utakwisha, na hutupa sisi wasifu wa Pepo na neema zake na Moto na adhabu zake na idadi ya milango yake. Majina ya baadhi ya malaika waliopewa majukumu mbali mbali, na hutuelezea pia kadhia za msingi za ukweli wa ulimwengu pamoja na mwanadamu, basi, ni kwa nadharia tete ipi Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* aliweza kujenga hayo maelezo yote kwayo?

Hayo hayapatikani kwa uwezo wa kiakili, kwani kimantiki ni lazima jambo liwe aidha kweli au uwongo, batili au la kubuni. Ni elimu ambayo haipatikani kwa kusoma na kusomeshwa na wanaadamu.

Ijapokuwa katika elimu za kibinadamu baadhi ya hakika hizo zimethibitishwa kutotofautiana na maarifa yenyewe, kama ambavyo yameafikiana yale yaliyo katika hicho Kitabu cha mbinguni na matukio ya kweli katika historia ya mwanaadamu na hali halisi za kijiografia zilizothibitishwa kisayansi miongoni mwa habari za ghaibu.

## Je inawezekana Qurani ikawa ni kutokana na vitabu vilivyoitangulia?



Hebu na tujiulize na kutafakari kidogo, hivi inawezekana maarifa yale akawa ameyachukua kutoka katika vitabu vya manabii waliyotangulia?

Tukiachana na fikra kuwa Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* hakuwa anajuwa kusoma na kwamba Waarabu wa wakati wake wengi hawakuwa wanajua kusoma wala kuandika, na ukweli kwamba Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* hakupata kusuhubiana na yeyote katika wanazuoni wa

kiyahudi, yaani watu wa kitabu hapo kabla na kwamba ukweli wa kihistoria unathibitisha kuwa wanazuoni wa kiyahudi, walikuwa wakificha elimu hizo ili kulinda uongozi na maslahi yao ya kiduniya,

Ni ukweli uliyo wazi kwamba Qur'ani haiafikiani na kila kilichokuja katika vitabu vya mbinguni wakati ule, bali imeteremshwa ili kuja kusahihisha baadhi ya mambo yaliyopotoshwa na kufichwa na wanazuoni wa kiyahudi. Kukamilisha upungufu katika baadhi ya sharia na simulizi, kudhihirisha elimu iliyokuwa inafichwa, kubainisha upotofu wa imani zao na kuwatakasa baadhi ya manabii na maadili mabaya ambayo baadhi ya wanazuoni wa kiyahudi waliyanasibisha nao. Hivi kwa mifano hii, mtu anaweza kudai kwamba yeye-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* alikuwa mwanafunzi wao, au inaweza ikawa kwamba alipata elimu na maarifa hayo kutoka kwao?

## Ukweli wa kihistoria.

Utafiti unathibitisha kwamba Mtume Muhammad - *Swalla llaahu alayhi wasallama* alikuwa Mwarabu wa kabila tukufu la Kikuraishi aliyezaliwa Makka na wazazi kutoka koo za watukufu wa Kikuraishi?

Na ni ukweli wa kihistoria pia kwamba moja ya fani kubwa iliyokuwa chini ya milki ya Waarabu wakati huo ni ufasaha na umbuji katika lugha yao. Walikuwa mahiri mno katika fasihi na katika utungaji, uandishi na usomaji wa mashairi. Walikuwa wakikusanyika katika mikutano na mabaraza na hafla mbali mbali na kila kabila lilisifu hadhi na mazuri ya kabila lake kwa mashari yaliyosomwa kwa ufasaha mkubwa.

Vitabu vya historia vinatufahamisha kwamba hapana mtu aliyepata kusoma shairi ila waliomfuata baadaye na kumkamilishia upungufu wake na kumuonyesha kilichompita na wengine kumpa changamoto kwa mashauri yao, na hii ndiyo ilikuwa ada na nguvu yao na kupambazukiwa kwao.

Iweje basi, ajitokeze mtu ambaye wao walimuona kuwa ni adui wa maslahi yao, ambaye kwake hawakuacha fursa yoyote ya kumpiga vita ipite.Yeye kuwapa wao changamoto ya kuleta mfano mdogo tu wa iliyo Qur'ani, walau Sura moja tu fupi katika Sura zake na wasifanye hivyo!

Kwani yeye alipowapa changamoto hiyo hakujuwa kwamba ataamsha ari katika stadi maalumu ya umbuji wa lugha waliokuwa nao na hivyo kuwafanyia wao kuingia kwa nguvu katika mashindano kwa mtu mmoja mmoja au hata kwa makundi ili angalau wadhihrishe moja ya hoja za kumpinga kwao!

Na kisha awaambie kabla kwamba katu hawataweza juu ya yeye kutambua uwezo mkubwa waliyonao, na vipi ashikilie tena kwamba hata vizazi vijavyo hadi siku ya Kiyama havitaweza kuleta mfano wake hata kama watakusanyika watu wote ili kusaidiana katika jambo hilo!

Kwa hakika hilo si jambo la kawaida na halisogelei ila mtu mwenye moyo uliyojaa imani na yakini ya kile inachokijuwa na jambo li vivyo hivyo mpaka leo hii. Makuraishi, kupitia wale mbuji na weledi katika lugha yao hawakuweza kabisa kutunga mfano wa iliyo Qur'ani na wakafedheheka na kuwa kichekesho kwa wapambe wao.

## Suratul Faatiha

Ni sura kubwa zaidi katika qur`an na muislamu anaikariri daima katika swaka yake na maana yake kwa mukhtasari ni kama ifwatavyo:

| | Maana ya suratul Fatiha |
|---|---|
| Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu | Na anza kwa Tadhima na adabu jina Mwenyezi Mungu msifika kwa rehema nyingi ambazo rehma zake zimeenea kila kitu. |
| Sifa njema zote ni za Mwenyeezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote | Namsifu Mwenyezi Mungu kwa sifa zake zote na kwa vitendo vyake na kwa neema zake zilizodhahiri na za siri, pamoja na kumenda na kumtukuza, yeye ndie Muumba mmiliki mwenye uwezo wakuzisurufu na kunemesha viumbe vyote ulimwenguni. |
| Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu | Anaesifika kwa sifa zote zenye maana zote za juruma na hali zake na maeneo yake, yeye ndie mwenye ruhuma ilioenea kwa viumbe vyake, wote hapa ulimwenguni , na Mwenye kuwarehemu waja wake hasa waumini siku ya Kiyama. |
| Mwenye kumiliki siku ya malipo | Mwenye kumiliki na kusurufu siku ya malipo na hesabu. |
| Wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada | Sisi tunakuabudu wewe peke ewe mola wetu kwa ibaada, hatukushirikishi pamoja na wewe yoyote katika ibada ya aina yoyote ile, na tunakuomba wewe msaada peke yako katika mambo yetu yote, wewe ndiwe mkili wa mambo yote na hakuna yoyote anaemiliki mfano wa mdudu chungu. |
| Tuongoe njia iliyonyooka | Ewe mola wetu tuelekeze na utuongoze na utafikie njia iliyonyooka, na utudumishe mpaka siku ya kukutana na wewe. |
| Njia ya ulio waneemesha | Njia ya watu ulio waneemesha kwa kuwaongoza na kuwapa misimamo kutoka na manabii na watu wema ambao walitambua haki na kuifuata. |
| Siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea | Na utuweke mbali na utuepushe njia ya uliowakasirikia na kuwachukia ,kwa sababu yakuitambua haki lakini hawakuifuata,na njia ya watu aliopotea kwa sababu ya ujinga wao na kutofanya bidii ya kuitafuta haki. |
| Amiin | Ewe mola itikia |

## Kila mmoja na neno lake.

Baada ya yote hayo likabaki neno la mwisho kwa kila mmoja kutoa hukumu kwa Qur'ani na msimamo wake kutokana na uzoefu wake, katika kusoma kwake na kufahamu kwa mazingatio pamoja na kuchagua tafsiri kwa mnasaba wa lugha yake kama hajui Kiarabu.

Mna katika Qur'ani tukufu dalili nyingi kuhusu ukweli wa Utume wa Nabii Muhammad-*Swalla Llaahu alayh wasallama* ambao tunaupata kupitia nyoyo na akili zetu kwa kuona hali halisi na matokeo baada ya kuisoma na kuzingatia kwetu maana ya Qur'ani. Allah-Mtukufu Anasema; *"Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanacho somewa? Hakika katika hayo zipo rehema na mawaidha kwa watu wanao amini."* (29:51)

Ni bora basi watu wakaisoma Qur'ani kwa mazingatio, na kwamba hapana mwenye kuacha hayo ila yule aliye na makufuli yake katika moyo na akili yake; *"Je! Hawaizingatii hii Qur'ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?"* (Q47:24)





# Nini maana ya ibada mbali mbali katika Uislamu?



Hivi ni kweli kwamba Allah-Mtukufu Anahitaji ibada zetu?

Allah-Mtukufu Hahitajii ibada zetu wala matendo yetu. Kufanikiwa na kuokoka katika Uislamu hakutegemei tu matendo ya kiibada pamoja na kutoa mali, lakini ile hali ya usafi wa nia na muelekeo wako kwa Allah-Mtukufu na kumuamini Yeye. Hivyo basi, kinachopaswa kufanywa ni kutafsiri mafunzo kwa vitendo katika maisha ya kila siku na tabia iakisi hilo na kufanya kazi kwa masilahi ya watu na kuharakia katika mambo ya kuleta maendeleo katika jamii.


Ndani ya Qurani Allah-Mtukufu Anasema; *"Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kuruzuku, Mwenye Nguvu, Madhubuti."* (51:56-58)

Na pale watu walipopata utata na kuuliza waelekee upande gani wakati wa ile Swala, na hilo ni kwa sababu katika Uislamu watu wote duniyani huelekea Al-Kaaba iliyo Makka wakati wa Swala zao. Qur'ani ikaleta majibu kwamba ukweli wa imani ya mtu, usafi wa nia na matendo mema ya kuwanufaisha wanadamu ndio jambo la msingi zaidi na si upande tu wa kuelekea wakati wa Swala, iwe ni magharibi au mashariki, Allah-Mtukufu Anasema;

*"Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Swala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida na dhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao."* (2:177)

Qur'ani inatuhakikishia tena kwa mara nyingine kwamba mwenye kujitahidi kufanya ibada na kuwa mtu mwema mwenye kuifuata Dini, basi hilo ni kwa manufaa yake na uokovu wake mwenyewe. Na ama yule mwenye kukataa basi, naye ni kwa hasara yake mwenyewe, kwa kuwa Allah-Mtukufu ni Mwenye Kujitosheleza kama Anavyosema;

*"Na anaye fanya juhudi basi bila ya shaka anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake. Hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji wa walimwengu."* (29:6)




Baadi ya watu walipo changanikiwa na wakauliza ni upi mwelekeo sahihi wa kibla wakati wa Swala, walihakikishiwa kwamba uhakika wa dini ni katika ukweli wa kuamini na kutenda amali njema na kunufaisha watu, wala sio mujardi wakuelekea Mashariki au Magharibi.

## Nguzo za Uislamu

Zenyewe ni ibada maalumu zilizoamrishwa katika Uislamu kama ifuatavyo;




Imani na kukiri hakika ya uja wa mtu kwa Allah-Mtukufu na kumfuata Mtume Wake Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama*, na hilo ni kwa kutamka shahada, yaani kushuhudia kwamba hapana muabudiwa wa haki ila Allah-Mtukufu na kwamba Mtume Muhammad- *Swallallaahu alayhi wasallama* ni Mjumbe Wake. (Angalia ukurasa 32)




Kuswali Swala tano zile zilizoamrishwa. (Angalia ukurasa 100)




Kutoa Zaka kwa wale wanaostahiki, yaani kwa kuwa na mali zilizofika kiwango cha kutolewa Zaka. (Angalia ukurasa 104)




Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani. (Angalia ukurasa 106)




Kwenda kuhiji nyumba ya Allah-Mtukufu iliyo Makka kwa wenye uwezo, yaani wa mali na afya njema. (Angalia ukurasa 108)

## Kwa nini majukumu hayo?

Hata kwa muweko tofauti, swali linaweza kuwa; Ni kwa nini sasa Allah-Mtukufu Ametuumba sisi, Ametupa kinywa, ulimi pamoja na tumbo ili tupate kula, kisha Anatuambia sisi: "Fungeni?" Na kwa nini basi Akatuumbia sisi vitu vizuri na kutupa sisi matamanio, kisha Anatuambia; 'Jizuieni na inamisheni macho yenu!' Na wengine huenda mbali zaidi na kuthubutu kusema; Kwa nini Ametupa sisi nguvu halafu Anatuzuwiya sisi kuzitumia tunavyotaka!

Kwa mafunzo ya Uislamu, jambo hili lipo wazi, Allah-Mtukufu Ametupa sisi uwezo na nguvu ya kujizuwiya na si kwamba Yeye Ndiye Anayetuzuia sisi. Allah-Mtukufu Amekupa farasi ili upande akupeleke unakotaka na si farasi akuendeshe wewe. Miili yetu na nguvu zetu ndiyo farasi wetu vyote vimeumbwa kwa ajili yetu ili tuvitumie kwa wakati muwafaka, sehemu muwafaka na kwa njia iliyo sahihi na si kinyume chake.

Hivyo basi, kwa nafasi ya mwanaadamu, uwezo wa juu anaotakiwa kuwa nao ni ule wa kuweza kudhibiti na kuzuwiya matamanio yake kuvuka mpaka. Na kuyaelekeza matamanio yale katika mambo yaliyo na manufaa ya kweli kwake. Na kwa hilo Allah-Mtukufu Amempambanua mwanadamu toka wanyama wengine na Akampa yeye nafasi ya uchaguzi, na kwa hilo ndio Allah-Mtukufu Ametuumba.

Kama ilivyokuja katika Qur'ani;

*"Hakika Sisi Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyo changanyika, Tumfanyie mtihani. Kwa hivyo Tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona. Hakika Sisi Tumembainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru."* (76:2-3)

Kwa hivyo kila linalomsibu mwanadamu katika majanga na taabu nyingine si vinginevyo ila ni mitihani tu kwetu ili sisi tupate kuendeleza hali zetu za kiroho, kimaadili na kiimani, na hivyo tujifunze subira katika maisha, kama ilivyokuja katika Qur'ani: *"Hapana shaka Tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri, Wale ambao ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake Yeye hakika tutarejea."* (2:155-156)

Kumbe maisha haya ya dunia ni nafasi kwetu ya kujiletea maendeleo na kuzipima imani na maadili yetu. Allah-Mtukufu Anatufunza sisi kwa kurudia rudia ili tupate kujisahihisha na kufuata uongofu kwa ustawi wetu na ili tuweze pia kutubia Kwake kila pale tunapoteleza na kufanya makosa, Mtume Muhammad-Swalla Llaahu alayhi wasallama amesema;

*"Kama hamfanyi dhambi, Allah-Mtukufu Atawaondoa nyinyi wote, kisha Ataleta watu ambao watafanya dhambi na halafu kuomba msamaha Kwake na Yeye Atawasamehe."* (Imamu Muslim 2749)



> Heshima ya mwanadamu na ubora wake ni pale atakapo weza kujizuia na matamanio,na kuziongoza matamani ya nasfi na hawaa zake katika kuzipeleka kwenye Manufaa yake.

# Swala ya Kiislamu

Huenda umepata kujiuliza kuhusu ukweli wa jambo hilo pale unapoona mandhari ya kustaajabisha wakati Waislamu wanapomsemesha na kumuomba Mola wao kupitia ibada hiyo ya Swala kwa kusimama, kurukuu na kusujudu kwa pamoja kana kwamba wameachana kabisa na dunia ile inayowazunguka.

## Swala ya Waislamu iko vipi?

Swala imechukua nafasi kubwa katika Uislamu kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kujipendekeza kwa Allah-Mtukufu na kumuomba na kunyenyekea Kwake, kama Alivyomwambia Nabii Wake-*Swalla Llaahu alayhi wasallama*; *"Nawe sujudu na ujongee!"* (96:19)

Mtume- *Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano; Kushuhudia kuwa hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah-Mtukufu na ya kuwa Muhammad-Swalla Llaahu alayhi wasallama ni Mjumbe Wake, na kusimamisha Swala."* (Imamu Bukhari 8)

Muislamu hulipwa thawabu kwa Swala zake kwa kadiri ya unyenyekevu wake ndanimwo na usafi wa moyo wake kwayo. Swala ni njia moja ya kusadikisha imani na uchaji Mungu wa mtu na ni kitulizo pia cha nafsi za watu na kwa hilo ndiyo Swala ikawa moja ya starehe kubwa za Mtume wetu Muhammad-Swalla Llaahu alayhi wasallama.

Qur'an inatutaka tustawishe Swala, na si kuswali tu kimazoea, kwani ustawishaji Swala wa kweli unahusisha roho, viungo, akili na hisiamoyo kwa pamoja. Na kwamba pale sisi tutakapofanya hivyo ndiyo Swala zetu zitakuwa heri yenye kuweza kutuhamasisha katika kufanya mambo mengine mema na kuwa mbali na maovu. Hivyo basi kule kumtaja Allah-Mtukufu kunakofanyika ndani ya Swala ni katika mambo makubwa kabisa anayofanya yule mtu.

Katika Kumhimiza Mtume Wake Allah-Mtukufu Anasema; *"Soma uliyo funuliwa katika Kitabu, na ushike Swala. Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu Anayajua mnayo yatenda."* (29:45)

Ama yule anayedhania kwamba Swala ni mazoezi tu ya viungo, yanayotanguliwa na kunawa au kukoga, huyo atakuwa amepitwa mbali na yale mengine muhimu katika harakati za Swala, kama kusimama, kurukuu na kusujudu, kwa kuwa hayo yote ni matendo ya kumtukuzu Allah-Mtukufu. Na ndiyo maana tamko la kuianza Swala huwa; "Allahu Akbar' yaani Allah ni Mkubwa.

Baada ya hapo anayeswali huinama (yaani hurukuu) kwa unyenyekevu mbele ya Allah-Mtukufu, huku akikiri udhaifu wake na kusema; 'Subhaana Rabil 'Adhwim' yaani Ametakasika Allah-Mtukufu. Baada ya hapo husujudu akitaraji kuwa karibu zaidi na Mola wake huku akiomba kujibiwa maombi yake. Huweka paji lake chini na kusema; 'Subhaana Rabi' Aala,' Ametakasika Allah - Mtukufu Aliye juu kabisa! Kisha humuomba Mola wake na kuendelea hivyo mpaka anapoikamilisha Swala yake! Izingatiwe kwamba wakati wa kuswali ni wakati ulio na thamani mno wa kujitosheleza mtu, ambapo yeye huwasiliana na Mola wake, Aliye sababu ya uwepo wake hapa duniyani.



"Swala ilikuwa ndio sehemu ambayo Mtume rehma na Amani zimfikie yeye akipa ladha kubwa humo.



Masjilu haram ndio Msikiti wenye heshima kubwa kwa Waislamu na humo kuna Al Kaaba ilio jengwa na Nabii Ibrahim nalo nijengo lenye pembe nne waislamu wamearisha popote pale walipo kuelekea huo katika Swala zao. Pamoja na kuamini kuwa hiyo al kaaba haidhurishi wala hainufaishi.

Allah-Mtukufu Amewajibisha kwa Waislamu Swala tano za kila siku, ambapo inafaa kuzitekeleza mahali popote pale palipo twahara kwa jamaa, pamoja na hayo watu wamehimizwa kuswalia Misikitini ili kupatikane uhusiano mzuri kati ya Waislamu, na hivyo kujenga mshikamano imara wa kuweza kusaidiana kati yao.

Kama ambavyo Uislamu umehamasisha watu kujitahidi kufanya ibada za ziada kama Swala na Swaumu za sunna, pale muislamu anapokuwa na muda na uchangamfu wa kutosha kuweza kufanya hivyo.

Waislamu huswali wakiwa wameelekea upande wa al-Kaaba katika mji wa Makka, magharibi mwa bara Arabu kutoka mahali walipo. Jengo lililojengwa na Nabii Ibrahim - *Alayhi salaam*, aliye baba wa Manabii - Allah Mtukufu Awarehemu wao wote, ambao wengi wao walipata kuhiji hapo. Waislamu wote wanajuwa kwamba katika al-Kaaba pana jiwe jeusi ambalo halina manufaa wala madhara kama lilivyo, lakini kwa Hekima Yake Allah-Mtukufu Ameamrisha kuelekea huko katika Swala zao.

## Adhana

Ni tangazo la kuingia kwa wakati wa Swala kwa waislamu na hivyo kuwakumbusha na kuwaita wao Misikitini kwa ajili ya Swala husika.

Na ni aina ya utajo wa Allah-Mtukufu na kumtukuza, na matamko yake ni kama yafuatayo;

1. Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar
2. Ashhadu An-Laailaha Illa Llaah, Ashhadu An-Laailaha Illa Llaah.
3. Ashhadu Anna Muhammadan Rasuulul Llah, Ashhadu Anna Muhammadan Rasuulul Llah
4. Hayya 'ala Swalat, Hayya 'ala Swalat
5. Hayya 'alal Falaah, Hayya 'alal Falaah
6. Allahu Akbar, Allahu Akbar
7. Laa ilaha Illa Llah



## Zaka

Wanazuoni wanakubaliana juu ya faida kubwa inayopatikana katika jamii ya Waislamu kwa watu kutoa Zaka. Moja ya faida hizo ni kupunguza idadi ya fukara ndani ya jamii. Lakini faida nyingine ni kupunguza ukubwa wa ufa kati ya matajiri na masikini, ili kuikinga jamii kutumbikia katika maovu, machafu na uharibifu.

Mifumo tofauti ya kiuchumi, falsafa zake na sheria mbali mbali zinatungwa katika jitihada za kushughulikia tatizo la kuzidi kupanuka kwa ufa kati ya masikini na matajiri bila ya mafanikio makubwa. Ni kwa namna gani Uislamu uliweza kulishughulikia tatizo hilo na kuliondoa kabisa?

Allah-Mtukufu Amewajibisha waislamu kutoa Zaka kila mwaka, asilimia 2.5 ya mali za ziada wanazomiliki baada ya kutoa matumizi yao binafsi, ili mali hiyo itumike katika kuwawezesha baadhi ya masikini ndani ya jamii kuondokana na hali hiyo kila mwaka na kulifanya hilo kuwa nguzo ya tatu ya Dini ya Kiislamu.

Zaka si suala la tajiri kumfadhili masikini, bali ni suala la haki za masikini kuchukuliwa kutoka katika mali za wenye uwezo na matajiri. Zaka imekusudiwa kuchukua haki za masikini zilizo mikononi mwa matajiri bila ya wao kuomba au kudhalilishwa katika jitihada za kujikwamua kwao kutoka katika hali ngumu zinazowakabili kwa zamu.

Kiasi kidogo kinachotolewa, hutolewa kama wajibu kwa mwenye uwezo na tajiri Muislamu, ama kiwango cha utoaji katika sadaka ni uwanja mpana na watu hushindana katika hilo. Matokeo ya utoaji huo huonekana wazi katika jamii na katika maisha yao, mali na furaha ndani ya jamii huongezeka na huko akhera mtoaji atakwenda kupata malipo mara mbili.



> Zaka sio ufadhili kutoka kwa tajiri kwenda kwa maskini, bali ni haki ya maskini inachukuliwa kutoka katika mali ya tajiri, na inamfikia mwenye haja bila ya yeye kuomba, au kumdhalilisha utukufu wake.

Qur'ani imelileta jambo hilo katika taswira mbali mbali kwa watoaji wa mali kwa kutafuta radhi ya Allah-Mtukufu, *"Mfano wa wanao tumia mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mwenye Kujua."* (2:261)

Qur'ani inaendelea kutujulisha kwamba kutoa mali kwa mwenye kuhitaji ni katika kuitakasa nafsi, na Allah-Mtukufu Anasema Akimwambia Mtume Wake;

*"Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo...."* (9:103)

Na kuhusu watu wasiopenda kutoa katika misingi ya nidhamu ya Dini ya Allah-Mtukufu Qur'ani imeweka wazi kuwa wao ndiyo wa kwanza watakaopata hasara; kwa sababu ni wenye kuzifanyia ubakhili nafasi zao na kuwapelekea kukosa mafanikio ya kidunia na akhera.

Imekuja katika Qur'aan: *"Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubakhili. Na anaye fanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi."* (Muhammad:38)

Inajulikana kwamba kwa kutekeleza nguzo hii kubwa miongoni mwa nguzo za Uislamu kwa ukamilifu wake, bila shaka mpango wa kuboresha maisha ya jamii ungefanikiwa. Hivyo basi, utoaji wa Zaka kwa wanaostahiki husaidia kuondoa tabia ya ulimbikizaji mali wa kundi fulani tu katika jamii. Katika historia ya Uislamu imepata kutokea Zaka ikazunguuka kutafuta wenye kustahiki.

Faida nyingine ya kijamii inayopatikana katika utoaji wa Zaka ni kule kujenga uhusiano mzuri kati ya wanajamii. Kwa kuwa ni kawaida kwa mtu kumpenda yule anayemfanyia wema. Na matokeo yake ni kwamba jamii ya Waislamu itaishi katika hali ya kupendana na matukio ya wizi, ujambazi na utapeli katika jamii kupungua.

> Inawafananisha Qur'ani wale wanaotoa mali zao kwa ajili ya kumrisha Mwenyezi Mungu ni mfano ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba Katika kila shuke zimo punje mia zimezidi mara mia saba.



# Swaumu

Kila mtu anampenda mtu na kumhusudu yule mwenye uwezo wa kujizuwiya. Yule anayeweza kujizuwiya chakula, au aina za vyakula, mwenye kulinda afya yake na kuchunga uzito wake kwa kufuata maelekezo ya kitabibu. Na hilo huchukuliwa kama jambo kubwa kwa mtu kwa kuwa udhibiti wa matamanio kwa lengo la kufanikisha jambo kubwa zaidi ni katika mambo ya kuazimiwa.

Kwa kufunga Muislamu anatengeneza kikubwa kuliko hicho cha kujizuwiya kula na mambo mengine yanayokatazwa kisheria. Mtu anapokuwa katika Swaumu, anakuwa ni mwenye kujizowesha tabia ya kiasi, uvumilivu na subira inayoambatana na kufuata maelekezo ya Muumba wake.

Na kufunga ni nguzo ya nne katika nguzo za uislamu , basi Uislamu unamlazimisha mwenye uwezo afunge na ajizuie na yanayofuturisha , nayo ni : chakula na kinywaji na mtu kufanya tendo la ndoa na mkewe kutoka kuingia al fajiri mpaka kuzama kwa jua , kila siku katika mwezi wa ramadhan , nao ni mwezi wa tisa katika kalenda ya kiislamu.

Qur'ani inatujulisha kwamba funga iliamrishwa pia kwa nyumati zilizotutangulia. Japo iwe ni kwa utaratibu uliyo tofauti na wa kwetu. Makusudio yake ni mamoja, yaani kupata kuwa wacha Mungu.

Katika Qurani Allah-Mtukufu Anasema; *"Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu."* (2:183)

Pale Muislamu anapodhibiti matamanio yake yale ya halali kwa saa kadhaa kila siku kwa idadi ya siku maalum, hapo yeye anakuwa mtawala wa nafsi yake. Mwenye uwezo wa kuimiliki, na kuizuwiya kuangukia katika mambo yaliyokatazwa katika maisha yake. Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amehadharisha kwamba mtu ambaye hatabadilika na kufuata maadili mazuri baada ya Swaumu atakuwa miongoni mwa wale ambao hawakufaidika na Swaumu zao. Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema: *"Yule ambaye hatoacha kusema uongo, basi Allah-Mtukufu hana haja ya mtu huyo kuacha chakula chake na kinywaji chake."* (Imamu Bukhari 1804)

Katika Swaumu, njaa ya aliyefunga na kiu yake huwa ni mafunzo kwake na msukumo wa yeye kuwasaidia watu wasiojiweza, wenye shida ya kupata chakula na maji pamoja na jitahada zao.

> Anatanabahisha Mtume wa Uislamu kwamba Mtu asiebadilika na kutengenea tabia zake baada ya kufunga kwake basi mtu huyo hakufaidika na saumu yake.



"Uislamu unapo mlazimisha muislamu kufunga,huwa unamtaka kwa funga yake awakumbe mafakiri wenye njaa na haja yao juu ya chakula.

# Hijja

Takriban dini zote ulimwenguni huwa na safari za kidini ambapo wafuasi wa dini hizo hudhihirisha ibada na unyenyekevu wao kwa Mungu wanayemuabudu. Katika aina hizo za safari, safari ya Hijja katika Uislamu ndiyo inayoongozwa kwa kuhusisha watu wengi zaidi duniyani pale wanapokusanyika kila mwaka katika mji mtukufu wa Makka.

**Ni nini nafasi ya Hijja katika Uislamu?**

Hijja ni nguzo ya tano katika nguzo za Uislamu, wajibu ni mara moja tu katika uhai wa Muislamu mwenye afya njema na uwezo wa mali.



Ni safari tukufu ambapo tabaka za watu na utaifa wao, mali, utajiri na kabila vyote hutoweka, wote huvaa nguo za aina moja, rangi moja na kuitikia wito mmoja na hujisalimisha kikamilifu katika uhusiano wa mja na Mola wake kwa wote kwa pamoja kuitika; *"Labaika Allahumma Labaika, Labaika La sharika Laka labaika, Innal hamdu waniimata laka walmulku la sharika laka"* yaani "Kwa kuitikia wito wako ee Mola wangu nasubiria jibu Lako, ee Mola wetu tumekuja Kwako na sisi tunaitika kwa ndimi zetu na tunakiri kwa nyoyo zetu kuwa Wewe ni wa Pekee Unayestahiki kuabudiwa kwa haki, na Wewe Ndiye Unaestahiki kuhimidiwa na kushukuriwa, Wewe ni Muumba na Mwenye kuneemesha na Wewe ni Mfalme usiye na mshirika!"

Hivyo basi Hijja ni safari ya kuthibitisha imani. Safari ambayo ndani yake Muislamu huwa katika hali mbali mbali za matendo na kauli. Katika hali zote hizo lengo ni kupata radhi ya Allah-Mtukufu na kumuabudu Yeye, na kudhihirisha uhitaji wa neema Zake. Huku akiomba msamaha na malipo ya thawabu kutoka kwa Allah-Mtukufu. Mtume Muhammad-*Swallallaahu alayhi wasallama* amesema: *"Kwa hakika kutufu na kufanya Sai (kati ya mlima Safwa na Marwa) katika Hijja ni kutukuza utajo wa Allah-Mtukufu."* (Ibn Abi Shaybah 15334)



Vazi la aliekusudia kwenda Makka kwa ajili ya kufanya hijja baada ya kuvua ngo zake za kawaida na kuvaa shuka mbili ni tangazo la unyenyekevu wake kwa Mwenyezi Mungu na kuwa yuko sawa na kila aliekuja kuhiji.



# Familia katika Uislamu

# Familia

Familia nyingi siku hizi zimegeuka kuwa makundi tu ya watu wenye kuishi katika nyumba moja wenye funguo tofauti.


Siku hizi watu wengi wanakimbia majukumu yao ya kweli kwa wake na watoto wao. Ni kikwazo gani kinachowakataza wao kupata ladha ya kuhudumia familia zao ni suala linalo hitaji mjadala wa kina?

Na muelekeo huo umeshika kasi katika karne hii ingawaje mabadiliko yalianza kujitokeza tangu mwanzo wa karne ya kumi na tisa katika baadhi ya tamaduni za watu katika historia. Na chanzo ni ubinafsi uliokithiri, uchoyo, roho mbaya mambo ambayo kila siku matokeo yake huwa mabaya kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii kwa ujumla wake.

Hivyo kutokea mwanzo Uislamu umekuwa ukihimiza mshikamano wa kifamilia. Haki zake mbali mbali na majukumu yake kwa wote wanaohusika. Kwa kuwa nyumba na familia katika Uislamu ni kituo cha malezi na mafunzo ya kidini, na hivyo kustawi kwake ndio kustawi kwa jamii yote.

**Hayo yanadhihiri katika hukumu mbali mbali ambazo hazihesabiki idadi yake, baadhi yake ni:**

**1**



## Ndoa na malezi ya familia katika Uislamu.

- Uislamu umeichukua ndoa na malezi ya familia kuwa moja kati ya matendo mazuri ya manabii waliotangulia. Na pale baadhi ya wafuasi wa Mtume-*Swallallaahu alayhi wasallama* walipotaka kujitenga na ndoa ili wapate muda wa kufanya ibada zaidi za kuswali na kufunga, Mtume-Swallallaahu alayhi wasallama aliwaambia wao; *"Hata mimi hufunga na kufungua, ninaswali na wakati mwingine ninalala, na ninaoa wanawake, asiyetaka mfumo wa maisha yangu yeye si miongoni mwetu"* (Imamu Bukhari 4776)
- Wakati Qur'ani inapozungumza kuhusu neema mbali mbali na Aya mbali mbali kuhusu mwanaadamu, mwanzo inataja namna Allah-Mtukufu Alivyojaalia utulivu, mapenzi na huruma vipatikane kwa mume na mke kuowana, kama ilivyokuja katika Qur'ani: *"Na katika Ishara zake ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu...."* (30:21)
- Uislamu umeamrisha kurahisisha masuala ya ndoa, na ukatoa ahadi kumsaidia yule anayetaka kuowa, kama alivyosema Mtume-*Swallallaahu alayhi wasallama*; *"Watatu Allah-Mtukufu ana haki ya Kuwasaidia, miongoni mwao akataja, 'Muoaji anayetaka kujisitiri"* (Imamu Tirmdhi: 1655)

- Na Uislamu unawataka vijana waliokwisha baleghe, wenye afya nzuri kuoa mapema ili wapate ule utulivu wa kinafsi na suluhisho la kisheria juu ya nguvu za matamanio walizonazo.



> Qur'an inpozungumzia kuhusu neema na ishara juu ya mwanaadamu inataja katika vilivyopewa kipao mbele katika hayo na yale aliyoyaumba ALLAH katika utulivu na mapenzi na huruma baina ya mtu na mkewe.

## 2

### Uislamu umempa kila mtu katika familia heshima yake awe ni mwanaume au mwanamke.

Uislamu umempa baba na mama majukumu makubwa katika malezi ya watoto wao. Mtume Muhammad-*Swallallaahu alayhi wasallama* amesema; *"Kila mmoja wenu ni mchunga na kila mmoja ataulizwa kwa kile alichokichunga, Imamu ni mchunga na ni mwenye kuulizwa kuhusu raia wake, mwanaume ni mchunga wa familia yake nae ataulizwa kwa alichokichunga, mwanamke ni mchunga wa nyumba ya mume wake, nae ataulizwa kwa alichokichunga, na mfanyakazi ni mchunga wa mali ya aliyekuwa juu yake nae ataulizwa kwa alichokichunga"* (Imamu Bukhari 853)



## 3

### Uislamu umeweka mkazo katika kuwaheshimu na kuwajali wazazi wote wawili wa kiume na kike katika uhai wao wote.

Kwa vyovyote atakavyokuwa kijana wa kiume au wa kike, yeye anatakiwa kuwaheshimu wazazi wake na kuwafanyia wema. Na hilo limeunganishwa na ibada anazofanya, na amekatazwa kuchupa mpaka kwa kauli au matendo yake, katika mahusiano yake na wazazi wake, kwa namna yoyote ile hata kwa kudhihirisha tu neno au sauti ya kuonyesha kukerwa. Katika Qur'ani Allah-Mtukufu Anasema; *"Na Mola wako Mlezi Ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa hishima."* (17:23)



> Uislamu umekataza mtoto kuvuka mipaka kwa maneno au kwa vitendo wakati wakuamiliana na wazazi wake, hata kama ni kuwambia neon dogo mno lenye kuwaudhi na kuwakasirisha.

## 4

### Amri ya kulinda haki za watoto wa kiume na wa kike na kufanya uadilifu katika kuwahudumia:

Mtume Muhammad-*Swallallaahu alayhi wasallama* amesema; *"Inatosha kwa mtu kuwa muovu kwa kutowahudumia anaotakiwa kuwalisha" (Imamu Abu Daud 1692). Na akasema tena kuhusu malezi na kuwahudumia hususan watoto wa kike: "Yule atakayekuwa katika mtihani kwa wasichana hawa, kisha akawafanyia wema, basi watakuwa kwake stara dhidi ya moto"* (Imamu Bukhari 5649)

## 5

### Uislamu umeamrisha kutembeleana na kuunga udugu.

Maana yake ni ule uhusiano mzuri kati ya mtu na nduguze na kuwasiliana na kutembeleana. Na jambo hilo limetajwa kuwa ni miongoni mwa mambo makubwa yanayomsogeza mtu kunako uchamungu. Na akatahadharisha na jambo la kukata udugu, kwa kufanyiana vibaya, na jambo hilo likahesabiwa kuwa ni katika madhambi makubwa. Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema*; "Hatoingia peponi mtu akatae udugu"* (Imamu Muslim 2556)



# Nafasi ya mwanamke katika Uislamu



Mtu unapotazama matangazo mbali mbali katika televisheni au mabango yanayotangaza biashara majiani au katika majalada ya majarida tofauti utaona ukubwa wa jinai inayofanywa na ustarabu wa kileo dhidi ya wanawake. Ambapo katika hali zote mwanamke huonekana kama bidhaa au kichocheo cha kuamsha hisia za ngono.

Na kwa hilo jamii yetu tunayodai kwamba ni ya kisasa haina tofauti kubwa na jamii katika zama za ujima. Kwa kumdhalilisha na kumtweza mwanamke pale walipomfanya kuwa ni kitu tu kinachoweza kurithiwa au kununuliwa. Hata katika harakati hizi zinazoendelea katika kujaribu kumkomboa mwanamke bado hali inazidi kuwa ya kutisha zaidi kwao kwa kuwa hapana dhamira ya kweli ya kuwakomboa.

Uislamu ndiyo Dini pekee iliyoleta mapinduzi ya kweli dhidi ya unyanyasaji, dhuluma na udhalilishaji mbaya dhidi ya wanawake. Uislamu umeweka sheria na taratibu mbali mbali kwa lengo la kulinda haki na hadhi yake, ili aweze kuishi maisha yenye heshima yatakayomuwezesha kutekeleza majukumu yake katika maisha kwa ukamilifu zaidi.

Na kwa kuonyesha umuhimu wao ndani ya jamii, moja ya Sura ndefu zaidi katika Qur'ani imeitwa kwa jina lao; 'An-Nisaa' (yaani wanawake) na katika Sura hiyo mmetajwa hukumu mbali mbali kuhusu wanawake. Katika kuwatukuza wanawake Allah-Mtukufu Hakuishia hapo, kwani ipo na Sura nyingine iliyo na jina la mmoja kati ya wanawake waliyo watukufu, Suuratul Mariyamu, ikimzungumzia kwa urefu mama wa Nabii wa Allah-Mtukufu, Isa mwana wa Mariyamu.

Uislamu ndiyo uliobadili mtazamo uliokuwepo zama hizo, yaani miaka zaidi ya 1400 nyuma na mpaka leo hii kuhusu hadhi na heshima ya wanawake ili wapate kuishi kama Alivyowaumba wao Allah-Mtukufu na sio kama bidhaa. Kwa kuwa wao ni washirika wa mwanaume katika maisha yake yote na si mshirika wa usiku mmoja tu.

Katika wakati ambapo baadhi ya watu, wenye fikra finyu, hasa katika nchi za magharibi wanautuhumu Uislamu kwa kumkandamiza mwanamke tunaona zaidi ya asilimia 75 ya watu wanaoingia katika dini ya Kiislamu katika nchi kama Uingereza ni wanawake, na wanaingia kwa wingi baada ya kuusoma Uislamu na kutambua ukweli kwamba ndiyo Dini inayowapa hadhi inayostahili na kwamba ndiyo Dini iliyoweka mkazo katika Ustawishaji wa familia kwa maana yake halisi, kama maneno ya Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama yanavyobainisha;

Kwanza mwanamke amepewa haki ya kuchagua mume anayemtaka, na amepewa majukumu makubwa ya kulea watoto. Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Na mwanamke ni mchunga katika nyumba ya mume wake na ataulizwa kuhusu kile alichokichunga."* (Imamu Bukhari)

Uislamu umekuja kubadilisha muono wa watu kuhusu mwanamke ili awe kama alivyomuumba Mola wake na sio kama bidhaa. Awe ni mshirika wa maisha yake wala sio mshirika wa usiku mmoja tu, ahusike katika utulivu, mapenzi na sio matamanio peke yake.

> Uislamu umebakiza jina la mwanamke na utukufu wa nasaba ya baba yake. Hivyo haujabadilisha nasaba ya mwanamke baada ya kuolewa kwake, lakini umemwachia haki yake ya msingi kabisa ya kujinasibisha na baba yake na familia yake.



### Mfano wa Sheria mbali mbali zinazohusiana na kumuheshimu mwanamke ni hizi zifuatayo:

- Mwanamke amepewa haki ya kuchagua mume, na akapewa majukumu makubwa ya kulea watoto. Mtume Muhammad Swalla Llahu Alayhi wasallam, amesema: *"Na mwanamke ni mchunga katika nyumba ya mume wake na mwenye kuulizwa katika kuchunga kwake."* (Al-Bukhari 853)
- Uislamu umebakiza jina lake na utukufu wa nasaba ya baba yake. Hivyo haujabadilisha nasaba yake baada ya ndoa, bali ataendelea kujinasibisha na baba yake na familia yake.
- Uislamu umeweka sawa kati ya mwanamke na mwanamume katika chumo la matendo yao mema na katika tangamano kati yao na wanaume kiasi cha Mtume-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* kusema: *"Wanawake ni ndugu za wanaume"* (Imamu Abu Daud 236)
- Uislamu umemwajibisha mtu kumhudumia mwanamke, iwe mwanamke huyo ni mke wake, mama, dada au binti yake.
- Uislamu umempa mwanamke haki ya kurithi katika mgawanyo mtukufu kwa uadilifu. Kuna baadhi ya sehemu ni sawa na mwanaume na sehemu zingine zinazidi na zingine kupungua kulingana na ukaribu na majukumu ya kutoa yanayomzunguuka. Ufinyu wa fikra za watu wengi umefanya baadhi yao kutupa lawama kwa mgawo wa mwanaume kupata mara mbili ya mwanamke katika mirathi, bila ya kutazama mgawanyo wa majukumu ambayo Allah-Mtukufu amewajibisha kwa mwanaume kama vile kumkimu mwanamke katika mahitahi yake.
- Uislamu umethibitisha utukufu wa mwanamke kwa kueleza wazi kuwa kumhudumia mwanamke aliye dhaifu kuna malipo makubwa mbele ya Allah-Mtukufu, hata kama huduma hiyo itatolewa na mtu asiye ndugu wa huyo mwanamke. Jambo hilo linahesabiwa miongoni mwa matendo bora mbele ya Allah-Mtukufu. Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema, *"Mwenye kuwashughulikia wajane na masikini, malipo yake ni sawa na mtu aliyepigana jihadi katika nidhamu ya Dini ya Allah-Mtukufu na pia ni kama yule anayesimama usiku kuswali na hachoki kusimama au mfungaji asiyeacha kufunga"* (Imamu Bukhari 5661)

> Uislamu umempatia mwanamke haki yake katika mirathi na kumgawia fungu la uadilifu, sehemu nyingine anarithi sawa na mwanamume na sehemu nyingine wanatofautiana kwa kuzidi au kupungua.

## Namna Uislamu ulivyomtukuza mwanamke:

**Kuhusu Mama:** Inasimuliwa kwamba mtu mmoja alikwenda kwa Mtume-*Swalla llaahu alayhi wasallama* na kumuuliza; *"Ewe Mjumbe wa Allah-Mtukufu ni nani mwenye haki zaidi kwangu ya kumfanyia wema?" Mtume-Swallallaahu alayhi wasallama akasema: 'Mama yako,' kisha akauliza tena, 'halafu nani?' Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama akasema; 'Mama yako' Akauliza tena, 'kisha nani?' Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama akajibu; 'Mama yako' kisha akauliza tena, 'halafu nani?' Mtume-Swalla llaahu alayhi wasallama akamjibu; 'Baba yako'* (Imamu Bukhari 5626)

**Binti:** Mtume Muhammad-*Swalla Llaahu alayhi wasallama* amesema; *"Mwenye wasichana watatu akawasubiria, akawalisha, akawanywesha na kuwavisha, watakuwa kwake kinga dhidi ya moto siku ya Kiyama."* (Ibn Majah 3669)

**Mke:** Mtume Muhammad-*Swalla llaahu alayhi wasallama* amesema: *"Mbora wenu nyinyi ni yule aliye mbora wenu kwa mke wake na mimi ni mbora wenu kwa wake zangu."* (Imamu Tirmidhi 3895)



Mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke katika uislamu ni mahusiano ya kukamilishana sio ya ugomvi , basi kila mmoja wao anaziba mapungufu ya mwenzake katika kujenga jamii ya kiislamu.

## Hakuna mgogoro wa kijinsia katika Uislamu:

Katika Uislamu hakuna mgogoro kati ya jinsia mbili, kwani hakuna maana yoyote ya watu kushindana katika mali za duniya. Katika Uislamu hakuna kampeni za wanaume dhidi ya wanawake wala za wanawake dhidi ya wanaume kwa kuwa Uislamu umekwisha mpa kila mmoja wao haki yake kwa mujibu wa maumbile yake.

Ni jambo la kushangaza, inakuwaje mtu aupige vita upande wake wa pili na kupambana na ndugu yake, kama anavyosema Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama kwamba wanawake ni ndugu za wanaume, na huku uhusiano kati yao ni wa kukamilishana, kwa kuwa kila mmoja hukamilisha upungufu wa mwenzake katika kuijenga jamii ya waislamu.

Qu'rani inatupigia mfano wa ukamilifu wa taswira hii pale Allah-Mtukufu Anaposema; "*...Wao ni stara kwenu nyinyi na nyinyi ni stara kwao...*" (Q2:187)

Kile ambacho mtu anaweza kukiona kuwa ni upungufu na udhaifu wa mwanamke ni nguvu ambazo mwanaume hana na ujenzi wa familia bora ni wenye kuhitajia vyote hivyo viwili. Na kinachoonekana katika upungufu wa mwanaume huenda ikawa ni aina ya hali ambazo hazimfai mwanamke, lakini maisha hayawezi kwenda bila ya hali hizo.

Hivyo si kwa mchezo ndiyo Allah-Mtukufu Amewaumba wanadamu katika jozi. Na si wanadamu tu Yeye Anatueleza sisi kwamba Ameumba kila kitu katika jozi, halafu baadhi ya watu husema; "Inapaswa kwa aina hizo mbili kufanana kwa kila kitu," hilo ni jambo lisilo wezekana.



Wakati baadhi ya wanaume walipotamani haki walizopewa wanawake Qur'ani ikawaambia; *"Wala msitamani Alicho wafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wana fungu katika walio vichuma, na wanawake wana fungu katika walio vichuma. Na muombeni Mwenyezi Mungu Fadhila Zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."* (4:32).

Hapo utaona kwamba kila mmoja ana nafasi na wadhifa wake uliotukuka. Kila mmoja anasimama kwenye nafasi aliyopewa akitafuta fadhila na radhi ya Allah-Mtukufu. Sheria haikuteremka kwa ajili ya wanaume au kwa ajili ya wanawake tu, imeteremshwa kwa wanadamu wote ili wapate kutangamana kwa wema.

## Uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke katika Uislmu

Tokea hapo kabla kulikuwa na rai na jitihada mbali mbali katika kuratibu uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke kwa mipaka ya kikanuni, desturi na maadili. Elimu inayohusiana na kumjuwa mwanaadamu, yaani – Anthropology-inatujulisha kwamba wapo watu wasioona haya au tabu kukaa uchi mbele za watu na kufanya watakavyo katika fujo za jimai na kadhalika. Na baadhi katika tamaduni za kale walikuwa wakiwafunga wanawake kwa minyororo ya chuma kwa kuwahofu, na katika baadhi ya tamaduni hivi leo, mwanamme ndie mwenye kustahili kuvaa kwa stara kuliko mwanamke, na yapo mengi mfano wa hayo yasiyo na hesabu.

Ndiyo watu, hasa wale waliostaarabika, wakaona haja ya kuwepo kwa miongozo na mifumo itakayofuatwa kwa lengo la kuzuwiya maisha ya wanadamu kugeuzwa na kutolewa maana na hivyo kufanya kusiwepo na tofauti kati yao na wanyama.

## Tabia ya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamme katika Uislamu:

Taratibu za uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume katika Uislamu si jitihada za mwanadamu zinazotokana na historia na jiografia, lakini ni utaratibu wenye kufaa katika kila zama na mahali, ambao Allah-Mtukufu Ameuteremsha ndani ya Qur'ani na Akamfundisha Mtume-Swalla Llaahu alayhi wasallama na yeye akawafundisha watu.

Taratibu za uhusiano huo hutofautiana kulingana na nafasi ya mwanaume na nafasi ya mwanamke kama inavyodhihirishwa kama inavyoelezwa katika Uislamu.

## Wanaume wanaohusiana na wanawake katika Uislamu wanagawanyika katika mafungu yafuatayo;

**1. Mwanaume aliye mume wa mtu;**

Hakuna mfano uliyo toshelezi kama ule wasifu ambao Qur'ani imeuleta, Allah-Mtukufu Amemuita mume kuwa ni stara kwa mke, na mke ni stara kwa mume. Ni wasifu wenye kufaa katika mawasiliano ya kinafsi, kihisia na kimwili kati yao. (Q2:187)

**2. Mwanaume aliye maharimu wa mtu;**

Makusudio ya maharimu ni yule mwanaume ambaye katu hawezi kumuowa mwanamke kwa sababu ya udugu uliyopo kati yao. Maharimu wapo aina kumi na tatu kwa upande wa wanaume; Kama vile baba, babu, mtoto, ndugu, baba mdogo, mjomba, mtoto wa kaka, mtoto wa dada, mjukuu wa kike au wa kiume, na mfano wa hao. Kwa watu hawa mwanamke anaruhusiwa kuonekana kwao bila ya hijabu kamili, yaani katika hali ya kawaida.

**3. Mwanaume aliye mgeni (Ajnabi):**

Huyu ni mwanaume ambaye si ndugu wa mwanamke.

Uislamu umeweka mipaka na kanuni kadhaa za kuratibu uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume ambaye si ndugu. Lengo ni kulinda heshima ya mwanamke na kufunga milango ya ushawishi wa shetani kwa mwanadamu. Allah-Mtukufu Ndiye Mwenye Kujuwa yalipo maslahi ya wanadamu kama ilivyokuja ndani ya Qur'ani: *"Hivi, Asijue Yule Ambaye Ameumba na huku Yeye daima Ndiye Mwenye udiriki wa ndani kabisa usiyomithilika katika Kujua Kwake, Aliye Muelewa-yote?"* (Q67:14)

### Kwa nini sheria ya Hijabu kwa ajili ya Kujihifadhi dhidi ya Wanaume?

- Ili mwanamke aweze kutekeleza majukumu yake ya kijamii katika maisha kwa njia nzuri huku akilinda hadhi na heshima yake.
- Kupunguza uwezekano wa kuchochea hisia za ngono ili kuilinda jamii kwa upande mmoja na kulinda haiba ya mwanamke kwa upande mwingine.
- Kuwapa amani wale wanaume wamtazame mwanamke kwa heshima na kumuona kuwa ni mtu aliyestarabika na si bidhaa ya kutosheleza ashki zao.

## Kinachotakiwa katika uhusiano huo:

**1. Kuinamisha macho:**

Allah-Mtukufu Amewaamrisha wanawake na wanaume wote kuinamisha macho yao kwa kutotazama vyenye kuchochea hisia za ngono kwa kujistiri vyema ili kulinda heshima zao. Kutazama kusiko na mipaka ni moja ya njia za kukaribia maovu, kama Alivyosema katika Qur'ani;

*"Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari za wanayo yafanya. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao..."* (24:30-31)

**2. Kuhusiana kwa heshima na tabia njema.**

Mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke kazini au kwenye kutafuta elimu au katika sehemu zingine zisizokuwa hizo, yanatakiwa kuchunga heshima ya kila mmoja wao na kujiepusha na kila kinachoweza kuchochea matamanio kwa njia yoyote ile.


**3. Hijabu.**

Allah-Mtukufu Ameamrisha Hijabu, yaani nguo ya stara kwa wanawake na si kwa wanaume. Na sababu ni ule uzuri ambao Yeye Amempamba kwao yule mwanamke na ambao humshughulisha yule mwanaume. Upo ushahidi wa kihistoria kutoka mwanzo huko hadi leo hii kuonyesha kwamba mwanamke ndiyo hutumiwa kuamsha hisia za wanaume na si kinyume chake.

Mipaka ya Hijabu kwa mwanamke ni yeye kujifunika mwili wake wote isipokuwa uso wake na viganja vyake kwa mwanamume asiyekuwa ndugu, kama Qur'ani ilivyoamrisha; *"..wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa ule unao dhihirika..."* (24:31)



> Wengi wanaoukosoa Uislamu kuhusu Hijabu wameghafilika na sura halisi ya haiba ya mwanamke katika historia nzima ya mwanaadamu. Inashangaza kwamba hawazingatii kwa kuona kuwa hata picha za Bikira Maria wanazochonga humuonyesha yeye akiwa kavaa Hijabu.



# Kanuni kuhusu vyakula na vinywaji



Watu wengi huwa wanahoji kwa nini Uislamu umeharamisha pombe na nguruwe?

Majibu ni kama ifuatavyo,

Qur'ani imewaruhusu Waislamu kunufaika na vyote vilivyo katika ardhi kama lilivyokuja andiko kuhusu jambo hilo; "*Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi...*" (2:29)

Kati ya hivyo ni vyakula na vinywaji, vyote ni halali isipokuwa vile vilivyotajwa kuwa ni haramu katika Qur'ani kutokana na uchafu na madhara yake kiafya;

## Nguruwe:

Qur'ani imemharamisha nguruwe moja kwa moja, pamoja na kuwa nguruwe hakufahamika kwa Waarabu wakati huo. Na wanaokosoa jambo hilo hawazingatii kwamba nguruwe hakuharamishwa kwa Waislamu peke yao. Hata kwa wayahudi nguruwe ni haramu. Lipo andiko katika agano la kale na lipo andiko katika agano jipya pia kwa Wakristo, japokuwa baadaye andiko hilo liliondolewa. (Angalia Marko 5:11-13. Mathayo 67. Na barua ya Peter 2: 22 na Luka 15: 11)

Kwani kuna ubaya gani kwa Allah-Mtukufu Kutukataza sisi kula baadhi ya vyakula baada ya Kuturuhusu kula vingi katikavyo. Ili Apate kupima imani zetu na utiifu wetu Kwake, kama vile Alivyompa mtihani Nabii Adam-*Alayhi salaam* baada ya Kumruhusu kula vyakula vizuri peponi na kumkataza ule mti?



## Pombe na madawa ya kulevya:


Kuharamishwa kwa pombe kumekuja kama jumla ya katazo la kujiepusha na maradhi na mambo yote yanayoangamiza maisha ya watu. Ni jukumu la mamlaka husika mahali popote pale kuweka kanuni na taratibu mbali mbali ili kulinda afya za jamii na maisha yao. Bila ya hivyo ni matatizo na uharibifu kwa jamii nzima! Na hivyo ndivyo Alivyofanya Allah-Mtukufu kwa maslahi yetu.

Katika utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniyani (WHO) huko Oxford na kuchapishwa katika jarida linaloitwa 'Nature' toleo namba 483 la tarehe 15 March 2012 na taarifa ya (WHO) ya tarehe 11.2.2012 inaonyeshwa kwamba waathirika kwa matumizi ya pombe katika mwaka huo walikuwa zaidi ya waathirika wote wa Ukimwi, Malaria na Kifua kikuu kwa pamoja. Na ni mara tatu ya waathirika wa vita vyote, mauaji ya kimbari, na ugaidi kwa mwaka huo.




Katika utafiti na taarifa hizo za (WHO) inaonyeshwa kwamba;

Zaidi ya watu milioni moja na nusu hufa kila mwaka kwa sababu ya pombe na madawa ya kulevya. Miongoni mwao ni vijana 320,000 wenye umri kati ya miaka 15-29 ambao hufa kila mwaka kwa sababu zenye uhusiano na pombe, asilimia 9 ya vifo vya umri huo husajiliwa kila mwaka.




Huko Marekani tafiti zimedhihirisha kuwa wanafunzi laki saba kila mwaka hushambuliwa na kuuwawa na wanafunzi wenzao na sababu kuu iliyotajwa ni matumizi ya mihadarati, ikiwemo pombe.







Tafiti za mwaka 2001 zinaonyesha kuwa asilimia 80 ya matumizi ya nguvu na ujambazi unaofanywa na vijana wa Astonia, una uhusiano na unywaji wa pombe.




Robo ya mauaji yote ulimwenguni yanatokana na matumizi ya mihadarati, ikiwemo pombe.




Ripoti zote za Shirika la Afya Duniyani (WHO) zinahimiza na kuzitaka nchi zote kuweka sheria kali ambazo zitapunguza matendo ya kijinai yanayohusishwa na unywaji wa pombe.



## Qur'ani imeharamisha pombe.



Allah-Mtukufu kupitia Qur'ani Alikwishabainisha madhara ya pombe kwa jamii. Kwa kuwa Yeye Ndiye Mwenye Kujuwa lile linalomfaa binadamu katika maisha na jamii yake.

Uislamu uliwafikia kwanza Waarabu, watu ambao kwao ulevi ilikuwa ni sifa katika jamii, wakiogelea kwao. Walikuwa wakijisifu kwa ulevi uliopindukia na wakitumia mali nyingi kwa ajili yake.

Qur'ani ikawakataza kwa kuwabainishia kwamba madhara yake ni makubwa mno katika jamii kuliko manufaa yake. Kwa kuwa mnywaji hupata ladha na burudani ya muda mfupi, lakini athari yake kiafya na hata kijamii ni ya muda mrefu. Na tiba yake ni ngumu inayochukua muda mrefu kwa mtu binafsi na hata jamii kwa ujumla, kama inavyobainishwa ndani ya Qur'ani: *"Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo zipo dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake."* (2:219)

Pombe ni katika matendo ya shetani ambayo husababisha bughudha na uadui na kuzuwiya watu kumtaja Allah-Mtukufu. Wakati ilipoteremshwa Aya hiyo Waislamu waliulizwa; 'Je mmeacha' wakajibu: 'Ndio tumeacha,' na wakamwaga pombe yote iliyokuwepo katika mji wa Madina wakati ule kwa kutekeleza amri ya Allah-Mtukufu katika Qur'ani.

## Katika mwaka mmoja huko Uingereza:

- Watu wanaokaribia milioni moja na nusu walikufa kwa sababu zinazohusiana na unywaji wa pombe.
- Hali milioni saba zimerokodiwa katika hospitali kwa gharama ya Pound Sterling za Uingereza 650 Milioni zinazotokana na pombe.
- Gharama zote zinazohusiana na matumizi ya nguvu kwa walipa kodi ni kati ya paundi 8-13 Milioni kila mwaka.





# MAKOSA NA TOBA




Ni jambo linalozingatiwa kwamba falsafa ya kupatia na kukosea ni moja kati ya changamoto kubwa za kifikra katika dini na itikadi nyingi, na zinatofautiana itikadi hizo katika hilo katika njia za kushughulika na kosa, dhambi, toba na majuto.

## Uislamu

Uislamu unaitazama tabia ya binadamu kwa kina ile ambayo Allah Mtukufu Amemuumba kwayo na Akaweka ndani yake mvuto wa kheri na shari. Binadamu hachukuliwi kama malaika ambao wameumbwa kutii amri za Allah Mtukufu tu. Uislamu unakiri kuwa kila binadamu ni mkosefu, lakini kwa upande mwingine unam-bebesha uwajibikaji kutokana na maamuzi yake na chaguzi zake. Na hapa ndipo inapokuja falsafa ya Kiislamu kuhusu makosa na toba, ambayo inawezekana kuifupisha katika yafuatayo:

- Cha mwanzo tunachokuta katika Qur’ani ni kwamba kosa ni kitu pekee na toba ni kitu pekee katika taswira iliyo wazi na nyepesi isiyo na utata ndani yake wala kificho. Hakuna kosa lililofaradhishwa juu ya binadamu kabla ya kuzaliwa kwake, bali kila mtu huzaliwa akiwa mnyofu, hazaliwi na dhambi yoyote iliyopita. Na hakuna mtu mwenye haki ya kusamehe na kufuta dhambi, na kwamba kosa la Nabii Adamu - Alayhi salaam ni kosa la kibinadamu alilokosea mwenyewe na alijitakasa nalo kwa njia ya toba ya moja kwa moja kwa Allah Mtukufu kwa njia nyepesi . Na kwa hivyo kosa la kila mtoto miongoni mwa watoto wake ni kosa la mhusika. Na Njia ya kutubia iko wazi katika mtazamo wa uadilifu na iliyo wazi katika kumfanya kila mtu ajitahidi kutokata tamaa na rehema ya Allah Mtukufu, na ni njia inayom-bebesha kila mtu mzigo wake, kama ilivyo katu habebeshwi mtu yeyote kosa la mtu mwingine. Na hayo ndiyo mafunzo waliyoleta Mitume na Manabii kutoka kwa Allah Mtukufu kama Qur’ani inavyotuarifu; *"Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa? Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi? Ya kwamba hakika nafsi iliyobeba madhambi haibebi madhambi ya mwengine? Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyafanya mwenyewe? Na kwamba vitendo vyake vitaonekana? Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu."* (Q53:36-41)



- Toba ni moja kati ya ibada kubwa na ni njia ya kujipendekeza kwa Allah Mtukufu, haihusiani na yeyote ila muhusika nayo, na wala haihitaji sehemu maalumu wala kukiri mbele ya mtu yeyote au kupata idhini yake. Bali hiyo ni ibada kati ya Allah Mtukufu na waja Wake. Katika majina ya Allah Mtukufu na Sifa Zake yaliyotajwa ndani ya Qur’ani ni (Msamehevu, Mwenye Huruma, Mwenye Kusamehe dhambi, mwenye Kukubali toba). Hapa Qur’ani inatuhesabia sifa za wachamungu ambao wataingia Peponi, inathibitisha kuingia kwao katika baadhi ya dhambi, lakini baada ya kufanya dhambi wanaharakisha kufanya toba na kuomba msamaha: *"Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamwomba msamaha kwa dhambi zao - na nani anayefuta*


*dhambi isipo kuwa Mwenyezi Mungu? - na wala hawaendelei na waliyoyafanya na hali wanajua."* (Q3:135).

Toba katika Uislamu haihitaji zaidi ya kuacha dhambi, yaani matendo yaliyokatazwa kwa mujibu wa Sharia. Na kujuta kutokana na matendo yake yaliyopita na kuazimia kutoyarejea tena. Pamoja na kurejesha haki kwa wenyewe ikiwa zipo. Na kama itatokea yeye kurejea kwenye kosa lake tena toba ya kwanza haitofutwa na wala makosa yake hayatarejeshwa, itakuwa amefanya dhambi mpya na ni juu yake kutubia tena.


Hivi ndivyo anavyoishi mtu katika Uislamu kwenye hali ya uwiano kati ya kujitahidi kufikia lengo, kupanda daraja, kuwa mbali na makosa na kuzingatia hulka ya binadamu ambayo mara nyingi humpandisha na kumshusha na hivyo kuweza kupondoka katika mwelekeo wake. Na ni wajibu wake katika hali ya nashati na uchaji wake, au uzembe na kupondoka kwake asikose mfungamano, bali aelekee kwa Allah Mtukufu na atubie Kwake na kuomba msamaha.

Na hapa ndipo ilipo tofauti kati ya watu wema na wengineo, kama Qur'ani inavyothibitisha pale inapotuarifu kuwa hakika tofauti ipo pale wachamungu wanapoingia katika makosa hukumbuka na kutubia kwa Allah Mtukufu, tofauti na wale wanaong'ang'ana kwenye makosa bila ya kuzinduka au kuonyeka.

"*Wale wamchao Mungu, zinapo wagusa pepesi za Shet'ani, mara huzindukana na hapo huwa wenye kuiona haki. Na ndugu zao wanawavutia kwenye upotofu, kisha wao hawaachi."* Q7:201-202)



Katika Uislam Hakuna dhambi iliyowekwa kwa mwanadamu kabla ya kuzaliwa kwake, lakini kila mwanadamu anazaliwa msafi habebi dhambi yoyote ya awali.



# UWILI WA AKILI NA DINI



Baadhi

Baadhi ya watu, wale wenye fikra finyu, hudhani kwamba Dini ni yenye kupingana na Akili. Kwa sababu dini kwa mtazamo wao ni chimbuko na taswira za hovyo, simulizi za watu wa kale na fikra potofu. Na ambapo kwao elimu na falsafa ni njia mbili za kupata maarifa yaliyopangika kwa kukamilika masharti ya utafiti, fikra na majaribio. Itikadi hii tunapo izingatia ina baadhi ya ukweli na sehemu kubwa ni makosa.

Ukweli ni kwamba kuna dini kadhaa ambazo huchukua akili na wakati mwingine zinapingana nayo. Vyanzo vyake na vitabu vyake vimejaa simulizi na itikadi potofu zilizo kinyume ambazo zinapingana na Elimu na Ulimwengu




Ama makosa ni kutoa hukumu ya kijumla kuhusu dini zote bila ya kuzingatia aina na tofauti zilizopo kati yake kwa kuzingatia chanzo chake, mafunzo yake na athari zake kihistoria.

Kama mtu ataitazama Qur'ani Tukufu,chanzo cha Uislamu, Kitabu kinachofunza Uislamu atatambua bila shaka yoyote kwamba Kitabu hicho kimeitukuza na kuipa hadhi akili ya binadamu kwa kiwango ambacho hapana dini iliyokwisha kifikia. Wala hahitaji mwenye kuisoma Qur'ani kufanya uchunguzi wa kina ili kutambua kwamba inahimiza tafakuri na uchunguzi kiasi cha kuichagiza kwa kuhoji zaidi ya mara kumi na tatu; *"Hivi hamna akili?"*

> Mwenye kuisoma Qur'ani hahitaji kuwa ni mjuzi sana wakufahamu ilia pate kujua kuwa Qur'ani inamlingani kuwa ni mwenye kutafakari na kutamali

**Yanadhihiri maelekezo ya Qur'ani katika kuifanyisha kazi akili kupitia hoja mbali mbali, miongoni mwazo ni kama ifuatavyo:**

**1**



Qur'ani inamsemesha mwanadamu mwenye akili razini, iliyo huru na kila aina ya ukandamizaji, kiburi, hofu na ujinga. Inajulisha juu ya wajibu wa kumwamini Allah Mtukufu kupitia dalili za kiakili na ushahidi wa kimantiki, na katika hayo ni Kauli Yake Allah - Subhaanahu wa taala;

"Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini." (Q52:35-36)

**2**



Qur'ani inajadili dalili za wapinzani na inakataa maneno yasiyo na dalili wala hoja kama inavyotoa changamoto; "Na pale wao wanapoambiwa: "*Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli."* (Q2:111)

**3**



Inawapa sifa mbaya wale wasiozitumikisha akili zao vyema na kuwataja kama watu wasio na milango ya fahamu. Kwa kule kutofaidika kwao na yale wanayoona na kusikia ili kuweza kuchagua na kuchukua maamuzi sahihi, kama Qur'ani inavyosema:

*'Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.'* (Q22:46)

**4**



Qur'ani imetahadharisha kuhusu vizuizi vya mtu kutafakari. Qur'ani haikutosheka na kuhimiza matumizi ya viungo vya fahamu na akili zetu katika kubaini umuhimu wa kufuata amri za Allah Mtukufu. Lakini imetuzindua pia yale yanayotelezesha akili kwa kuzingatia kwamba akili ya mwanadamu huvutwa pande mbili upande wa kheri na upande wa shari. Jambo linalofanya matokeo kuwa tata ya kukosea na kuiacha haki baadhi ya nyakati kwa kupenda, kwa khofu au kwa kuhadaika.



> Waislam anaamini kwamba uumbaji wa Mungu hauwezi kupingana na dini yake, ambayo amewaagiza watu, basi ni kwanini kuogopa Masuali na kutumia Akili??

**Baadhi ya vikwazo vya tafakuri vinavyowekwa wazi na Qur'ani ni kama ifuatavyo:**

- **Kuiga:** hilo ni kwa sababu kurithi itikadi, tabia na desturi za kufikiri vibaya huweza kuathiri muundo wa mazingatio na kufikiri na hivyo kuwa vigumu kuikubali haki na kuiacha batili. Na huenda kufikiri kukaenda kombo kwa hoja kwamba haya ndiyo niliyozoea au nimezaliwa na kukuta haya yakitendeka. Kama Qur'ani inavyotusimulia kuhusu baadhi ya wale ambao haki imewadhihirikia na kule kuiga kukawazuia wao kuifuata, pale wanapoambiwa fuateni yale aliyoteremsha Allah Mtukufu wao husema tunafuata yale tuliyozoea, yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Hapo Qur'ani inaleta angalizo, 'Hivi watawafuata tu hata kama hawana muongozo wowote au hoja zilizo bayana kwa kuwa tu baba zao wanafanya hivyo?

*"Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?"* (2:170)

- **Ubishi na kiburi:** Hilo hutokea pale akili inapobaini ukweli wa jambo, lakini ikajizuia kuukubali na kuufuata kwa ajili ya kulinda maslahi fulani, hadhi au husda tu na dharau ya kile chanzo cha uongofu. Kama Allah Mtukufu Anavyosema ndani ya Qur'ani kuhusu aina ya watu ambao walikanusha haki iliyowekwa bayana mbele yao pamoja na kukiri ndani ya nafsi zao kuwa ni haki, hakuna kilichowazuia kuifuata isipokuwa kiburi na dhulma.

*"Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!"* (Q27:14)

- **Kuzama katika anasa:** Hutokea akili ikatambua jambo lililo sawa lakini ikakosa ushujaa wa kulichagua kwa sababu ya kuzama katika anasa. Qur'ani inatusimulia sisi mfano wa mtu aliyepewa elimu na maarifa, lakini badala ya kuvifanyia kazi katika maisha yake, akajivua kutokavyo na akafuata matamanio na maslahi yake ya muda mfupi. Na hayakuwa hayo ila kwa sababu ya kuzama katika anasa kwa kiwango ambacho hawezi tena kuchukua uamuzi uliyo sahihi.

*"Na wasomee khabari za yule ambaye Tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na Shet'ani akamuandama, akawa miongoni walio potea. Na Tungelitaka Tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara Zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari."* (Q7:175-176)

Wakati wote Qur'ani huhimiza watu kutumia akili zao vyema, kudadisi, kuchunguza, kutafakari na kuzingatia juu ya nafsi, ulimwengu na viumbe vilivyopo bila ya kutanguliwa na masharti yoyote ya kujidhalilisha kulikoshurutwishwa.

Kwa kawaida anaekimbia hoja za kimantiki huwa haziafikiani na mafunzo yanayopingana au yasiyoeleweka kwa urahisi. Lakini dini ya haki ni lazima iwe imetoka kwa Allah Mtukufu na haiwezekani kupingana na viumbe vya Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye Allah ndie alie waawekea watu sharia, basi kwa nini iwe inaogopa Masuala ya watu na kutumia Akili? *"Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote."* (Q7:54)


UISLAMU NI DINI
YA AMANI



Watu wengi hushangaa kutokana na yale yanayotangazwa katika vyombo vya habari, pale wanapofahamu kwamba amani ina nafasi ya kipekee katika Uislamu. Muislamu hukariri neno amani na kuhisi maana yake mara nyingi tu kila siku.

*As-salaam* (Mwenye Amani) ni Jina miongoni mwa Majina ya Allah Mtukufu. Na Pepo Yake akhera jina lake jingine ni Nyumba ya amani. Na salamu ya Waislamu inaanza kwa jina la amani. Na Swala pia humalizikia kwa Waislamu kutamka amani mara mbili, mara moja kulia na ya pili kushoto. Pamoja na tamko hilo linakusanya pia jina la Dini yenyewe, Uislamu ni amani na yaliyo katika maana ya amani na utulivu.



Kama Uislamu unaalika kunako amani na kuheshimu haki za viumbe wanyonge, wenye maarifa kidogo, Mtume -*Swallallaahu alayhi wasallama* anatufahamisha kwamba; *"Mwanamke mmoja aliingizwa Motoni kwa sababu ya kumtesa paka, yeye alimfunga mahali hadi akafa, hakuwa anampa chakula wala kumnywesha wala hakumuacha ale katika wadudu wa ardhini."* (Imamu Muslim 2242) na kwamba, "*Mwanamke mzinzi aliingizwa Peponi kwa sababu ya kumnywesha maji mbwa aliyekuwa na kiu."* (Imamu Bukhari 3280)



Uislamu umetoa mifano ya kustaajabisha na Sharia katika kuheshimu haki za watu na kuishi nao kwa wema. Bila ya kujali tofauti zilizopo katika dini au fikra, hata Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* akafikia hatua ya kumtolea kitisho yule mwenye kumdhulumu mtu asiyekuwa muislamu au kumuudhi au kumlazimisha kufanya kazi iliyo juu ya uwezo wake kwamba atakuwa mgomvi wake mwenyewe siku ya Kiyama (Imamu Abu Daud 3052).

Lakini pale Uislamu unapohimiza kuwapa amani watu wengine, kwa kweli kinachokusudiwa ni amani ya haki na uadilifu ambayo inampa kila mwenye haki, haki yake. Na ambayo inamzuia mwenye dhulma kuendeleza dhulma yake, na mporaji katika kupora kwake. Na si amani ya hadaa, inayompa mwizi haki ya kile alichoiba na kumridhisha mwenye nyumba kwa thamani ndogo.

Na itabaki lugha za kilaghai zisizoeleweka vyema na matangazo kupitia vyombo vya habari, ndiyo njia inayotumiwa na watu wengi kwa ajili ya kuuza bidhaa na riwaya za mitazamo ya kuwaelekeza watu kusiko na manufaa. Wanasahau kwamba kila tukio lina pande zaidi ya moja na kila kisa kina zaidi ya mapokezi. Na ni wachache katika watu walio tayari kubeba hamu katika kutafuta ukweli na kupambana na changamoto za matangazo ya kilaghai na upotoshaji wa habari ili wapate kuchimbua elimu kutoka katika vyanzo vyake halisi na kuhukumu mambo kwa vigezo sahihi, maudhui na uwiano.

## Na mbele yako ukweli wa kutafakari

> Watu wachache wanao beba hamu ya kuitafuta haki, na kupambana na propaganda ya vyombo vya habari ili kuchunguza na kupata uhakika kutoka kwa vyanzo vake,ili kuchukuwa uamuzi wa sawa na uwiano.



## Uislamu ndiyo dini inayoenea kwa kasi hivi leo

Hivi leo Uislamu unaenea kwa kasi ya kushangaza duniyani kote. Kuanzia Amerika, Ulaya, Afrika na Asia. Pamoja na udhaifu wa Waislamu katika harakati za kuhubiri dini kisasa, na usaliti wa vyombo vya habari vya kimagharibi katika juhudi za kuharibu haiba ya Uislamu kwa madai na maelezo potofu, na kutangaza mambo mabaya kuuhusu wakati hayana uhusiano wowote na Uislamu! Na tujiulize basi, kuenea kwake ni kwa sababu ya watu kulazimishwa au ni kwa sababu ya kutosheka na mafunzo yake na kwa hiyari?

Bila shaka ukweli unaoshuhudiwa na kila mchunguzi ni kwamba watu wanavutiwa na Uislamu kwa kuwa mafunzo yake kupitia Qur'ani huweka wazi ukweli unaoaminika kwa urahisi kupitia tafiti za kisayansi na hata simulizi za kihistoria. Uislamu ndiyo Dini pekee iliyo na maelekezo maalumu ya njia bora ya kustawisha maisha ya kijamii, kulinda haki za watu wengine na kuheshimu uhuru wao na maarifa yao. Na hayo ndiyo mambo yaliyo na athari kubwa katika nafsi za watu na hivyo wao kushawishika kuielekea Dini hii. Na hilo si kwa fadhila za Waislamu lakini ni kwa kuifanyia kazi kanuni ambayo Allah Mtukufu Ameisititiza ndani ya Qur'ani tukufu kwa kila aina ya uwazi, *"Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu"* (Q2:256)

## HIVI WATU WALILAZIMISHWA KUINGIA KATIKA UISLAMU


Historia imejaa ushahidi kwamba kwa muda mrefu binadamu walikuwa wakitumia nguvu ili kulazimisha rai zao na utawala wao kwa lengo la kuhakikisha kwamba wanapata maslahi yao. Historia imejaa mifano juu ya hilo kwa makundi yote yenye kujinasibisha na dini pamoja na madhehebu mbali mbali.

Kwa mfano historia ina kumbukumbu ya mauaji ya halaiki yaliyofanywa na wakurusedi kwa wakazi wa asili huko Andalusia (Hispania) wakati walipofika wanaojiita wakombozi na wahami kwenye ulimwengu mpya kiasi cha kasisi wa kihispania, Bartolomede, baada ya kushuhudia uchinjaji huo kusema, "kwa hakika hawakuwa wakimtazama mkazi ambaye ni mwenyeji kwa jicho la kibinadamu bali walikuwa wakiwatesa kuliko hata wanyama".

A Brief Account of the Destruction of the Indies by Bartolome de las Casas (Jan 1, 2009)

## WAISLAMU WALIFANYA VIPI PALE WALIPOHUKUMU MIJI MIPYA?

## Waislamu walitawala Andalusia (Hispania) kwa karne 8



Waislamu walikuwa watawala wa Hispania kutoka mwaka 781 na kuanzia 711-1492 ikawa ndiyo kituo kikubwa cha ustaarabu wa ulimwengu. Hakuna mnaswara aliyelazimishwa kuingia katika Uislamu, bali Uislamu ulilinda haki zao. Biashara zao zikastawi na vyeo vyao katika dola vikapanda na Waislamu wakaondoa dhulma waliyokuwa wakifanyiwa mayahudi kabla ya ukombozi, wa Uisalamu na kumbukumbu za kihistotria zimejaa ukweli huo.

Lakini wakati Esabella na Fernando walipowashinda Waislamu huko Hispania alizuwia kila kielezo cha Uislamu na zikaundwa mahakama za upekuzi kwa ajili ya kutoa adhabu kwa kila yule atakayepatikana na hatia ya kubaki katika Uislamu wake hata kama ni kwa kificho.

Waislamu wakafukuzwa na kutolewa katika majumba yao. Lakini jambo la kuzingatia hapa ni kwamba Waislamu walifukuzwa Hispania pamoja na mayahudi, na wao wakafuatana na Waislamu kwenda kwenye miji ya Kiislamu na huko wakapata makazi ya amani na maisha mazuri.

## Waislamu walitawala Misri zaidi ya miaka 1400 na wakati wote walilinda hadhi na haki za Waqibti waliokuwa wenyeji kwa muda wote wa utawala wao.




Waislamu walitawala Misri mwanzo wa Uilsmau Baada ya Amru Ibnul Aswiy, mmoja kati ya maswahaba wa Mtume - *Swallallaahu alayhi wasallama* kuikomboa, yeye hakuhifadhi dini yao na vitakatifu vyao tu, lakini aliwaokoa kutoka katika taabu, adhabu na kutengwa kulikokuwa kukifanywa na warumi dhidi yao. Kwa sababu ya tofauti katika madhehebu ya dini zao pamoja na kuafikiana katika baadhi ya mambo. Katika utawala wa Kiislamu, ukarejea kwa Waqibti uhuru wa dini yao na ibada zao, na wanafika hivi leo zaidi ya watu milioni tano.

**Waislamu walihukumu kwa uadilifu India kwa karibu miaka elfu moja na huku asilimia 80 ya wakazi wake si waislamu.**



Waislamu walitawala bara hindi kwa miaka inayokaribia elfu moja, waliwalinda watu wa dini nyingine na wala hawakuwazuwiya kufanya ibada zao. Wakaondoa dhulma kwa dini zilizokuwa zinabanwa. Na wanahistoria wote wanathibitisha kwamba Uislamu haukuenezwa kwa nguvu na wala hapana aliyelazimishwa kuingia katika Uislamu.


**Miji mikubwa yenye Waislamu wengi ulikoingia Uislamu bila vita au majeshi.**



Indonesia ndiyo mahali palipo na mkusanyiko mkubwa wa Waislamu katika mji mmoja, mji una wakazi zaidi ya milioni 250. Miongoni mwao Waislamu ni asilimia 87. Uislamu uliingia huko kwa sababu ya tabia nzuri na uadilifu wa wafanyabiashara wa Kiislamu walipofika huko katika karne ya sita Hijiriyya. Hapana jeshi lililopelekwa wala hapakuwa na umwagaji damu, isipokuwa baada ya kufika majeshi ya wakoloni wa Kireno, halafu Waholanzi na kisha Waingereza na wote hao ni wakristo.



# Uislamu na Hali ya baadhi ya Waislamu leo



Ni mgongano ulioje? Ni ukweli uliyo wazi kwamba Waislamu wengi hawafuati mafunzo ya Uislamu katika mengi ya mambo yao. Msiba ulioje! Kimsingi Uislamu unahimiza mambo mazuri na maadili mema katika maisha ya dunia, na kufanya mambo yaliyo na manufaa kwa wanadamu ikiwa ni pamoja na kuwalingania watu kunako Uislamu. Watu wanaotaka kujifunza Uislamu hushangazwa na matendo ya baadhi ya watu wanaojinasibisha na Uislamu kiasi cha kufikia hatua ya kujiuliza, ni upi ukweli wa Dini ya Kiislamu?

## Kubabaika huko kunatakiwa kufanyiwa tafakuri katika mambo yafuatayo:

- Si kila anayejinasibisha na Uislamu, kwa kuzaliwa au vinginevyo kuwa ni Muislamu. Kwa kuwa Uislamu si nadharia lakini ni utaratibu wa maisha unaomtaka kila anayehusika kuzingatia mipaka iliyowekwa na Allah-Mtukufu katika matendo yake. Kwa maana ya kufuata amri zote kama zilivyokuja kwa kufanya yale yanayohimizwa na kuacha yale yanayokatazwa. Hakuna njia ya mkato na kwa wale wasiofuata utaratibu huo wao ndiyo wale wanaoitwa wanafiki.

- Na ndiyo maana si kitu kinachokubalika kunasibisha makosa ya mtu anayejiita Muislamu na Uislamu kama ulivyofundishwa kwetu na aliye mtukufu wa daraja Mtume Muhammad-*Swalla llaahu alayhi wasallama*. Kama isivyofaa kusema ukatili na udhalimu wa Hitler ulitokana na dini yake. Au ya kwamba dini ya kikristo ni yenye kuhimiza mauaji ya watu wasio na hatia kama tunavyoshudia huko Palestina na kwingineko duniyani. Ambako kumeanzishwa vita kwa lengo la kukidhi maslahi ya kibiashara ya nchi za magharibi, ambazo wakazi wake wengi na hata watawala wake ni wakristo. Au kusema kwamba mtu asiye na dini ni lazima awe katili kwa kuleta mfano wa Joseph Stalin aliyeua watu milioni kadhaa kwa madai ya kipuuzi, kwa kuwa madai yote hayo ni mbali na haki.

> Haiwezekani kwa hali yeyote kunasibisha makosa ya watu na dini zao na madhehebu yao.




- Kihistoria Uislamu una nafasi iliyotukuka hasa tukizingatia taaluma na ustaarabu ulioenea ulimwenguni kote, ambao kimsingi chimbuko lake ni Uislamu. Ushahidi wa hayo umeenea kutoka mashariki ya India hadi magharibi ya Hispania, iliyokuwa njia ya ustaarabu kuenea Ulaya.

- Na bado athari yake ipo hadi leo hii. Uislamu ulikuwa ni mwanga na njia ya ustarabu ambayo tunaishi nayo hadi leo hii. Kama ambavyo kuna mifano mingi katika nchi ambazo zinajitahidi kukimbizana na maendeleo ya ulimwengu leo hii, mbali na mifano binafsi katika makonde yote ya elimu katika nchi nyingi ulimwenguni.

- Hakuna anayekataa ukweli wa elimu ya tiba, na kujizuwiya matibabu kwa sababu ya kujuwa tu kwamba baadhi ya madaktari ni wabaya. Na hakuna anayepiga vita elimu na kuwakataza watoto wake kusoma kwa kujuwa tu kwamba wapo walimu wanaoharibu sifa ya taaluma hii adhimu kwa matendo yao ya hovyo. Hivyo mazingatio ni kwa hakika ya jambo na si kwa mifano mibaya ya watu wanaojinasibisha nalo.

La kushangaza ni kuwa pamoja na vita vya kuupaka matope Uislamu vinavyoendelea idadi kubwa ya watu duniani kila kukicha wanaingia katika Uislamu. Kwa kuona taswira halisi na sahihi iliyo katika Qurani, Kitabu kilicho mwongozo kwa Waislamu.



> Hakuna yoyote atakaepiga vita masomo na kuwanyima watoto wake kusoma kwa sababu chuo Fulani wamefundisha vibaya au mwalimu Fulani amekuwa mbaya.

## Mtazamo Mpya

Ni mara ngapi umebabaika kuchukua maamuzi na kuikamata fursa kwa ajili ya maslahi yako. Hadi leo hii unaonekana bado upo kwenye babaiko hilo.

Na kwa hakika utukufu wa mwanadamu ni ule uhuru na uwezo wake wa kuchukua maamuzi kwa maslahi yake bila ya kuhofishwa na vitu visivyo halisi.

Mtu husifiwa na kuitwa shujaa kwa kuweza kupambana na changamoto na masaibu mbali mbali ikiwa ni pamoja na ushujaa wa kukiri kosa pale haki inapobainika kwake. Huu ni ushujaa dhidi ya ubinafsi na ghururi na baada ya hapo mtu huwa na amani katika nafsi na haiba yake.

Kama ulivyoipa nafsi yako fursa ya kuufahamu Uislamu kutoka kwenye vyanzo vyake, usiinyime fursa katika kutafakari kile ulichosoma.

Kama uzuri wa Dini umeanza kudhihiri kwako na unapenda kuendelea kutafuta na kuuliza kuhusu Uislamu, basi mbele yako kuna nafasi ya kutosha kuuliza na kupata ufafanuzi. Angalia kutokea hivi sasa kwa jicho jingine tofauti.




GLOBAL MAP





Bu kitabın tamamını okumuş olmanız bizler için son derece değerlidir. Zihninizde bazı soruların ortaya çıkması yahut katılmış olduğunuz ve katılmadığınız görüşleriniz olabilir. Sizlerden görüşünüzü, sorunuzu ve katılmadığınız noktaları dinlemek isteriz. Sizlerden tarafımıza ulaşacak her şeye gereken önem ile cevap vereceğiz hakkında söz veririz.


LAUNCHING CURiOSiTY JUST SCAN IT.!!

THISISLAM.net

Shirikiana nasi katika uzoefu wako

info@modern-guide.com

SWAHILI





- Hivi huoni umuhimu wa kuiona taswira sahihi iliyo bayana ya ubora wa Dini yenye kujadiliwa zaidi kwenye vyombo vya habari duniyani?

- Hivi huoni haja ya kutulia na kuitambua kwa kina Dini inayoenea kwa kasi duniani na inayo kubalika kwa haraka kwa mujibu wa takwimu za kimataifa

- Hivi wewe hupati raha katika kuvumbua na kuzifahamu tamaduni za watu wengine na falsafa zao kuhusu maisha, Dini, na ulimwengu unaotuzunguka?

- Je utaipa nafsi yako nafasi kwa ajili ya kutambua maarifa yaliyothibitishwa yahusuyo Dini ya Kiislamu kutoka katika vyanzo vyake vya asili, kisha uyahukumu kwa kutumia uwezo wako wa kufikiri na akili yako?

**Ikiwa unaona hilo ni jmabo muhimu au ni lenye kuvutia basi kitabu hiki chaweza kukusaidia kwenye jambo unalo litaka**

9 786039 140856

LAUNCHING CURiOSiTY JUST SCAN IT.!!

MODERN GUIDE

THIS IS ISLAM

THISISLAM.net